**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh’d Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Nane - Tarehe 26 Mei, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti, (Mahmoud Muhammed Mussa)alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**Nam. 75**

**Tatizo la Kutohudhuria Watendaji Wakuu wa Wizara Wakati Yanapoulizwa Maswali Barazani**

**Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny Mhe. Jaku Hashim Ayoub) -** Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla halijajibiwa swali kwanza naomba nimpongeze Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kuweza kutetea mali ya SMZ, lile shamba la Makurunge kule na hatimaye tarehe 30 mwezi wa Juni inawezekana SMZ ikapata hati miliki ya lile shamba. Kwa hivyo kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wapiga kura wa jimbo la Wawi natumia fursa hii kumpongeza sana Mhe. Jaku Hashim kwa kuweza kutetea ile mali ambayo miaka 40 hatujapata hati miliki, na hatimaye kesho kutwa tarehe 30 inaweza SMZ ikapata Hati miliki.

Baada ya maelezo hayo naomba swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub Nam 75 lipate majibu ya serikali hivi sasa.

Kwa kuwa miongoni mwa kazi za Baraza la Wawakilishi ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali. Na kwa kuwa njia moja ya kusimamia serikali ni kuiuliza maswali na kutoa majibu sahihi na ya uhakika kutoka serikalini. Lakini kuna tatizo la kutokuhudhuria watendaji Wakuu wa Mawizara wakati wa kujibiwa maswali hayo ambayo ni miongoni mwa wahusika wakuu katika utekelezaji wa majibu yanayotolewa.

a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazowafanya baadhi ya watendaji wakuu kutohudhuria wakati maswali yanapoulizwa.

b) Je, kutokuwepo kwa watendaji wakuu wakati yanapoulizwa maswali sio kukidharau chombo hiki.

c) Je, serikali itachukua hatua gani kuhakikisha watendaji dhamana wanakuwepo wakati maswali yanapojibiwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 75 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, inawezekana wapo baadhi ya watendaji Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanaoshindwa kuhudhuria wakati wa kipindi cha maswali na majibu hapa Barazani lakini sio kwa nia ya kudharau chombo hichi, ila baadhi ya wakati wanadharurika kutokana na kubanwa na majukumu ya kazi na wakati mwengine wanakuwa safarini nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla wako watendaji wetu wanawajibika ipasavyo katika kuwasaidia Viongozi (Waheshimiwa Mawaziri) kwa kuwatayarishia majawabu sahihi ya maswali yanayohusu Wizara zao. Hivyo hawana lengo la kukidharau chombo hiki Kitukufu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali itaendelea kuwakumbusha na kuwataka watendaji wa serikali kuhudhuria vikao vya Baraza vinavyowahusu, ili kuhakikisha matakwa ya Baraza la Wawakilishi yanatimizwa na wakati huo huo kujenga mashirikiano mazuri kati ya Baraza na watendaji wa serikali na serikali kwa jumla.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, mdogo wangu hapa Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Kwa kuwa Waheshimiwa Wawakilishi hutumia muda mwingi kufanya *thorough feasibility study* ya matatizo yaliyomo katika majimbo yao na hatimaye kuweza kutunga maswali kuiuliza serikali. Na kwa kuwa Mawaziri wetu hao ni wanasiasa na mara nyingi huwa wanatumia mawazo yao sana katika majimbo yao kwa wale wenye majimbo, na wale walioteuliwa na Mhe. Rais huwa wanatumia muda mwingi katika kumshauri Rais wetu. Haoni Mhe. Waziri kwamba kutokuwepo Makatibu wakuu katika *speaker's gallery* wakati maswali ya Waheshimiwa Wawakilishi yanajibiwa hapa, huoni kwamba ni kufanya khiyana kwa wananchi.

b) Kwa kuwa hufika wakati mwengine yakatokea masuala ya utendaji ambayo ikabidi Waziri awajibike na huku hatajwi Katibu Mkuu. Je, huoni kwamba kwa sasa kuna haja ya kwamba ikiwa Waziri limetokea tatizo la

utendaji badala ya kuwajibika Waziri wawajibike Makatibu Wakuu sasa, kutokana na uzembe kwamba hawaji katika *speaker's gallery* kusikiliza matatizo ya wananchi pale.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niwapongeze Waheshimiwa Wawakilishi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kufanya utafiti wa kina na matokeo yake kuisaidia serikali katika kutekeleza majukumu yake. Baraza hili limeonesha mfano mkubwa kwa kazi hiyo, kwa hivyo tunawapongeza sana Waheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli upo umuhimu wa watendaji wetu kuwepo katika Baraza hili hasa katika kipindi hichi cha maswali na majibu pale ambapo Wizara inahusika. Lakini kwa bahati watendaji wana utaratibu kama hawakuhudhuria wao wanaleta mwakilishi wao. Kwa hivyo tutazidi kuhakikisha kwamba ndani ya serikali jambo hilo linafanyika.

Naelewa majukumu mengine kama nilivyosema ndani ya jibu hili kwamba pia wana majukumu mengine makubwa ya kufanya katika shughuli za serikali, lakini nina wajibu wa kupata maoni ya Baraza hili ni ya muhimu sana.

Kwa hivyo tutaendelea kukumbushana ili pale watendaji watakapokuwa wana shughuli nyengine wahakikishe wale wanaowasaidia wengine wanakuwepo Barazani hapa kwa mujibu wa mahitaji ya Baraza na kwa mujibu wa shughuli zao zinavyowahusu, kwa maana ya mahitaji ya Baraza kwa wakati huo.

Hili ni kweli utaratibu usiofichika pale ambapo Waziri anawajibika kwa mujibu wa mambo ya kisiasa lakini vile vile na Katibu Mkuu anawajibika pale anapokwenda kinyume na utaratibu. Kwa hivyo linatizamwa kosa lilivyo, ikiwa kosa linawahusu wote wawili, wote wawili wanapaswa kuwajibika na ikiwa kosa chanzo chake ni Katibu Mkuu basi moja kwa moja anapowajibika Waziri ni vyema na Katibu Mkuu akawajibika ili kuonesha kufanya kazi kwa pamoja katika Wizara.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri sana yamenikosha.

Mheshimiwa utakumbuka kuwa Mhe. Rais anapounda Baraza lake au anapounda Ofisi zake huwaweka watu ambao na wasaidizi wake, Katibu huwa na Naibu Katibu na Wakurugenzi na wao huwa na wakurugenzi wengine wasaidizi.

a) Mheshimiwa huoni kuwa kutokutokea Katibu Mkuu je, Naibu Katibu Mkuu yeye hahusiki kuweza kuja kusikiliza masuala ambayo Wawakilishi wanakuja ku-*present* hapa.

b) Mheshimiwa kutokana na hali kama hii hatuoni Mheshimiwa tunaipunguza nguvu ya Ikulu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, utaratibu Makatibu Wakuu wamejiwekea pale ambapo ana shughuli nyengine inayohusu majukumu ya Wizara yake hutafuta mwakilishi wa kuwakilisha. Tabaan mwakilishi wa mwanzo wa kuwakilisha huwa Naibu Katibu Mkuu, lakini inapotokea pia Naibu Katibu Mkuu ana shughuli wakati huo, Katibu Mkuu hufanya uamuzi wa kutafuta mwakilishi ili kuiwakilisha wizara katika eneo hilo linalohitajika.

Kwa hivyo nataka nimuhakikishie Mhe. Mshimba tutazidi kutanabahishana ili pale penye uhitaji wa Baraza watendaji wetu wakuu hawa, kwa maana ya Makatibu Wakuu waweze kuziwakilisha Wizara zao hapa Barazani au kumleta mwakilishi ambaye atahakikisha anayachukua yale ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wanahitaji yakafanyiwe kazi.

Lakini kwa upande wa kuonekana kwamba kutohudhuria kwa baadhi ya watendaji hapa kunaondoa hadhi Ikulu hilo sio sahihi. Mheshimiwa Ikulu ina utaratibu wake, inafanya mambo yake na serikali inatekeleza utaratibu wake na majukumu yake yamegaiwa vizuri katika utarabibu huo wa kiserikali.

Kwa hivyo nataka nimuhakikishie Mhe. Mshimba, la msingi hapa ni wizara kuwajibika ipasavyo katika Baraza letu hili Tukufu, na vile vile watendaji nao kushiriki pale wanapohitajika kwa vile ambavyo Baraza litaona inafaa.

**Nam. 61**

**Nyumba ya SMZ Afrika Kusini**

**Mhe. Saleh Nassor Juma: Kny: (Mhe. Jaku Hashim Ayoub) -** Aliuliza:

Kwa muda mrefu SMZ imekuwa inamiliki nyumba nchini Afirika Kusini, nyumba hiyo ipo hadi hivi sasa lakini haina matunzo yoyote na hakuna mpango wa SMZ kuifanya nyumba hiyo kama chanzo cha mapato.

(a) Nyumba hiyo bado ipo katika miliki ya SMZ.

(b) Kama bado ipo katika miliki ya SMZ, kuna mpango gani wa baadaye katika nyumba hiyo.

(c) Nyumba hiyo kuachwa bila kushughulikiwa si sawa na kuiacha kupotea bure.

**Mhe. Waziri wa Fedha -** Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnamo mwaka 1996 ilinunua nyumba mjini Pretoria, Afrika ya Kusini kwa thamani ya Randi laki nane, na nyumba hiyo hadi hivi sasa inamilikiwa kwa asilimia mia moja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(b) Mhe. Mwenyekiti, mpango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao umo katika hatua za kukamilika ni kubadilishana nyumba hiyo na nyumba inayotumiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama Afisi ilioko Dar es Salaam karibu na Ikulu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kwa sasa nyumba hiyo inamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mpango huo utaifanya nyumba ya Afrika ya Kusini kutumika kwa shughuli za Kibalozi na kuwa chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Dar es Salaam kuendelea kutumika kwa shughuli za SMZ na kuwa mali ya SMZ.

(c) Mhe. Mwenyekiti, nyumba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilioko Afrika ya Kusini haijaachwa, inafanyiwa matengenezo madogo madogo kila inapobidi na inaangaliwa kila siku.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa katika kipindi hichi *transition* hii ya kabla ya kubadilishana kukaribia na kubadilishana ile nyumba ya SMZ pale tunaambiwa ilikuwa ipo na ilikuwa inafanyiwa matengenezo.

a) Je, Mhe. Waziri anaweza akatueleza kwamba nyumba ile kwa kipindi hichi ilikuwa ikikodishwa au fedha hizi za matengenezo zilikuwa zikitoka SMZ, na kama zilikuwa zikitoka SMZ ni kiasi gani zimetumika kufanyiwa ukarabati wa nyumba ile.

b) Na kama zimekuwa zikitoka SMZ ni kiasi gani zimetumika kufanyiwa ukarabati wa nyumba ile. Na kama imekuwa ikikodishwa ni kiasi gani cha Randi zimepatikana katika nyumba ile.

c) Kwa kuwa Pretoria ni *International Business Center* ukilinganisha na Dar-es-Salaam. Je, kwa kiasi gani wataalamu kutoka SMZ wamekwenda kule wakaiona ile nyumba na kuifanyia tathmini na kuja hapa Dar-es-Salaam wakafanya tathmini ya hii hapa Dar-es-Salaam, ikaonekana kwamba ilipo nyumba ya SMZ iliopo Pretoria ina kiasi hichi na ilioko Dar-es-Salaam ina kiasi hichi. Je, kazi hiyo imefanyikana au ni yale yale kwamba tunataka kutoa nyumba yenye thamani kubwa tupewe nyumba yenye thamani ndogo sisi.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kujibu maswali matatu ya nyongeza ya Mhe. Saleh Nassor Juma, Mwakilishi wa Wananchi wa jimbo la Wawi ambaye pia ni baba yangu, mzee wangu kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, nyumba ile haikuwa inakodishwa kule Afrika ya Kusini. Nyumba ile iliponunuliwa mwaka 1996 ilinunuliwa kwa lengo la kuifanya Ofisi ambayo itasaidia kuvutia wawekezaji kutoka Afrika ya Kusini kuja kuwekeza Zanzibar. Kwa hivyo lengo lake ilikuwa ni Ofisi, kwa hivyo haijawahi kukodishwa nyumba ile. Kwa hivyo hakuna mahesabu kwamba nyumba ile iliwahi kukodishwa.

b) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Nassor ametaka takwimu za fedha za matengenezo, na kwa kuwa sikuwanazo hapa, naomba nimjibu kwa maandishi hizo takwimu ni fedha ambazo tumetumia kuifanyia ukarabati ule mdogo mdogo.

c) Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Nassor na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwamba nyumba hizi mbili zina thamani tayari, nyumba ile ambayo tunataka tuichukue sisi Dar-es-Salaam na nyumba ile ya Afrika ya Kusini.

   Lakini nataka niwaambie kitu kimoja ndugu zangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na ndugu zangu Wazanzibari, tukishakubadilishana nyumba ile ya Afrika ya Kusini itakuwa ni nyumba inayomilikiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sisi Wazanzibari ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo lenye (a) na (b).

a) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina nyumba nyengine zozote ambazo wanazimiliki nje ya Tanzania?

b) Na kama zipo ni wapi na wapi.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti,

a) Ofisini kwangu sina kumbukumbu ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kumiliki nyumba nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, isipokuwa kabla ya Mapinduzi 1964 Serikali yetu ilikuwa inamiliki nyumba Uingereza, Egypt, lakini baada ya Muungano 1964, nyumba hizo tumezitoa kama ni sehemu yetu ili ziingie katika sehemu ya Muungano na zitumike na balozi zetu zilizoko nje. Kwa sasa sina kumbukumbu ya kumiliki nyumba nje ya Tanzania.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi asubuhi ya leo kuweza kunipatia nafasi kwa mara nyengine kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri kutokana na sheria ya Afrika Kusini kwa muda mwingi nyumba ambayo haina matengenezo huwa inataifishwa. Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa nyumba ilikuwa ikitengenezwa na Balozi wa Tanzania, na kama ni hivyo, kama unavyosema kuwa takwimu utatuletea kutokana na matengenezo haya. Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba ukweli uko wapi kati ya ukweli wako wewe na ukweli ambao walikuwa wakitwambia Ofisi ya Makamu wa Pili tulipokwenda ziara.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, hakuna tofauti baina ya maelezo yangu na maelezo yaliyowahi kutolewa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Hata kama Ofisi ya balozi ndio iliyokuwa ikifanya hayo matengenezo madogo madogo lakini ilikuwa ikifanya kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hivyo hakuna tatizo hapa ni yale yale tu kwamba matengenezo yote yalikuwa yakifanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyokuwa yakihitajika kwa nyumba ile alikuwa akifanya. Kwa hivyo kama balozi alikuwa akifanya, akifanya kwa niaba, kwa sababu ndio mwakilishi halali tuliomuweka kule kuiangalia hiyo nyumba. Kwa hivyo hakuna tofauti baina ya majibu yangu na majibu ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

**Mhe. Mwenyekiti**: Waheshimiwa Wajumbe tukumbushane jambo moja baada ya swali la msingi maswali yanayotakiwa ni mawili tu kwa mujibu wa kanuni. Kifungu cha 40(3) kinaelekeza maswali ya nyongeza ni mawili kwa mujibu wa Kanuni, angalieni Kanuni.

**Nam. 1**

**Wagonjwa wa Ukoma Kutengwa**

**Mhe. Mohammed Haji Khalid** - Aliuliza:

Zamani watu waliokuwa na ugonjwa wa ukoma walitengewa sehemu zao maalum za kuishi mbali na makaazi ya kawaida ya jamii, lakini katika miaka ya hivi karibuni wagonjwa hao wamesambaa katika maeneo mbali mbali hasa maeneo ya Darajani.

Je, kulikuwa na sababu gani zilizopelekea hapo zamani wagonjwa kutengwa na familia zao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:

Mhe. Spika, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote katika Baraza hili la Wawakilishi tukiwa kwenye afya njema na wazima.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kumjibu Mhe. Mohammed Haji Khalid Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mtambile swali lake Nam. 1 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hapo zamani watu waliokuwa wakigunduliwa na maradhi ya ugonjwa wa ukoma walikuwa wakiwekwa katika kambi maalum kwa ajili ya kupatiwa matibabu. Haya yalikuwa yanafanyika mpaka kati kati ya miaka ya 1990.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Unguja, wagonjwa hao walikuwa wakiwekwa pale Welezo, na kwa upande wa Pemba ilikuwa wanawekwa pale Makondeni.

Hali hii ya kuwatenga imeanza tangu enzi za zamani ulipogundulika ugonjwa huo kwa sababu kulikuwa hakuna dawa zenye uwezo mkubwa wa kuwatibu au kuwakinga na maradhi hayo, kwa hivyo kuwatenga ilikuwa ni namna moja ya kujaribu kupunguza maambukizi kwa jamii zao zilizokuwa zinawazunguka.

Mhe. Mwenyekiti, hata baada ya kupatikana dawa za kutibu hazikuwa na uwezo mkubwa wa kuponyesha na kupunguza maambukizi kwa jamii, hali iliyopelekea kupata ulemavu ambao umetokana na ukoma.

Hivi sasa wagonjwa wa ukoma hawatengwi tena, sababu dawa wanazotumia zina uwezo mkubwa wa kutibu na kuua vimelea kwa wingi na kwa muda mfupi kuanzia wiki mbili na hatimae kupunguza maambukizi katika jamii.

Mfano Mhe. Mwenyekiti, walipokuwa wanatengwa wagonjwa hao walikuwa wanatumia dawa za muda usiopungua miaka mitano hadi kumi na hali ya uponyeshaji ilikuwa mdogo sana.

Baada ya hapo dawa mseto zilitumika ambazo zina uwezo wa kukatisha maambukizi katika muda mfupi sana wa siku kumi tu hadi miezi mitatu na kuzuia maambukizi ndani ya wiki moja. Dawa hizo *Dapsone, Rifampisin, clofazimine* ambazo zote hutolewa chini ya msaada wa *WHO*.

Wakati mwengine *antibiotic* nazo pia hutumika kutibu maradhi haya. Mhe. Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba ukoma unaweza kusababisha ulemavu ikiwa mgonjwa hakugundulika na kutibiwa kwa wakati. Kwa maana hiyo watu wanaoonekana hapo Darajani kama Mhe. Mwakilishi alivyouliza au mitaani ni wale wenye ulemavu unaotokana na ukoma na hawana maradhi ya ukoma tena.

Kwa hivyo watu hao hawana uwezo wa kumuambukiza mtu yeyote kwa kuwa tayari walishatibiwa na hizo ni athari zilizobaki.

Mhe. Spika, inashauriwa na tunawaomba wananchi kutowatenga na kuwanyanyapaa wagonjwa wa maradhi ya ukoma au wale wenye ulemavu uliotokana na ukoma.

Pia tunaombwa tuielimishe jamii kwa wale wenye dalili kujitokeza mapema iwezekanavyo katika Vituo vya Afya ambazo dawa hizi za kutibu maradhi ya ukoma zipo na zinatolewa bila ya malipo, ili watibiwe mapema na kuepuka ulemavu unaotokana na ugonjwa huo.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu mazuri na marefu ya Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa kashauri kuwa jamii ielimishwe na isiwatenge hawa watu, je, ni dalili zipi zinazoonekana kujua kuwa dalili hizi ni za ugonjwa wa ukoma.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, dalili za mwanzo, maana haya maradhi yanakuwa mengi lakini dalili za mwanzo huanza kama punye

dogo kwenye ngozi hiyo ndio dalili ya mwanzo kabisa. Lakini punye lile linaweza kusababishwa na matatizo mengi sana au maradhi mengi sana lakini punye la maradhi haya ya ukoma huanzia kutokana na kupungua nguvu za kinga za mwili.

Linapoanza lile punye hugeuka likawa gumu na baadae likageuka rangi ya fedha, na linapogeuka rangi ya fedha hapo huingia ndani moja kwa moja kuathiri mishipa ya fahamu inakwenda sambamba na damu na ndio maana unamuona mgonjwa wa ukoma anaanza kuvimba kama vifundo kwenye mishipa yake, na hapo ndipo maradhi haya yanapoanza na baadae kuvamia moja kwa moja kwenye *soft tissues* ama *cartilage* kwenye mifupa na ndio maana vidole vinaanza kulika. Jina jengine anaitwa *bacteria* huyu mbali ya jina lake la asili ambaye anaitwa *basilar siliprae* jina jengine pia anaitwa *acid-fast basilli,* ambapo anakula viungo vyenye mifupa laini kama *acid* vile inavyokula, na ndio maana unaona wagonjwa wa ukoma wanalika viungo vyao.

Hizo ndio dalili kuu za maradhi haya yanapoanza na baada ya hapo husamba na kuathiri *system* nzima ya mishipa ya fahamu kama hajapata tiba kwa wakati. Lakini hadi kufikia *stage* hii ni ya mbali sana, naamini dawa huwa zitapatikana kabla.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Swali mama linasema hapo zamani watu waliokuwa na ugonjwa wa ukoma walikuwa wakitengwa lakini hivi sasa hawatengwi wanasambaa tu na hasa Darajani, hapa haikuelezwa kuwa wanatibiwa au vipi.

Swali je, kwa nini zamani walikuwa wanatengwa na sasa wanasambaa ovyo, haya mambo ya tiba yanakuja katika kujibu swali lakini humu kwenye swali mama halikutajwa. Je, hawa wagonjwa wa ukoma wanaotembea sana hivi sasa ovyo hawawezi wakasababisha hatari kutokana na majibu ya swali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, narudia tena Mhe. Mwenyekiti, hapo awali nilishajibu hilo na narudia tena wale wanaonekana sasa hivi si wagonjwa wa ukoma wameshatibiwa tayari ukoma, zile ni athari zilizobakia kutokana na maradhi ya ukoma.

Ukoma Mheshimiwa unaambukizwa kwa *respiratory tract fluids* yaani maji maji yanayotokana na hii *pipe* ya kuvutia pumzi, kwa hivyo maji maji hayo yanaweza kuwa kamasi, mate, makohozi, ukipiga chafya mate yakimrukia mtu ndio ukoma unaambukizwa kwa namna hiyo.

Hivi sasa hakuna tena maradhi hayo kwa sababu yakishaanza kujitokeza tu kwa dalili za mwanzo za kwenye ngozi huwa yanapata tiba moja kwa moja, na tiba hiyo inachukua siku kumi tu, kwa hivyo si rahisi kumkuta mgonjwa wa ukoma mitaani ama Darajani ama popote pale pengine.

Wale wagonjwa tunaowaona mitaani si wagonjwa wa ukoma, bali zile ni athari zilizobakia kutokana na maradhi ya ukoma, ukiwaona hivi zile ni athari ambazo zimetokana na ugonjwa wa ukoma.

La pili Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hapo awali kweli hii dawa imegunduliwa mnamo miaka 1980 kabla ya miaka 1980 nchi zilizoendelea zote nazo pia zilikuwa zinawatenga na kuwaweka wagonjwa wa ukoma katika *isolation,* yaani kambi maalum hawaruhusiwi kuchanganyika. Kwa sababu dawa hizi zilikuwa bado hazijagunduliwa, wakati huo zilikuwa zinatumika dawa zile *long therapy,* ambazo zinachukua miezi 6 hadi mwaka kumtibu mgonjwa wa ukoma. Lakini dawa za sasa ndani ya siku kumi kabla hajafikia kwenye ule ukoma wenyewe yule *bacteria* anakuwa anauliwa, na maradhi yale hayawezi kuambukizwa.

Kwa hivyo naomba nirudie tena tusiwatenge wale wala tusiwanyanyapae, kwa sababu wale tayari washapona zamani, na hivi sasa dalili ikionekana tu ya mwanzo ya lile punye linalotoka kwenye ngozi basi mgonjwa huyo hupatiwa matibabu ndani ya siku kumi kabla ya kufikia huo ukoma wenyewe wa kuambukiza. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Waziri ametunasihi kwamba wale watu waliosambaa Darajani na sehemu nyengine tusiwatenge jambo ambalo mimi ninalikubali sana, na hoja yake ni kwamba wale sio wagonjwa wa ukoma ni watu waliopata athari ya ugonjwa huo wa ukoma.

Hebu atwambie, mwananchi wa kawaida atajuaje kwamba yule hana athari za ugonjwa wa ukoma, je Wizara yake imefanya vipimo lini kututhibitishia kwamba wale watu waliosambaa mule ni walemavu tu lakini hawana maradhi ya ukoma.

Pili, ni nani aliowashauri wagonjwa wale, kwa sababu wale ni sehemu ya wanadamu, wanahitaji hifadhi ya msingi ya kibinadamu, nani aliowashauri kukaa barabarani pale wakiwa wagonjwa walemavu wa ukoma, huku wakiomba omba haoni wizara yake inachangia kuwashawishi waje pale kudhalilika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa hivi mimi kusimama hapa ni mojawapo ya jukumu letu kuwaelimisha wananchi.

Ninaamini kwa sisi wenyewe kuelimishana humu ndani ya Baraza la Wawakilishi kuhusu hao wagonjwa waliobakia na zile athari zilizotokana na maradhi ya ukoma pamoja na Wawakilishi wa wananchi wakiwa wanatusikia hiyo ni njia mojawapo ya kuwaelimisha kwamba wale si wagonjwa wa ukoma bali wamebakia na athari zinazotokana na maradhi ya ukoma.

Lakini wakati huo huo Wizara ya Afya inaendelea na jitihada mbali mbali kupitia vyombo vya habari, kupitia majukwaa mbali mbali ambayo yanatoa elimu kwa maradhi mbali mbali kutoa elimu hiyo.

La pili, naomba pia kumwambia Mhe. Hija wale tunaowaona Darajani wanaishi vizuri wana wake zao, wanafanya mapenzi vizuri na wanazaa watoto ambao hawana maradhi yale, hiyo ni ithibati tosha kwamba wale sio wagonjwa wa ukoma bali wamebakia na taathira za maradhi yale.

Lakini kweli ninakubaliana na wewe kuna wengine wanatumia *advantage* ya kuwa na maradhi yale kwa ajili ya kuomba, na haya si hapa tu hata ukienda kule Dar es Salaam pale mitaa ya Samora, mitaa ya Bibi Titi, ukienda mitaa ya Kariakoo utaona wengine wanakuwa wamekamata na mabakuli kabisa. Lakini wale wale wanakuwa na familia zao na wana watoto wengine wanafanya kazi, wengine wamesoma vizuri isipokuwa mtu anataka kutumia *advantage* ya ule ulemavu aliopata kutokana na maradhi ya ukoma.

Lakini kwa hivi sasa maradhi ya ukoma naweza kusema yakianza tu basi yanagunduliwa mapema kabla hayajaleta taathira katika jamii, wala kufikia *stage* hiyo. Sasa hivi hufikii tena *stage* ya kupata ulemavu, unafikia *stage* ya lile punye la ngozi tu, likishajulikana pale unafanyiwa *test* na vifaa vya ku-*test* vipo unapewa dawa. Ahsante sana.

**Nam. 35**

**Utoaji wa Huduma ya Umeme**

**Mhe. Saleh Nassor Juma: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) -** Aliuliza:

Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati siku ya Alhamis tarehe 12/2/2015 ilikuwa Ikulu na Watendaji wake katika mpango kazi wa Bango Kitita na vyombo vya Habari vimetangaza kuwa Waziri dhamana wa Wizara hiyo amesema Dira yake ni kuhakikisha wananchi wote wanapata maji na makaazi nafuu katika kipindi

cha Julai hadi Disemba 2014 yakiwemo mambo kadhaa, Sera ya Ardhi na Mradi wa Ukingo wa Bahari wa Forodhani. Vile vile Waziri amesema katika kipindi hicho kidogo tu, kuna vijiji 20 vimepatiwa huduma za umeme Unguja na Pemba.

(a) Je, kwa nini Wizara isivitaje vijiji hivyo 20 vilivyopatiwa umeme ili kujua ukweli wa Wizara hiyo.

(b) Na lini Wizara itashusha bei ya umeme wakati ndugu zetu Tanzania Bara wametangaza kushuka huduma hiyo.

(c) Kwa nini kusiwe na utaratibu maalum wa kuuza huduma ya umeme kwa madaraja ya watu wake kama nchi nyengine zilivyofanya kutokana na uwezo wao kuwa mdogo, huku wakiwa wanahitaji umeme wananchi waliokuwa wanyonge.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, vijiji vilivyobahatika kusambazwa umeme katika kipindi hicho kwa Unguja na Pemba ni kama hivi vifuatavyo:-

| **Unguja** | **Pemba** | |
|---|---|---|
| Dole Ndunduke | Banani | Michungwani |
| Dongongwe | Chanjaani Mtambile | Misooni |
| Fukuchani Mvuleni | Chanjamjawiri | Mzambarauni |
| Fuoni Michenzani | Gongo mawe | Sumbukae Ole |
| Fuoni meli tano | Jojo | Tironi |
| Ghana | Kifumbikai Wete | Tumbe |
| Kibele | Kivugo | Uondwe |
| Kilombero | Kwa Changawe | Wingwi kidodi |
| Kisauni | Likoni Kengeja | Wingwi mjanaza |
| Kwarara kwa Tobi | Manyaga | Wingwi mtakuja |
| Mwera mabatini | Maweni | Micheweni |
| Tunguu mji mpya | Maziwa ng'ombe | |
| | | |
| | | |

(b) Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi ya kwamba, bei ya umeme inayouzwa hivi sasa ni pungufu kwa shilingi 79 ukilinganisha na bei ambayo ilitakiwa itumike ili kukidhi gharama za uendeshaji wa *ZECO*. Ukilinganisha na punguzo ambalo limetolewa na *TANESCO* la shilingi 3 kwa kila *unit* moja.

(c) Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme ndivyo inavyofanya katika kuweka utaratibu maalum kwa ajili ya watumiaji wenye kipato cha chini, ambapo kwa mujibu wa utaratibu huo wenye kipato cha chini wanalipa shilingi 90 kwa *unit* moja kwa kulinganisha na watumiaji wa kawaida ambao malipo yao ni shilingi 222 kwa *unit* moja.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Kwa heshima kubwa naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa punguzo la umeme alilolitaja Mhe. Naibu Waziri ni la siku za nyuma sana, na kwa kuwa mara baada ya kuteremka bei ya mafuta hivi karibuni vile vile wenzetu wa Tanzania Bara wamepunguza bei ya umeme. Kwa kuwa Zanzibar inapata umeme wake kutoka Tanzania Bara, ni sababu gani za msingi ambazo zimesababisha hadi leo hii mara baada ya kupungua bei ya mafuta na umeme kupungua bei kwa huku Zanzibar bado hadi leo tunatumia bei ile ile ya umeme badala ya kupunguza kama ambavyo wenzetu wa Tanzania Bara wamefanya, jambo ambalo linaleta usumbufu sana kwa watu wa Muyuni na hata wa Jimbo la Wawi na majimbo mengine ya Zanzibar.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, bei ambayo tunauzia umeme *ZECO*, na ni sababu zipi ambazo zinasababisha kwamba kutokushuka zaidi ya hivyo, ni kwamba bado punguzo ambalo tumepunguziwa na *TANESCO* halijakidhi kushusha umeme zaidi ya hapo ukilinganisha na uendeshaji wa Shirika letu la Umeme *ZECO* kulingana na gharama za ununuaji wa vifaa na vyenginevyo.

Kutokana na kipindi hiki ambacho wametupunguzia kweli, lakini ni kiwango kidogo sana cha bei walichotupunguzia *TANESCO*. Kwa hiyo, hatuwezi kupunguza punguzo dhidi ya kiwango hicho ambacho tunachoendelea kwa sasa hivi.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, *ZECO* na *ZAWA* wote ni watoto chini ya Wizara ya Mhe. Waziri ambaye anajibu swali. Wazanzibari kwa muda mwingi wamekuwa wakikosa maji kwa sababu ya tatizo la gharama za umeme kwamba watu wa umeme wanakuwa na gharama kubwa, na *ZAWA* wameshindwa kulipia madeni hayo ya umeme. Kwa kuwa juzi Waziri wa Fedha amekuja na sheria ya kodi, kwamba sasa kila unaponunua umeme utatozwa kodi asilimia mbili ili kugharamia huduma za maji vijijini.

a) Je, kwa kuwa kodi hiyo itaanza tarehe 1 Julai, ni lini sasa wizara yako itaondosha mita za TUKUZA kwenye visima vya maji ili Wazanzibari wapate maji ya uhakika na kwa wakati wote.

b) Hivyo Mhe. Naibu Waziri nakumbuka Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi ilipitisha sheria ya mamlaka ya kusimamia masuala ya bei za umeme (*ZURA)*, ni lini sheria ile itaanza kazi ipasavyo ili Wazanzibari sasa wapate manufaa kama ambavyo Watanganyika wanapata manufaa kwa *EWURA*.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nikubaliane na yeye kwamba Shirika la Umeme *ZECO* na Mamlaka ya Maji *ZAWA* ni baba mmoja mama mmoja, kwa sababu inatoka wizara moja, hilo nakubaliana naye. Lakini pia nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi au nimkumbushe tu kwamba mita za TUKUZA ndani ya visima vya maji tayari zimeshaondolewa. Hili ni agizo la Mhe. Rais, ni kweli kipindi cha nyuma zilikuwepo mita za TUKUZA ndani ya visima vya maji, lakini baada ya Mhe. Rais kutoa agizo rasmi ni kwamba mita zimeshaondolewa na visima vyote vya maji sasa hivi vinatumia mita ya kawaida.

Na pia nataka nimjuilishe Mhe. Mwakilishi kwamba *ZAWA* na Shirika la Umeme hakuna tofauti yoyote, pia ni kweli kulikuwa na deni kupitia Mamlaka ya Maji (*ZAWA*), lakini deni hilo sasa hivi limebebwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, hakuna tofauti hiyo na hakuna tatizo lolote ambalo litalozuia wananchi kukosa huduma ya maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, pia suala la *ZURA* liko njiani na si muda mrefu tukijaaliwa *ZURA* itafanya kazi yake.

**Mhe. Panya Ali Abdallah:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi nilitaka nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa amevitaja vijiji ambavyo vimeshapelekewa umeme, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwa kazi kubwa na nzuri ya kuwapelekea wananchi umeme vijijini. Lakini pia nimuulize Mhe. Naibu Waziri

kuna vijiji vingapi ambavyo bado havijapata huduma hii ili sasa serikali ielekeze nguvu zake katika vijiji hivyo ambavyo havijapatiwa umeme ili nao wananchi waweze kufaidika na huduma hii kama wenzao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu kwanza na mimi nimpongeze kwa kuijua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama inafanya kazi vizuri ya kuwasambazia wananchi wake huduma hii ya umeme katika vijiji vyote vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, vipo baadhi ya vijiji ambavyo bado hatujavisambazia huduma hii, lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lengo lake ni kuvisambazia vijiji vyote ambavyo havijasambaziwa huduma hii. Kwa hiyo, vijiji vilivyobakia Mheshimiwa vipo vijiji vingi, lakini ningeomba tu labda aniambie kijiji gani na kijiji gani alivyovilenga ili nipate kumjibu vizuri.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaingia kwenye hotuba kumsikiliza Mhe. Waziri kwanza tuna wageni wetu ambao wamekuja kwa siku ya leo kututembelea hapa. Naomba tuwatambue.

Wageni wetu wa leo ni wageni wa Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Makunduchi, wageni hawa wanatoka katika Jimbo la Makunduchi na jumla yao ni wageni 45 wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Jimbo Bwana Hamdu Vuai Suleiman, ambapo ndani yake kuna wageni wa jimbo lenyewe, shehia, wadi na matawi, naomba wasimame ili tuweze kuwatambua. Ahsanteni kaeni kitako, hawa ni wageni wa Mhe. Haroun Ali Suleiman wamekuja kumuona namna anavyowasilisha hotuba yake hapa. (*Makofi*)

Lakini pia tuna wageni wa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, wageni hawa ni wanafunzi wa *Zanzibar Junior Academy* jumla yao ni wanafunzi 17 wakifuatana na walimu watano, wakiongozwa na Mwalimu Mkuu wa skuli hiyo Bibi Maryam Amour, naomba wasimame tuwatambue. Haya ahsante hii inadhihirisha kwamba Waziri huyu hashughuliki na masuala ya afya tu mpaka elimu pia mambo yake mazuri. Ahsante Mhe. Naibu Waziri. (*Makofi*)

Lakini tukimaliza hapo pia kuna na watendaji ambao wanaongozwa na Katibu Mkuu kwa wizara ambayo inasimamiwa na Maalim Haroun Ali Suleiman nao pia wamefika wote, nimeambiwa niseme wote wapo, *inshaallah* simameni tuwaone kidogo. Ahsanteni kaeni. (*Makofi*)

Sasa tunaendelea na shughuli zetu tutamkaribisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma Mhe. Haroun Ali Suleiman.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 – Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Baraza kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Kabla sijaendelea naomba nitangulize kutoa pole kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kufiliwa na dada yake mpenzi, inshaallah Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Na awape subra ndugu na jamaa wote.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa rehma, kwa kutujaalia uzima, hekima na afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kila siku na kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake katika kuiongoza Zanzibar.

Chini ya uongozi wake mahiri, serikali imetekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa wananchi wa Zanzibar wakati wa uchaguzi mkuu kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010.

Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha awamu ya saba chini ya uongozi wake, na ambayo yamefafanuliwa zaidi hapo chini, yamepelekea kukua kwa uchumi wa nchi yetu, kiasi cha kuwavutia washirika wa maendeleo kuendelea kuiunga mkono serikali yetu na wawekezaji kuendelea kuwekeza nchini.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi zangu za dhati zimwendee Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza shughuli mbalimbali za Umma. Pia, natumia fursa hii kumpongeza Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali, Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kusimamia vyema utekelezaji wa shughuli za Serikali. Hotuba aliyoitoa kwenye Baraza lako Tukufu wakati akiwasilisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2015/2016 ni kielelezo cha ukomavu wake katika uongozi, na imetoa muelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za serikali katika mwaka 2015/2016.

Mafanikio ya ofisi yetu kwa kiasi kikubwa yametokana na miongozo na maelekezo anayotupa ambayo yamesaidia sana katika utekelezaji wa majukumu tuliyopangiwa na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti Mhe. Ussi Jecha Simai Mwakilishi wa Jimbo la Chaani na Makamu wake Mhe. Abdalla Juma Abdalla Mwakilishi wa Jimbo la Chonga, kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano mzuri tulioupata wakati wa kupitia taarifa ya utelekezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015 na mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Ushauri na maelekezo ya kamati yametuwezesha kuandaa na kuwasilisha Barazani hotuba hii ya Bajeti. Wizara yetu itaendelea kuzingatia ushauri wa kamati hii wakati tukitekeleza malengo yetu kwa mwaka huu wa fedha na katika siku zijazo.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Waziri wa Fedha, Mhe. Omar Yussuf Mzee kwa hotuba yake ambayo imeainisha misingi na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Pia nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwa hotuba yake kuhusu Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, naishukuru sana familia yangu kwa msaada wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. Shukrani za pekee kwa wananchi wangu wa Jimbo la Makunduchi kwa kuendelea kuniunga mkono.

Aidha, naomba waendelee kuniunga mkono kwa lengo la kuimarisha maendeleo zaidi. Napenda kwa dhati kumshukuru Katibu Mkuu Ndugu Fatma Gharib Bilal na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Yakout Hassan Yakout kwa ushirikiano wao mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi yetu.

Pia napenda kuwashukuru Wenyeviti, Makamishna na Wajumbe wa Bodi, Kamisheni na Tume ya Utumishi, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Idara na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa utendaji na ushirikiano wao wanaonipa katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyonayo. Shukurani maalumu kwa Vyama vya Wafanyakazi kwa mashirikiano yao ya dhati wanayonipa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Katiba katika nchi zinazosimamia ujenzi wa demokrasia, amani na utulivu, nahisi nina wajibu mkubwa wa kuwapongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuanzisha Mchakato wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyopelekea kuundwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo imeratibu vizuri na kukusanya maoni ya wananchi ambayo hatimaye yalisaidia Bunge la Katiba kuandika "Katiba Inayopendekezwa".

Mhe. Mwenyekiti, hatua hii inaonesha nia ya dhati ya viongozi wetu wakuu katika kusimamia na kuimarisha Utawala Bora na Demokrasia nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwajaalia afya njema, busara na hekima katika uongozi wao, ili nchi zetu ziendelee kuwa na amani, utulivu na maendeleo endelevu.

Aidha, natoa ombi rasmi kwa viongozi na wananchi wote wapenda amani, kushiriki kikamilifu kutumia haki yao ya kupiga Kura ya Maoni wakati ukifika na kushiriki katika Uchaguzi Mkuu mwishoni mwa mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Spika kwa kuliongoza Baraza letu Tukufu kwa busara na hekima. Kazi nzuri anayoifanya hapa Barazani ni kielelezo tosha cha busara, hekima na uzoefu wake.

Nampongeza pia Naibu Spika Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini kwa kuendesha vyema shughuli za Baraza hili. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Baraza Mhe. Mgeni Hassan Juma Mwakilishi wa nafasi maalum na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kuendelea kumsaidia Mhe. Spika katika kuendesha vikao vya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba uniruhusu kwa dhati kabisa, kwa niaba ya Wizara na Jimbo langu la Makunduchi, nitoe mkono wa pole kwa familia na ndugu wa Marehemu kufuatia kifo cha aliyekuwa Mwakilishi mahiri wa Jimbo la Magomeni, Mhe. Salmin Awadh Salmin. Mungu ailaze roho ya Marehemu mahala pema Peponi. AMIN.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kutoa pole kwa wananchi wote wa Zanzibar kwa ujumla kutokana na maafa yaliyotokana na athari za mvua na kusababisha vifo vya wananchi mbali mbali na upotevu wa mali. Namuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira na ustahamilivu katika kipindi hiki kigumu cha maafa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile katika kipindi hiki tunachokaribia kumaliza, kikao hiki ndicho cha kumalizia miaka mitano yetu hapa Barazani, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote walioteuliwa na Mhe. Rais kuwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wawakilishi. Aidha, ninawapongeza viongozi na watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kipindi hicho. Naamini juhudi zao zimechangia sana kuleta ufanisi katika Baraza

na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba yangu itazungumzia maeneo makubwa manne ambayo ni: Muhtasari wa Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa Miaka Mitano iliyopita 2010 hadi 2015; Muhtasari wa Utekelezaji wa Malengo ya Kiidara na Taasisi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Muelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

## MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MIAKA MITANO

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuweka kumbukumbu, naomba uniruhusu nitumie fursa ya kikao hiki kueleza japo kwa ufupi matunda ya mafanikio yaliyopatikana angalau kwa kipindi hicho cha miaka mitano ya awamu ya saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika sekta mbali mbali kwa lengo la kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini. Utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi kwa miaka mitano kwa Zanzibar unaendelea kufanyika katika mazingira ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya ufunguzi wa Baraza la Wakilishi Novemba 2010, kwa upande wa Sekta ya Kazi na Utumishi wa Umma, Mhe. Rais wa Zanzibar alitoa ahadi mbali mbali zikiwemo kuongeza nafasi za ajira na kuimarisha maslahi ya wafanyakazi ili kujenga utumishi uliotukuka.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa fupi inatoa maelezo ya ufafanuzi wa Ilani ya CCM kama alivyoahidi Mhe. Rais kutekeleza katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 2010, ambapo Chama cha Mapinduzi kilishinda.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza ahadi hizo serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha mifumo ya Utumishi wa Umma inayozingatia Sera, Sheria na Kanuni za Kazi pamoja na mikataba ya utoaji huduma ili kuhakikisha kwamba inajenga mazingira mazuri kwa watumishi, na kuhakikisha watumishi wa umma wanatekeleza wajibu wao ipasavyo wa kuwatumikia wananchi

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha miaka mitano ya uongozi wa serikali ya awamu ya saba, serikali imeanzisha Wizara na Taasisi mbali mbali na imeweka taratibu na miongozo ya kusimamia Utumishi wa Umma ili kuimarisha mazingira bora ya kazi.

Jumla ya kanuni 12 za Sheria za Kazi zimetungwa na kuanza kutumika. Kanuni hizo ni za Sheria ya Ajira Nam.11, Sheria ya Mahusiano Kazini Nam. 1 zote za mwaka 2005 na Kanuni ya mwaka 2014 za Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011. Ofisi pia imekamilisha Sera ya Usafiri wa Watumishi wa Umma ya mwaka 2014 na Sera ya Serikali Mtandao ya mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa maslahi, mwaka 2011, serikali ilipandisha mishahara ya watumishi wa umma kutoka kima cha chini cha mshahara wa Shilingi 100,000/= hadi Shilingi 125,000/= kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimia 25. Serikali pia ilifanya marekebisho ya vianzio vya mishahara ya wataalamu mbalimbali wakiwemo Madaktari na Walimu wa Sayansi. Katika mwaka 2013, Serikali ilipandisha kima cha chini cha mshahara kutoka Shilingi 125,000/= hadi Shilingi 150,000/= sawa na ongezeko la asilimia 20 pamoja na kurekebisha mishahara ya watumishi wazoefu waliotumikia utumishi wa umma kwa miaka kumi na tano na zaidi ambao wana mishahara kati ya Shilingi 150,000/= hadi Shilingi 225,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na marekebisho hayo ya mishahara, serikali ilifanya mapitio ya maposho mbalimbali kwa nia ya kuongeza ufanisi katika Utumishi wa Umma. Katika hatua hii, serikali tayari imeidhinisha posho kwa Makatibu Muhtasi na Madereva wa viongozi, Mahakimu wa Mahkama za Mwanzo, Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Waendesha Mashtaka wa Ofisi ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Serikali pia iliruhusu maposho kwa Matarishi na Wakuu wa Masjala za Siri, Walimu Wakuu, Wakuu wa Vitengo, Walezi na Wahudumu wa nyumba za kulelea wazee na watoto yatima na watumishi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa. Aidha Madaktari Bingwa na Wasaidizi wao katika kada ya Afya wamepatiwa posho la “On call “ na posho la Mazingira hatarishi.

Serikali itahakikisha kuwa maslahi ya Watumishi wa Umma yanaimarishwa kutokana na utendaji wao wa kazi, ili yawe bora zaidi, kwa kuwaongezea mishahara na stahili nyengine kadri hali ya uchumi wetu inavyoimarika na kwa kuzingatia miundo ya utumishi mipya ambayo sasa iko tayari kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa sekta binafsi serikali imeweka kima cha chini cha mshahara kuwa ni Shilingi 145,000/= kutoka Shilingi 70,000/= cha mwaka 2010 ikiwa ni ongezeko la asilimia 107. Aidha, waajiri wamekuwa wakitekeleza agizo la Serikali na kuwapatia maposho wafanyakazi hao kwa mujibu wa aina ya kazi na uzoefu wao ili kuwapunguzia ukali wa maisha.

Mhe. Mwenyekiti, katika juhudi za kuimarisha uhusiano mwema kazini, ofisi imeanzisha Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Mambo ya Kazi ili kuharakisha maamuzi ya migogoro ya Kazi. Hatua hiyo imesaidia kupunguza

migogoro na mrundikano wa kesi katika mahakama ya kazi na kuongeza uzalishaji kwa maslahi ya Taifa ambapo jumla ya migogoro 317 imepokelewa, kati ya hiyo migogoro 214 imesuluhishwa, 48 imeamuliwa, 22 imefutwa, 23 imepelekwa mahkama ya Kazi na 10 inaendelea na hatua za usuluhishi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha vijana wanapata fursa za ajira, serikali imeanzisha mfumo wa taarifa za watafuta kazi (LMIS), imezindua Mpango Mkakati wa Ajira kwa Vijana wa mwaka 2014/2018 na imeanzisha mifuko mbalimbali ikiwemo mfuko wa uwezeshaji ili kuwapatia mitaji vijana ya kujiajiri.

Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, jumla ya vijana 19,758 walibahatika kupata ajira. Kati ya hao 5,667 waliajiriwa serikalini na kwenye mashirika ya umma, 7,256 waliajiriwa katika sekta binafsi na 6,835 waliajiriwa katika vyama vya ushirika. Aidha,
wapo wananchi waliojiajiri wenyewe baada ya kupata mikopo ambao ni 3,400 na wananchi 4,000 wamepata ajira zisizokuwa za moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuimarisha huduma za mawasiliano Serikalini, Serikali ilianzisha mradi wa serikali mtandao “e-government” uliozinduliwa mwaka 2013. Hadi hivi sasa, jumla ya majengo 53 yenye ofisi za serikali yameunganishwa katika mfumo wa serikali mtandao na tayari yameanza kupata huduma ya intaneti na mawasiliano ya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa, Ofisi imeweka mtambo wa CCTV katika jengo la Nyaraka na kuanza utekelezaji wa mradi wa kuzihamisha nyaraka katika mfumo wa elektroniki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuimarisha masuala mbalimbali yanayohusu wafanyakazi yakiwemo maslahi yao yanapatiwa ufumbuzi wa haraka, serikali imeamua kuyaweka pamoja masuala ya Kazi na Utumishi wa Umma chini ya Wizara moja Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma. Kwa kupitia utaratibu huu, watumishi wa umma na wafanyakazi wa sekta binafsi wanapata fursa pana zaidi ya kuwasilisha maoni yao na kupitia vyombo vyetu vya UTATU ambavyo vinaundwa kwa pamoja kati ya serikali, waajiri na Shirikisho la Vyama huru vya Wafanyakazi.

**MUHTASARI WA MATUMIZI NA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 7,084,758,950/= kupitia fungu 27, 47 na 48. Kati ya fedha hizo Shilingi

6,784,758,950/= zilikuwa kwa matumizi ya shughuli za kawaida, ambapo Shilingi 2,942,080,600/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 3,842,678,350/= kwa matumizi mengineyo na Shilingi 300,000,000/= zilipangwa kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi 2015 jumla ya Shilingi 4,898,349,003/= zilitumika kwa utekelezaji wa shughuli za kawaida, ambapo Shilingi 2,256,251,864/= ni malipo ya mishahara sawa na asilimia 77 ya makadirio na Shilingi 2,486,757,139/= ni matumizi mengineyo sawa na asilimia 65 ya makadirio. Kwa upande wa Kazi za Maendeleo Shilingi 155,340,000/= zilitumika sawa na asilimia 52 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma ilipangiwa kukusanya Mapato ya Shilingi 251,000,000/=. Hadi kufikia Machi 2015 wizara yangu ilikusanya Shilingi 227,489,900/= sawa na asilimia 91 ya makadirio. Mapato hayo yanatokana na Vibali vya Kazi kwa Wafanyakazi wa Kigeni, uthibitishaji wa Mikataba ya Kazi na Usajili wa sehemu za kazi kwa ajili ya Usalama na Afya Kazini. Angalia kiambatanisho nambari 1a, 1b na 1c.

**MALENGO MAKUU YA OFISI**

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais kazi na Utumishi wa Umma inaendelea kuwa na majukumu makuu yafuatayo:

i. Kuongeza upatikanaji wa fursa za ajira za heshima kwa wananchi hususan vijana.
ii. Kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kazi.
iii. Kuanzisha na kusimamia mipango endelevu ya upatikanaji wa rasilimaliwatu wenye sifa.
iv. Kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.
v. Kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu na Nyaraka.
vi. Kuhakikisha Wizara na Ofisi zote za umma zinafuata Miundo ya Utumishi.
vii. Kuimarisha Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na
viii. Kuimarisha usalama na afya kazini ili kuhakikisha hali bora ya usalama na afya katika sehemu za kazi.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu haya unasimamiwa na idara tisa, ofisi ya Afisa Mdhamini, kitengo cha Waziri na Taasisi nne.

Idara hizo ni:-

i. Mipango, Sera na Utafiti
ii. Uendeshaji na Utumishi
iii. Mipango ya Rasilimali Watu
iv. Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi
v. Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi,
vi. Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa,
vii. Teknologia ya Habari na Mawasiliano,
viii. Ajira,
ix. Usalama na Afya Kazini na
x. Ofisi ya Ofisa Mdhamini- Pemba.

Taasisi ni;

i. Kamisheni ya Utumishi wa Umma,
ii. Kamisheni ya Kazi,
iii. Tume ya Utumishi Serikalini na
iv. Chuo cha Utawala wa Umma.

**UTEKELEZAJI WA MALENGO KI-IDARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo ya utangulizi naomba kutumia fursa hii kutoa ufafanuzi wa mapitio ya taarifa za utekelezaji wa mpango wa bajeti wa Ofsi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

**Malengo ya Mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 idara hii ilipanga kuwajengea uwezo watendaji wake ili kuimarisha shughuli za mipango, ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Ofisi, ukusanyaji wa takwimu na uimarishaji wa mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; kuandaa Mpango Mkakati wa Sera ya Malipo na Sera ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa; kuandaa Mpango Mkuu wa Utafiti wa Ofisi na kuendelea na uratibu wa uanzishwaji wa mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar.

**Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 idara,

i Imeandaa rasimu ya Sera ya Malipo ya Watumishi wa Umma na kuwasilishwa kwa Makatibu Wakuu na maoni yaliyotolewa yanaendelea kufanyiwa kazi. Rasimu ya Sera ya Nyaraka na kumbukumbu za Taifa imekamilika na ipo katika hatua ya kuidhinishwa.

ii Imeandaa Mpango Mkuu wa Utafiti wa Ofisi, pia inaendelea na uratibu wa uanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya afya imeshampata mshauri elekezi na ameanza kukusanya taarifa za mwelekeo wa mfuko huo kifedha na huduma.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, idara imetumia jumla ya Shilingi 107,522,292/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 87,067,400/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 20,454,892/= kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa utekelezaji wa kazi za maendeleo Shilingi 155,340,000/= zimetumika.

## IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

### Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara ilipanga kuwajengea uwezo watumishi 35 ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; kuimarisha na kuweka mazingira mazuri ya kazi yatakayorahisisha utekelezaji wa kazi za wizara kwa wakati; kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na manunuzi wa wizara; kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli za wizara ili kuelimisha na kujenga taswira nzuri kwa umma na kuhakikisha haki na maslahi ya watumishi yanapatikana kwa wakati.

### Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 Idara,

i. Imewapatia wafanyakazi 24 wa Wizara mafunzo ya muda mrefu kati ya hao (wanawake 16 na wanaume 8), Aidha Idara imewapatia watumishi 10 (wanawake 5 na wanaume 5) fursa za mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. (Angaliakiambatanisho nam. 2a na 2b)

ii. Imesimamia vikao vya Kamati ya Uongozi, Kamati tendaji, Bodi ya Zabuni, Ukaguzi, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na vikao vya Washirika wa Maendeleo.

iii. Imetoa huduma mbali mbali za kiutawala na uendeshaji zikiwemo uwekaji wa mazingira bora, ununuzi wa vifaa, matengenezo ya jengo na zana na utayarishaji wa ikama.

Mhe. Mwenyekiti, Hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, Idara imetumia jumla ya Shilingi 603,679,795/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 391,579,155/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 212,118,640/= kwa matumizi mengineyo.

**OFISI YA WAZIRI**

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mhe. Waziri iliendelea na uratibu wa shughuli mbalimbali za kimaendeleo na kijamii za Mhe. Waziri. Ofisi imepokea wageni mbalimbali wakiwemo Balozi mdogo wa India, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kanda ya Afrika na Balozi mdogo wa Oman pamoja na wananchi wapatao 1,423. Aidha, ofisi iliratibu shughuli 10 ambazo waziri alishiriki kama mgeni rasmi. Miongoni mwa shughuli hizo ni mahafali ya Chuo Kikuu cha Zanzibar – Tunguu. Aidha, Mhe. Waziri alihudhuria mkutano wa Asasi ya Vijana ya Umoja wa Mataifa Tanzania na warsha ya mafunzo ya kimataifa ya mitaala katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha marehemu ABDUL RAHMAN BIN-SUMAIT – (Chukwani Zanzibar).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015 waziri alifanya safari za kikazi katika nchi mbalimbali ikiwemo Ethiopia, Geneva – Switzerland, Zimbabwe, U.A.E na India. Safari hizo zimekuza uwakilishi wa Zanzibar katika Jumuiya ya Kimataifa na kuimarisha mahusiano kati ya Zanzibar na nchi hizo katika Sekta ya Kazi na Utumishi, kutafuta fursa zaidi za mafunzo na ajira kwa vijana.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo cha habari ambacho kipo chini ya Afisi ya Mhe. Waziri kinachoshughulikia habari na mawasiliano, kwa mwaka 2014/2015 kimerusha vipindi 10 vya televisheni na 2 vya redio kuhusu Sheria ya Usalama na Afya Kazini na changamoto kuhusu ajira. Jumla ya taarifa 21 za redio, 8 za TV na taarifa 10 zilitolewa katika magazeti kuhusiana na shughuli mbalimbali zinazohusiana na wizara.

Aidha, Mhe. Waziri ameimarisha mahusiano na wananchi mbalimbali wa Zanzibar kwa kutimiza ahadi mbalimbali alizozitoa za fedha na vifaa ili kutatua kero zinazowakabili
wananchi.

## IDARA YA MAFUNZO NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

### Malengo ya mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, idara ilipanga kusimamia na kuratibu mafunzo ya watumishi wa umma kwa kada mbalimbali yanayotolewa na washirika wa maendeleo; kuratibu upatikanaji wa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 150 na watumishi 15 mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi; kuendelea na utafutaji wa fursa zaidi za masomo kwa Watumishi wa Umma kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ili kuongeza idadi ya wataalamu nchini.

Mhe. Mwenyekiti, pia idara ilipanga kuandaa na kuendesha mafunzo mafupi kwa kada zilizo chini ya utumishi pamoja na kusimamia mafunzo ya awali ya miongozo na maadili ya kazi kwa watumishi wapya watakaoingia katika utumishi wa umma; kuendesha mafunzo mafupi ya viongozi wa ngazi mbali mbali na kukamilisha tathmini ya mahitaji ya mafunzo ya watumishi na kutoa mafunzo kwa watumiaji hususan maafisa mafunzo na maafisa utumishi.

### Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 idara,

i. Imeratibu mafunzo ya watumishi wa umma kwa kada mbalimbali yanayotolewa na Washirika wa Maendeleo ikiwemo Indonesia, Korea, China, India na Japan. Ambapo jumla ya watumishi 113 wamepatiwa fursa hizo. Kati ya hao 94 mafunzo ya muda mfupi na 19 mafunzo ya muda mrefu.

ii. Imeratibu mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi kuhusiana na usimamizi wa kumbukumbu na Nyaraka za Taifa kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma na Idara ya Nyaraka, jumla ya makarani 25 wamepatiwa mafunzo hayo.

iii. Katika kuongeza fursa za mafunzo Idara imefanya mazungumzo kwa nyakati tofauti na Ofisi za Ubalozi wa Indonesia, Japan na wakala wa Ubalaozi wa Australia nchini Tanzania.

iv. Imeandaa muongozo wa kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo “Training Needs assessment guideline” utakaotumika kukusanya mahitaji ya taarifa za masomo za watumishi na kusaidia kuandaa mpango mkuu wa mafunzo.

v. Kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma imeandaa mafunzo mafupi kwa kada ya karani masjala. Jumla ya makarani 25 walihudhuria mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, idara imetumia jumla ya Shilingi 71,898,350/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 63,733,200/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 8,165,150/= kwa matumizi mengineyo.

## IDARA YA MIPANGO YA RASILIMALI WATU

### Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, idara ilipanga kutoa mafunzo kwa Maafisa Utumishi na Maafisa Utumishi Wasaidizi juu ya utayarishaji na utekelezaji wa mpango wa miaka mitano na mwaka mmoja mmoja wa rasilimaliwatu katika utumishi wa umma; kuratibu utoaji wa taaluma kwa maafisa waandamizi wa Wizara 16 juu ya kuwaandaa kushika nafasi mbali mbali za uongozi katika Taasisi za Umma "Succession Plan"; kufanya mapitio ya Ikama "Norminal Roll" ya mwaka 2014/2015 na kuidhinisha Ikama ya mwaka 2015/2016; kukusanya taarifa za kiutumishi na kuziingiza katika mfumo wa Elektroniki "Human Resource Database" na kushiriki katika mkutano wa Kimataifa wa Utawala wa Umma na Uongozi (AAPAM) utakaofanyika nchini Ethiopia.

### Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 idara,

i. Imeandaa mafunzo kwa Maafisa Utumishi na Maafisa Utumishi Wasaidizi juu ya utayarishaji na utekelezaji wa mpango wa miaka mitano na mwaka mmoja mmoja wa rasilimali watu katika Utumishi wa Umma kwa Taasisi za Umma.

ii. Imeandaa Muongozo wa Mpango wa Urithishaji Uongozi "Succession Plan" katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuziwezesha Taasisi za Umma kukabiliana na changamoto ya kuwatayarisha watumishi kujaza nafasi zinazoachwa wazi kutokana na sababu mbalimbali.

iii. Imefanya vikao 16 vya kujadili Ikama "Norminal Roll" ya mwaka 2014/2015 na kuidhinisha Ikama ya mwaka 2015/2016 kwa wizara zote 16. Jumla ya nafasi mpya za ajira 2,376 zimeidhinishwa. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya watumishi 401 wanatarajiwa kustaafu kazi kwa kufikia umri wa lazima. Pia imefanya vikao vinne vya Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa Wizara zote ili kujadili masuala ya Kiutumishi.

iv. Imeshiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa Utawala wa Umma na Uongozi (AAPAM) uliofanyika Nchini Morocco badala ya Ethiopia kwa lengo la kujifunza mbinu mbalimbali za Kiutumishi na Kiutawala.

v. Imewapatia mafunzo maafisa utumishi na wasaidizi maafisa utumishi juu ya uingizaji na uhakiki wa Taarifa za Watumishi kwa njia ya elektroniki. Pia imebadilishana uzoefu na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa umma juu ya kuimarisha mfumo wa uwekaji wa taarifa za watumishi kwa njia ya elektroniki.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, idara imetumia jumla ya Shilingi 107,845,021/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 83,159,200/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 24,658,821/= kwa matumizi mengineyo.

**IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI**

**Malengo ya Mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015 idara ilipanga kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miundo ya Utumishi kwa Wizara na Taasisi zote za Umma ambazo hazijakamilisha zoezi la kuwapanga watumishi wake kwa mujibu wa Miundo ya Utumishi; kukamilisha uingizwaji wa taarifa za watumishi kwenye mfumo wa malipo ya mishahara “Pay Roll System”; kufanya mapitio ya mishahara na malipo mengine ya watumishi wa umma na kukamilisha muongozo wa kufanya tathmini ya uchambuzi wa kazi na madaraja “Job Evaluation and Grading”.

Mhe. Mwenyekiti, idara pia ilipanga kutoa elimu kwa watendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu Kanuni za Utumishi wa Umma iIi kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu pamoja na kufanya tathmini ya idadi ya watumishi wa umma na mahitaji ya taasisi “Staffing Levels”; kuendelea na kazi ya kutoa taaluma ya utayarishaji wa Mkataba wa utoaji huduma kwa mteja kwa Wizara 11 na Taasisi zilizobakia na kufanya ufuatiliaji kwa Wizara zilizopatiwa mafunzo ya uandaaji wa mkataba huo pamoja na kufanya ziara nje ya nchi kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo maafisa kuhusu mambo mbalimbali ya kiutumishi.

**Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2014/2015**

Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 idara,

i. Imefanya utekelezaji wa kuwapanga watumishi katika Miundo ya Utumishi “Scheme of Service” kwa wizara 14. Hatua za ukamilishaji wa Wizara

mbili zilizobakia zinaendelea. Ni mategemeo ya Wizara hii kwamba mwanzoni mwa mwaka mpya wa fedha 2015/2016 watumishi wote watakuwa wamepangwa katika madaraja yao kwa mujibu wa Miundo ya Utumishi.

ii. Imefanya mapitio ya Posho mbalimbali zinazotumika sasa kulingana na gharama za maisha. Posho hizo zinajumuisha posho za safari za ndani na nje ya nchi, Posho za mazingira maalum, Posho za Maafisa Sheria, Makatibu wa Mawaziri na Watumishi wa SMZ waliohamishiwa Tanzania bara.

iii. Imefanya marekebisho ya mishahara na kutengeneza vianzio vipya vya mishahara kwa taasisi za CAG, DPP na AG.

iv. Imefanya marekebisho ya mishahara kwa Watumishi wazoefu wa muda mrefu. Marekebisho hayo yaliwajumuisha Watumishi wenye uzoefu kuanzia miaka 15 na mazingatio maalum ya marekebisho kwa walimu wenye uzoefu wa miaka 30. Hadi sasa jumla ya walimu 900 kutoka Unguja na walimu 650 kutoka Pemba wamefanyiwa marekebisho.

v. Imetoa mafunzo juu ya utaarishaji Mkataba wa utoaji huduma kwa Mteja kwa Wizara 15. Wizara saba zimeshatayarisha Rasimu ya awali na kuwasilisha Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi Umma kwa kupatiwa muongozo wa kitaalam. Mashirika ya Umma Mamlaka ya Viwanja vya ndege, Wakala wa Barabara nao pia wamepatiwa mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, idara imetumia jumla ya Shilingi 120,559,440/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 92,618,700/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 27,940,740/= kwa matumizi mengineyo.

## IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

### Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, idara ilipanga kutayarisha mfumo wa uhifadhi wa Nyaraka kwa njia ya elektroniki; kutayarisha mgawanyo wa majalada “File Classification” na daftari la uhai wa kumbukumbu “Retention Schedule” kulingana na majukumu ya msingi ya Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi za Umma; Kuimarisha mfumo bora wa usimamizi wa kumbukumbu, kutoa mafunzo ya mfumo wa usimamizi wa Kumbukumbu kwa wafanyakazi wa masjala na wasimamizi wa kumbukumbu kwa Wizara 11 zilizobakia na Kufanya ukaguzi wa kumbukumbu na Nyaraka katika Taasisi na Mashirika ya Umma.

**Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 idara,

i. Imefunga mtambo wa CCTV katika jengo la Nyaraka ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nyaraka. Kazi ya uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu kwa njia ya elektroniki inaendelea, ambapo majalada 69 yamehifadhiwa (Angalia kiambatanisho Nam.3a). Aidha, uhuwishaji wa nyaraka zilizokuwa katika hatari ya kuharibika umefanyika (Angalia kiambatanisho Nam.3b).

ii. Imetoa huduma kwa watafiti 361. Kati ya hao Watanzania 319 na wageni 42. (Angalia kiambatanisho Nam.3c).

iii. Imefanya ukaguzi wa kumbukumbu pamoja na utoaji wa mafunzo mafupi ya usimamizi wa kumbukumbu kwa Taasisi za Umma 34.

iv. Imetoa huduma za kiutawala na Uendeshaji ikiwemo, kuandaa kikao kimoja cha Bodi ya Ushauri wa Nyaraka na Kumbukumbu, kuwapatia watumishi stahili zao na kufanya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, idara imetumia jumla ya Shilingi 236,439,117/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 171,877,582/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 64,561,535/= kwa matumizi mengineyo.

**IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO**
**Malengo ya Mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, idara ilipanga kutoa miongozo itakayowezesha Taasisi za Serikali kuwasiliana kwa mfumo wa data na sauti; kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake ili kuwajengea uwezo kulingana na ukuaji wa teknolojia ya Habari na Mawasiliano; kutayarisha vipindi vya elimu kwa wananchi na kuvirusha hewani kwa kupitia shirika la utangazaji ZBC na kufanya ziara katika Wizara 16 Unguja na Pemba; kuanzisha “domain” ya Serikali ili iweze kutumika katika tovuti ya Serikali, barua pepe za watumishi wa Serikali na huduma za kielektroniki “e-services”.

Mhe. Mwenyekiti, idara pia ilipanga kufanya mapitio ya Sheria ya “Evidence Act and Criminal Proceeding Act” na kuanzisha Sheria zitakazosimamia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; sheria hizo ni; “Cyber Crime Act” na “Data Protection Act” na kuhamisha mfumo wa kumbukumbu za watumishi (HRM) na mfumo wa malipo ya mishahara kwa wafanyakazi “Pay Roll” na kuziweka katika kituo kikuu cha Mfumo wa taarifa “Data Center”

**Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara

i. Imeanzisha barua pepe za wafanyakazi wa serikali ambazo zimeshaanza kusambazwa kwa baadhi ya watendaji wakuu wa serikali ili kurahisisha mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali na kupunguza gharama za utumiaji wa karatasi pamoja na utoaji wa barua baina ya Taasisi.

ii. Imenunua vifaa mbalimbali kwa ajili ya uunganishwaji wa Taasisi na mkongo wa Taifa. Jumla ya Taasisi 53 zimeunganishwa na mkongo wa mawasiliano kwa upande wa Unguja. Aidha, Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kushirikiana na Idara ya mawasiliano, ZTE na kampuni ya Zantel zinaendelea na zoezi la kuziunganisha Taasisi za Pemba ili nazo ziweze kupata huduma za Serikali Mtandao.

iii. Imefanikiwa kutoa mafunzo ya awali kwa teknolojia mpya kwa wafanyakazi 14, mfanyakazi mmoja anaendelea na shahada ya pili nchini Korea na mfanyakazi mmoja amepata mafunzo ya ndani ya "cyberoam".

iv. Imefanya ukaguzi katika kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa "data center"

ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Teknolojia na kukidhi viwango vya usalama vya kimataifa "ISO". Aidha, imeratibu vikao Saba vya Kamati ya Usimamizi na vikao vinane vya Kamati ya wataalamu.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, Idara imetumia jumla ya Shilingi 384,343,606/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 174,360,400/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 210,183,206/= kwa matumizi mengineyo.

## IDARA YA AJIRA

**Malengo ya Mwaka 2014/15**

Mhe. Mwenyekiti, idara ilipanga kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za soko la ajira; kuimarisha shughuli za ukuzaji wa ajira nchini; kuimarisha mashirikiano baina ya serikali na Sekta Binafsi katika masuala ya kukuza ajira nchini na kuzalisha ajira zipatazo 2,000 kwa vijana kwa kushirikiana na sekta binafsi.

**Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara,

i. Imesajili Watafuta kazi 384 (wanaume 187 na Wanawake 197) katika mfumo wa ukusanyaji wa Taarifa za Ajira, kati yao 170 ni kutoka Pemba.

ii. Imezindua mfumo wa Taarifa za watafuta kazi ambapo Mipango mikuu ya Serikali inayohusu ukuzaji wa Ajira, Sheria, Sera, na kanuni za Taasisi mbalimbali ambazo zinatoa taarifa kuhusu ukuzaji wa Ajira zimewekwa katika mfumo huu. Aidha taarifa za ripoti mbalimbali zinazohusu nguvu kazi zimewekwa kwenye Mtandao huo ambazo zinaweza kutumiwa na wananchi.

iii. Imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo ya kukabiliana na Usaili, uwezo wa kujiamini na matumizi ya LMIS kwa vijana 100 (wanawake 35 na wanaume 65) wa Unguja na Pemba.

iv. Imeshiriki mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa inayohusu ukuzaji wa ajira ikiwa ni pamoja na mkutano wa mashirikiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar na mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoandaliwa na Shirika la Kazi Duniani na Umoja wa Mataifa.

v. Kwa kushirikiana na washirika wa masuala ya kazi imeandaa mikutano miwili iliyowashirikisha Wakala saba waliosajiliwa juu ya masuala ya ukuzaji na usimamizi wa ajira katika sekta binafsi na Taasisi za Umma. Fursa za Ajira 934 zimepatikana katika sekta binafsi. Kati ya hizo 365 ni ajira za ndani ya nchi na 569 ni ajira za nje katika nchi za Oman, Saudi - Arabia, Kuwait, Uturuki, Itali na Dubai.

vi. Imechapisha mpango wa miaka minne wa Utekelezaji wa Ajira kwa vijana wa 2014 - 2018. Idadi ya nakala 570 zimesambazwa kwa Wizara na Taasisi za Serikali, Wilaya za Zanzibar, Washirika wa Masuala ya Kazi, Washirika wa Maendeleo, Shirika la Kazi Duniani na VSO & SHELL.

vii. Kwa kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, Tume ya Mipango na VSO & SHELL iliandaa matamasha mawili yaliyowashirikisha na kuwaunganisha waajiri na watafuta kazi. Aidha, jumla ya Makampuni 30 yalishiriki katika tamasha la Unguja na watafuta kazi zaidi ya 1,500. Kwa upande wa Pemba makampuni binafsi 17 yalishiriki na vijana 800 watafuta kazi walishiriki.

Mhe. Mwenyekiti, Hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, Idara imetumia jumla ya Shilingi 70,253,701/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 57,978,000/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 12,275,701/= kwa matumizi mengineyo. Pia Idara imekusanya jumla ya Shilingi 14,900,000/=.

## IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

### Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, idara ilipanga kusimamia utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini kwa kufanya ukaguzi katika maeneo 180 na kusajili taasisi 140; kusimamia sehemu za kazi ili kuhakikisha kuwa zinafuata na kutekeleza Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usalama na Afya Kazini; kuimarisha uwezo wa Idara ya Usalama na Afya Kazini ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuimarisha ushirikiano na uratibu wa masuala ya Usalama na Afya Kazini na kukuza uelewa kwa waajiri, wafanyakazi na jamii juu ya Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini.

### Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 idara,

i. Imekagua sehemu za kazi 142 na kutoa miongozo kwa waajiri na waajiriwa juu ya umuhimu wa kuweka mazingira bora ya Usalama na Afya Kazini.

ii. Ukaguzi kwa ajili ya Usajili umefanyika kwa sehemu 124 za kazi.

iii. Imetayarisha vipindi 11 vya Radio na 4 vya Televisheni na kurushwa hewani kupitia ZBC Radio na ZBC TV, Hits FM na Bomba FM. Vipindi hivyo vilihusiana na ufafanuzi wa sheria nam. 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini.

iv. Kamati ya Usalama na Afya Kazini imeendelea kuishauri Idara juu ya masuala ya Usalama na Afya Kazini. Vikao viwili vimefanyika na kupitia Miongozo, Sera na masuala tofauti ya Usalama na Afya Kazini. Maelekezo ya kamati yamesaidia kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa majukumu ya Idara.

v. Imeshiriki katika Mkutano wa kupitia Muongozo wa Usalama na Afya Kazini kwa wafanyakazi wa vyombo vya baharini. Muongozo huo umekubaliwa na wawakilishi wa waajiri, waajiriwa na Serikali na unatarajiwa kupitishwa katika mkutano wa baraza kuu la ILO wa mwaka huu Geneva.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, idara imetumia jumla ya Shilingi82,281,360/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi62,435,200/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi19,846,160/= kwa matumizi mengineyo. Pia idara imekusanya jumla ya Shilingi25,740,000/=.

**OFISI KUU PEMBA**

**Malengo ya Mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi Kuu Pemba ilipanga kuratibu mafunzo kwa maafisa utumishi wa Wizara zote 16 juu ya utayarishaji wa mpango wa miaka mitano wa rasilimali watu na kushiriki katika vikao 16 vya kujadili nominal roll; kuratibu mafunzo ya utayarishaji wa Mpango wa Urithishaji Uongozi "Succession Plan"; kutoa mafunzo ya Usalama na Afya katika sehemu za kazi kwa taasisi 40 binafsi na taasisi 40 za Umma; kufanya ukaguzi wa usalama na afya katika sehemu 60 za kazi; kufanya uchunguzi wa ajali na maradhi katika sehemu za kazi; kufanya ukaguzi maalumu na kusajili sehemu 40 za kazi na kuratibu mkutano wa ushirikiano ya masuala ya Usalama na Afya Kazini.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi pia ilipanga kuratibu mafunzo juu ya kuongeza ufanisi "Perfomance Improvement" kwa maafisa utumishi na maafisa wa masjala; kuendelea kuwalipia gharama za masomo pamoja na kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji kwa ofisi; kufanya ukaguzi wa utunzaji na utumiaji "Baseline Survey" wa kumbukumbu katika Taasisi tatu za Serikali; kuondosha mrundikano wa kumbukumbu mfu "Decongestion"; kuandaa mkutano kwa wakuu wa Taasisi na Maafisa wa Masjala kwa Taasisi tatu zitakazofanyiwa ukaguzi na kuimarisha mfumo wa upozaji hewa katika Jengo la Nyaraka Pemba.

**Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka fedha 2014/2015 Ofisi kuu,

i. Imekagua jumla ya Taasisi 24 kuhusu masuala ya Usalama na Afya Kazini, kati ya hizo 19 kutoka Mkoa wa Kusini na tano Mkoa wa Kaskazini na Taasisi sita zimesajiliwa.

ii. Imefanya ukaguzi kazi kwa Taasisi binafsi 25, Taasisi 10 za Mkoa wa Kaskazini na 15 Mkoa wa Kusini. Elimu juu ya sheria za kazi imetolewa kwa Taasisi ya Laurent Nursery & Primary School kuhusu umuhimu wa mikataba na upimaji wa afya za wafanyakazi.

iii. Imeratibu mkutano mmoja wa vijana wenye lengo la kuwajengea uwezo kwa kuwabadilisha tabia ili waachane na fikra za kuchaguwa kazi na badala yake wapende kazi. Jumla ya vijana 40 walishiriki katika mkutano huo.

iv. Imekagua Taasisi 11 kuhusu masuala ya Ajira na kukusanya taarifa za wafanyakazi 585, kati ya hao 583 wenyeji na wawili wageni.

v. Imetoa mafunzo juu ya upokeaji, usambazaji, utumiaji na uhifadhi wa kumbukumbu kwa Maafisa wa masjala kutoka Taasisi tisa za Serikali. Mafunzo ambayo yalifanyika kwa nadharia na vitendo kwa lengo la kuleta mabadiliko katika Taasisi hizo na kuweka uwiano wa usimamizi wa kumbukumbu katika Taasisi za serikali.

vi. Imewalipia gharama za masomo watumishi watatu wanaoendelea na masomo kwa ngazi ya diploma na shahada ya kwanza katika vyuo mbalimbali.

vii. Imeendelea na zoezi la uingizaji wa taarifa za wafanyakazi katika mfumo wa elektroniki "Human Resource Database". Aidha, ufuatiliaji umefanyika katika Wizara mbalimbali ili kuona zoezi hilo linakamilika.

viii. Imefanya utekelezaji wa kuwapanga watumishi katika Miundo ya Utumishi "Scheme of Service" kwa Wizara 14. Hatua za ukamilishaji wa Wizara mbili zilizobakia zinaendelea. Ni mategemeo ya Wizara hii kwamba mwanzoni mwa mwaka mpya wa fedha 2015/2016 watumishi wote watakuwa wamepangwa katika madaraja yao kwa mujibu wa Miundo ya Utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, Hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, Ofisi kuu Pemba imetumia jumla ya Shilingi 323,816,350/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 252,900,850/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 70,915,500/= kwa matumizi mengineyo.

## KAMISHENI YA KAZI

### Malengo ya Kamisheni ya Kazi kwa Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Kamisheni ya Kazi ilipanga kufanya ukaguzi kwa taasisi 240 za kazi ili kuhakikisha zinatekeleza ipasavyo Sera na Sheria za kazi; kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba minane ya msingi ya kimataifa inayohusu masuala ya kazi pamoja na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani; kuimarisha Mfumo wa usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kazi; kuimarisha uhusiano na majadiliano ya pamoja ya sehemu za kazi, kuendeleza mashirikiano ya kazi Kikanda, Kitaifa na Kimataifa yanayohusu Sekta ya Kazi na kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Kupambana na Ajira za Watoto.

**Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Kamisheni ya Kazi,

i. Imekagua Taasisi 167 za kazi, waajiri na waajiriwa wameendelea kusisitizwa juu ya umuhimu wa kufuata sheria za kazi na kuimarisha uhusiano mwema kazini ili kuongeza tija.

ii. Imetayarisha taarifa za utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) na kuwasilishwa Shirika la Kazi Duniani (ILO - Geneva). Aidha, watendaji wawili wa Kamisheni ya Kazi wameshiriki katika kuandaa taarifa ya pamoja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani (ILO).

iii. Imepokea jumla ya migogoro ya kazi 74, kati ya hiyo migogoro 29 imesuluhishwa, migogoro 15 bado inaendelea na hatua ya usuluhishi, migogoro 24 ipo katika hatua ya Uamuzi na migogoro 6 imefutwa kutokana na kutokufika kwa walalamikaji siku ya uamuzi. Migogoro hiyo ilihusiana na kufukuzwa kazi, kukatishwa mkataba na tuhuma za kukosa uaminifu kazini. Aidha Kamisheni ya Kazi imefanya ukaguzi katika matawi ya vyama vya wafanyakazi 12 kwa Unguja na matano kwa Pemba na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Zanzibar – ZATUC.

iv. Imeimarisha mashirikiano ya kazi Kikanda, Kitaifa na Kimataifa yanayohusu sekta ya kazi, Uongozi wa Wizara ulishiriki katika mkutano wa Bodi ya Magavana 323 wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) uliofanyika Geneva mwezi Machi 2015. Mkutano huo ulijadili maandalizi ya mkutano mkuu wa ILO wa mwezi Juni, 2015.

v. Jumla ya watoto 5,065 (Unguja na Pemba) wametolewa katika ajira za watoto na kurejeshwa skuli na kupatiwa vifaa vya masomo. Aidha, familia 1,085 zimewezeshwa kiuchumi ili kujiongezea kipato na kuwanusuru watoto wasijiingize katika ajira.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, Kamisheni imetumia jumla ya Shilingi 157,518,257/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 139,418,229/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 18,100,028/= kwa matumizi mengineyo. Pia Kamisheni ilikusanya jumla ya Shilingi 186,849,900/=.

**KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA**

**Malengo ya Mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utumishi ilipanga kutoa ushauri kwa Mhe. Rais kuhusu masuala mbalimbali ya kiutumishi ikiwemo uteuzi wa watendaji wakuu na mishahara ya watumishi wa umma; kuwezesha na kusimamia Tume za Utumishi, Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Wakala wa Serikali kufikia utawala unaolenga matokeo bora; kufuatilia na kutathmini usimamizi wa Watendaji Wakuu wa Taasisi za umma kwa kufanya Uchunguzi na Ukaguzi wa kawaida na Ukaguzi wa kushtukizia kuhusu usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma; kupokea na kushughulikia Rufaa na Malalamiko dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma kadiri yatavyopokelewa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni pia ilipanga kushughulikia na kuidhinisha Mapendekezo ya Miundo ya Utumishi, Miundo ya Taasisi na Miundo ya Mishahara kadiri yatavyopokelewa; kuandaa na kufanya ziara 15 na mikutano 15 kwa ajili ya kujadili na kutoa maamuzi kuhusu masuala mbalimbali ya kiutumishi; kuandaa Muongozo kuhusu Ukaguzi wa Afya na Usalama Kazini katika Utumishi wa Umma na Muongozo kuhusu Mashauri ya Nidhamu na Rufaa katika Utumishi wa Umma; imepanga kuchapisha, kusambaza na kutoa Elimu na Ufafanuzi juu ya Miongozo mbalimbali na kuendelea kutoa elimu na ufafanuzi wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake kwa Watumishi wa Umma kupitia Mikutano ya Kazi, Warsha na Semina.

**Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Kamisheni ya Utumishi wa Umma,

i. Imesambaza nakala za Kanuni za Utumishi wa Umma 300 katika Taasisi za Umma Unguja na Pemba kwa lengo la kuongeza uelewa na uzingatiaji wa taratibu za usimamizi wa Utumishi wa Umma.

ii. Imefanya ukaguzi maalum kuhusu Masuala ya Mishahara na Maposho katika Mashirika ya Umma 11 na Wakala Tendaji 12 wa SMZ.

iii. Rufaa nne zimepokelewa na kufanyiwa uchambuzi na kutolewa uamuzi, rufaa moja imekubaliwa na tatu zimekataliwa kutokana na Kamisheni kutoridhika na madai yao (Angalia kiambatanisho Nam. 4a). Aidha, Kamisheni ilipokea Malalamiko manane ambayo yalifanyiwa uchambuzi na kutolewa uamuzi (Angalia kiambatanisho Nam. 4b).

iv. Imefanya mikutano 20 iliyojadili na kutoa uamuzi kuhusu masuala mbalimbali katika Utumishi wa Umma na kuidhinisha Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi ya Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, Miundo ya Utumishi ya Taasisi ya Viwango Zanzibar na Miundo ya Mishahara ya Shirika la Biashara la Zanzibar (ZSTC).

v. Imetoa mafunzo kuhusu Ufuatiliaji na Tathmini ya Usimamizi wa Rasilimali watu na Mafunzo maalum kuhusu Usimamizi wa Mashirika ya Umma yaliyoendeshwa kwa mashirikiano na Ofisi ya Msajilli wa Hazina Tanzania Bara kwa Makamishna na Watumishi wa Kamisheni.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, Kamisheni ya Utumishi wa Umma imetumia jumla ya Shilingi 466,628,951/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 201,916,115/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 264,712,836/= kwa matumizi mengineyo.

## TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

### Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Utumishi Serikalini ilipanga kuandaa na kusimamia shughuli za ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki, ambapo ajira 1,862 zilitegemewa kutangazwa na Tume ya Utumishi Serikalini; kusimamia haki na nidhamu za Wafanyakazi wa Serikali ikiwa ni pamoja na kutoa nyongeza za muda wa utumishi, kusikiliza rufaa za wafanyakazi wasioridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka za nidhamu zilizo chini ya usimamizi wa Tume; kuratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba, kuthibitisha kazi, kubadilisha kada, kufukuza kazi kwa watumishi watakaothibitika kwenda kinyume na taratibu za kazi, likizo bila ya malipo na kustaafisha kisheria watumishi wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, tume pia ilipanga kujenga uelewa juu ya Muongozo wa Upandishwaji Vyeo kwa Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi na Maafisa Utumishi wa Wizara na Taasisi za Serikali; kutoa elimu juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na Kanuni zake na kuimarisha huduma za kiutawala na uendeshaji.

### Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Tume ya Utumishi Serikalini,

i. Imepokea na kutangaza nafasi za ajira 418 kupitia ZBC Redio na TV. Usaili kwa nafasi 404 za ajira ulifanyika Unguja na Pemba na kibali cha ajira kwa nafasi hizo kilitolewa.

ii. Malalamiko 12 yaliwasilishwa na kufanyiwa kazi na Watumishi 13 wameongezewa muda wa utumishi. Tume imeidhinisha ajira za mikataba kwa watumishi 22. Ruhusa ya likizo bila ya malipo kwa watumishi 28 imetolewa, watumishi 43 wamestaafu kazi kwa hiari na watumishi 390 wamestaafishwa kazi kwa kufikia umri wa lazima.

iii. Watumishi 1,493 wamethibitishwa kazi, 29 wamebadilishwa kada, mmoja amethibitishwa wadhifa na wanne wameacha kazi kwa hiari. Makosa ya kinidhamu kwa watumishi watatu yamewasilishwa na kujadiliwa, kati ya hayo mawili yametolewa maamuzi. Mtumishi mmoja amerejeshwa kazini na mmoja amefukuzwa kazi na shauri moja linaendelea kushughulikiwa. (Angalia viambatanisho nam. 5a, 5b na 5c).

iv. Rasimu ya awali ya Muongozo wa upandishwaji vyeo imekamilika na kuwasilishwa katika kamati ya uongozi ya Wizara.

v. Imelipia gharama za mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Watumishi wanne. Aidha, Imetoa huduma za utawala na uendeshaji zikiwemo ununuzi wa kompyuta, vifaa vya kuandikia na matengenezo ya Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, Tume imetumia jumla ya Shilingi 403,683,900/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 99,834,900/= kwa malipo ya mishahara na Shilingi 303,849,000/= kwa matumizi mengineyo.

## CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

### Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Utawala wa Umma kilipanga kutoa fursa zaidi kwa watumishi wa umma kujiunga na chuo kwa mafunzo ya kukuza uwelewa na mafunzo ya kujenga uwezo katika fani mbalimbali kulingana na mahitaji ya taasisi husika; kuendelea kutoa mafunzo ya maadili kwa Watumishi wapya 907 watakaoajiriwa katika Taasisi za Serikali, wakala na mashirika ya Umma; kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa Taasisi zote katika fani za Matumizi Bora ya Kumbukumbu, Mikataba ya Ajira, umuhimu wa majukumu ya kazi "Job Description"na uandishi wa kumbukumbu za vikao.

Mhe. Mwenyekiti, chuo pia kilipanga kuendelea na zoezi la kupitia mitaala ambapo, mitaala mipya ya mafunzo ya "International Relations and Diplomacy", "Public Relations" na "Procurement and Supply" ilihusika; kufanya ziara katika taasisi mbalimbali kwa ajili ya kubadilishana uzoefu; kutafuta fursa za mafunzo

kwa ajili ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Chuo; kuandaa Sera ya Mafunzo na Muongozo wa Upimaji Kazi na Kupandishwa Vyeo kwa watumishi wa Chuo; kufanya manunuzi ya "transformer" moja ili kupunguza tatizo la umeme ambalo linajitokeza mara kwa mara katika jengo la Chuo – Tunguu; kununua "server" kwa ajili ya utunzaji kumbukumbu, majoho 100 kwa ajili ya wahitimu, mashamiana saba, kompyuta na vifaa vyengine vya uendeshaji na utawala na kuendeleza ujenzi wa jengo la chuo kwa hatua ya kupandisha ghorofa ya kwanza.

**Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Chuo cha Utawala wa Umma,

i. Kimepokea Watumishi wa Umma 512 waliojiunga katika mafunzo ya fani mbalimbali kwa ngazi ya msingi, cheti na stashahada. Aidha, Watumishi 110 kutoka Serikalini, Mashirika na NGOs wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya Protocol na Diplomasia na Watumishi wapya 331 kutoka Taasisi za Serikali wamepatiwa mafunzo ya maadili ya kazi.

ii. Kimeandaa mitaala miwili ya ngazi ya cheti na stashahada katika fani ya Ununuzi na Ugavi na imeanza kutumika. Watahiniwa 2,562 walifanya mitihani kwa muhula wa Julai-Disemba 2014.

iii. Kimefanya ziara Tanzania bara katika Chuo cha Diplomasia na ESAMI kwa kubadilishana uzoefu ambapo wakufunzi watano walishiriki. Mkufunzi mmoja amehudhuria mafunzo ya mahusiano ya kikanda China na watumishi sita wamepatiwa fursa ya kujiendeleza kitaaluma ndani na nje ya nchi.

iv. Kimeandaa Muongozo wa Sera ya mafunzo ya upimaji kazi na kupandishwa vyeo kwa watumishi wake.

v. Kinaendelea na ujenzi wa jengo katika hatua ya ghorofa ya kwanza na unatarajiwa kukamilika Septemba 2015. Aidha, huduma za utawala na uendeshaji zimetolewa zikiwemo ununuzi wa mashine za kupiga chapa 34, ununuzi wa samani na vitendea kazi vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, Chuo kimetumia jumla ya Shilingi1,606,320,863/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo TZS.377,372,933/= kwa malipo ya mishahara na TZS.1,228,947,930/= kwa matumizi mengineyo.

## MUELEKEO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Maelezo ya Programu Zilizomo Katika Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa ufafanuzi wa utekelezaji bajeti ya 2014/2015, napenda kutumia fursa hii kutoa maelezo ya muelekeo wa bajeti ya 2015/16 yenye ufumo unaotumia PBB.

Mhe. Mwenyekiti, Programu zilizomo katika Afisi hii zinalenga kuimarisha utoaji wa huduma bora na kwa ufanisi; kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano; uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka; kuhakikisha upatikanaji wa ajira za staha hasa kwa vijana; kusimamia viwango vya usalama na afya katika sehemu za kazi na kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi. Programu hizi zinatekeleza lengo la kwanza katika klasta ya kwanza na lengo la tatu katika klasta ya tatu ya MKUZA II.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma inasimamia Voti tatu. Voti namba EO1 ya Afisi Kuu ya Kazi na Utumishi wa Umma, Voti namba EO2 ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma na Voti namba E03 ya Tume ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya Programu ya Afisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma kwa Mujibu wa Umma kwa mujibu wa Vote vinavyohusisha matokeo ya muda mrefu madhumuni, huduma zinazotolewa viashiria na shabaha ya utekelezaji wa kila Programu kama ifuatavyo:-

## VOTI E01: AFISI YA RAIS KAZI NA UTUMISHI WA UMMA

Mhe. Mwenyekiti, katika Voti E01 Ofisi kuu inasimamia Programu tano zifuatazo:-
Programu 01: Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Mifumo na Miundo ya Taasisi

Programu 02: Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano Serikalini

Programu 03: Uratibu wa Uzalishaji na Upatikanaji wa Ajira za Staha

Programu 04: Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi

Programu 05: Mipango na Utawala
Mhe. Mwenyekiti, Programu hii imegawika katika Programu ndogo ndogo na uchambuzi wake na malengo yake kama inavyosomeka kwenye ukurasa wa 41 hadi 42.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Miundo na Mifumo ya Taasisi inatekelezwa na Idara ya Mipango ya Rasilimaliwatu na Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi. Jumla ya TZS. 589,333,000/= zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

Programu 02: Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii imegawika katika programu ndogo ndogo na uchambuzi wake na malengo yake kama kama inavyoonekana katika ukurasa wa 42 hadi 43.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali inatekelezwa na Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Jumla ya TZS.947,854,000/= zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

Programu 03: Uratibu wa Uzalishaji na Upatikanaji wa Ajira za Staha

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo na uchambuzi wa huduma zinazotolewa na ndani ya Program ni kama zinavyosomeka kwenye ukurusa wa 43 hadi 44.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Ukuzaji na Upatikanaji wa Ajira za Staha inatekelezwa na Idara ya Ajira. Jumla ya TZS. 117,232,000=/ zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

Programu 04: Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii imegawika katika programu ndogo ndogo na uchambuzi wake na malengo yake kama kama inavyoonekana katika ukurasa wa 44 hadi 45.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi inatekelezwa na Kamisheni ya Kazi na Idara ya Usalama na Afya Kazini. Jumla ya TZS. 407,832,000/= zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

Programu 05: Mipango na Utawala

Programu hii imegawika katika katika programu ndogo ndogo na uchambuzi wake na malengo yake ya huduma kama inavyosomeka katika ukurasa wa 45hadi 46.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Mipango na Utawala, inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Afisi kuu Pemba na Chuo cha Utawala wa Umma. Jumla ya TZS. 2,390,149,000/= zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

**VOTI E02: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA**

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utumishi wa Umma inasimamia Programu mbili zifutazo:-

Programu 01: Usimamizi wa Mifumo ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma

Programu 02: Utawala na Uendeshaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma

Programu 01: Usimamizi wa Mifumo ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma
Utekelezaji wa malengo na uchambuzi wa huduma zinazotolewa na Programu ni kama zinavyosomeka katika ukurasa wa 47.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Usimamizi wa Mifumo ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma inatekelezwa na Idara ya Miongozo, Uchambuzi na Utafiti na Idara ya Ukaguzi, Ufuatiliaji na Tathmini. Jumla ya TZS. 341,506,000/= zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

Programu 02: Utawala na Uendeshaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma
Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo ya uchambuzi wa huduma zinazotolewa na Programu hii ni kama zinavyosomeka katika ukurasa wa 47 hadi 48.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Utawala na Uendeshaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma inasimamiwa na Idara ya Utawala, Utumishi na fedha. Jumla ya TZS. 381,894,000/= zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

**VOTI E03: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Utumishi Serikalini inasimamia Programu mbili.

Programu 01: Usimamizi wa watumishi Serikalini

Programu 02: Utawala na Uendeshaji

Programu 01: Usimamizi wa watumishi Serikalini
Kuhusu Programu hii ya mwanzo usimamizi wa Watumishi Serikalini Mhe. Mwenyekiti, programu hii inasimamia Programu ndogo mbili zifuatazo:-

- Usimamizi wa Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini
- Usimamizi wa uajiri wa Watumishi wapya

Programu ndogo 01: Usimamizi wa Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii imegawika katika program ndogo ndogo na malengo yake pamoja na huduma kama zinavyosomeka katika ukurasa wa 48 hadi 49.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Usimamizi wa watumishi Serikalini inatekelezwa na kitengo cha Ajira na kitengo cha Nidhamu na Haki za Watumishi. Jumla ya TZS. 273,266,200/= zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

Programu 02: Utawala na Uendeshaji
Mhe. Mwenyekiti, Utekelezaji wa malengo na uchambuzi wa huduma zitakazotolewa na Programu hii ni kama zinavyosomeka katika ukurasa wa 49.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Utawala na Uendeshaji inatekelezwa na kitengo cha Utawala na Uendeshaji. Jumla ya TZS. 192,833,800/= zimepangwa kwa ajili ya utekelezaaji wa programu hii.

**SHUKURANI**

Afisi yangu inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Washirika mbalimbali wa Maendeleo kutokana na michango yao ambayo kwa kiasi kikubwa imefanikisha utekelezaji wa majukumu ya Afisi. Aidha, Afisi yangu itaendelea kutoa mashirikiano na Washirika wetu wa Maendeleo ili kufanikisha dhamira na malengo yake.

Kwa niaba ya Serikali na Afisi yangu napenda kuwashukuru kwa dhati Washirika hao wa Maendeleo ambao ni pamoja na nchi wahisani, zikiwemo China, Korea ya Kusini, Japan, Singapore, Uholanzi, India, Oman, Marekani, Sharja, Ras Al Khaimah na Mashirika ya Kimataifa yakiwemo Shirika la Kazi Duniani, KOICA, JICA , Sweden na Save the Children.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu pia inapenda kutoa shukrani kwa Taasisi mbalimbali kwa mashirikiano waliyotupa na naziomba kuendelea kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuwaletea wananchi wenzetu wa Zanzibar maendeleo.

Taasisi hizo ni pamoja na Jumuiya ya Waajiri Zanzibar ZANEMA, Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi ZATUC, Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii ZATI, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ZSSF na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, Natumia fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi hususan Wakurugenzi wa Uendeshaji na Utumishi na Viongozi mbalimbali na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano mazuri tulionayo katika kutekeleza majukumu yetu.

**HITIMISHO**

Mhe. Mwenyekiti, Kama nilivyotangulia kusema katika maelezo yangu ya awali, Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma ikishirikiana na Idara na Taasisi zote zilizopo chini yake kwa jumla kwa mwaka wa fedha 2015/2016 itasimamia kuharakisha upatikanaji wa ajira bora, kusimamia haki na wajibu wa watumishi wote, kuongeza fursa za ajira nchini na kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kupitia Baraza lako tukufu vilevile napenda kutoa wito kwa Watumishi wote wa Umma kuendelea kufanyakazi kwa bidii, ari, maarifa, ubunifu na kuacha vitendo vya rushwa, ili kutimiza malengo yalioainishwa katika Ilani ya Chama Tawala ya kuleta maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya TZS. 7,520,400,000/= katika utekelezaji wa Programu zake zote na kukusanya jumla ya TZS. 325,387,000 kwa kuchangia mfuko mkuu wa Serikali. Uchambuzi zaidi wa muelekeo wa matumizi na makusanyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 unapatikana katika viambatanisho namba 4, namba 5 na namba 6.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante hoja imepokelewa. Sasa tutamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis (Kny**: **Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Mhe. Mwenyekiti, naomba kusoma hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala wa Baraza la Wawakilishi kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka 2015/16.

Mhe. Mweyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga Taifa letu.

Pia, nachukua nafasi hii adhimu kwa moyo wa dhati kabisa, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti**,** nachukua nafasi hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ushirikiano wao mkubwa walionionesha katika kipindi chote tulichokuwa tunafanya kazi za Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati hii ina wajumbe wenye uwezo unaolingana, upeo na uzoefu katika ngazi mbali mbali za uongozi, hivyo imeweza kutoa miongozo yake katika taasisi na idara mbali mbali inazozisimamia kwa lengo la kuziendeleza taasisi hizo ziweze kufikia malengo yake kama yalivyopangwa. Naomba nichukue nafasi hii niwatambue Wajumbe hao wa Kamati kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ussi Jecha Simai | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Aziza Wazir Kheir | Katibu |
| 8. | Ndg. Khamis Hamad Haji | Katibu |

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma ndiyo kiungo cha utendaji kazi wa Serikali nzima ambao unategemea zaidi nguvu kazi ya wataalamu katika kada mbali mbali za utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, Watumishi wa Umma ndiyo daraja la kuvukisha huduma za Serikali kuwafikia wananchi wetu, huduma ambazo zinatokana na mipango, mikakati na vipaumbele tunavyovipanga na kuamua katika chombo hiki. Kazi kubwa ya watumishi wa umma ni kuhakikisha kuwa wanatumia utaalamu na ujuzi wao kuisaidia Serikali kufikisha huduma hizo kwa wananchi kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma katika bajeti ya mwaka 2015/2016 ambayo imeanza kutumia utaratibu mpya wa kibajeti ambao umeelemea katika utekelezaji wa program kwa lugha ya kiingereza

ni *Programme Based Budget PBB.* Mfumo huu umeiwezesha Wizara hii kusimamia program tano ambazo ni Usimamizi wa Rasilimali watu, mifumo na miundo ya Taasisi. Uimarishaji wa Kumbukumbu na mawasiliano ya Serikali. Uratibu wa uzalishaji na upatikanaji wa ajira za staha. Usimamizi wa utekelezaji wa sheria za kazi na program ya Mipango na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, program zote hizo zina lengo la kuhakikisha kuwa maslahi na mienendo ya wafanyakazi wa umma yanazingatiwa na kufuatiliwa kwa umakini mkunwa ili maendeleo ya pande zote yaweze kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, mfumo huu wa kibajeti endapo utasimamiwa vizuri na taasisi husika, utawezesha baadhi ya changamoto zilizopo katika taasisi hizo kutatuka kwa haraka, endapo upatikanaji wa fedha zilizotengwa zitaingizwa kwa wakati.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii katika bajeti ya mwaka 2015/2016 imepangiwa programu moja kuu ambayo ni Mipango na utawala. Katika prograsmuhiyo zipo program ndogo ndago tatu ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na program ya Kuratibu shughuli za Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezwaji wa program hizo utasaidia kwa kiasi kikubwa kuratibu shughuli za watumishi na Umma na kuondoa baadhi ya changamoto zinazowakabili. Aidha, mipango ya kuwaendeleza watumishi wa Umma itafanikiwa kwa kiasi kikubwa endapo Idara hii itashirikiana na taasisi husika za Wizara mbali mbali za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa sera ya *E-Government* umefanikiwa kwa kiasi kikubwa ambapo Kamati ilielezwa kuwa taasisi za Serikali 53 kwa upande wa Unguja zimeshaunganishwa na mradi wa *E-Government* na kwa upande wa Pemba matayarisho ya kuziunganishia taasisi za Serikali yanaendelea ambapo kampuni ya *ZTE* kwa kushirikiana na kampuni ya *ZANTEL* wanafanya juhudi za kukamilisha mopango hiyo ili zoezi hilo liweze kukamilika.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la huduma za Serikal mtandao ni kumsaidia mwananchi kupunguza gharama za upataji wa huduma na kuleta unafuu wa maisha ya mwananchi huyo. Hivyo, Kamati yangu inatarajia kuwa kuunganishwa huduma hiyo kwa baadhi ya Taasisi za Serikali, kunamaanisha kuwa wananchi watanufaika kwa kiasi kikubwa na kurahisishiwa huduma za msingi wanazozihitaji.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inapendekeza kupitishwa kwa program hizi na fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa program hizi zipatikane kwa wakati.

**IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA KITAIFA**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa idara hii imepangiwa programu ndogo ya uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu za Taifa ikiwa na lengo la kuhifadhi na kusimamia nyaraka na kumbukumbu za Taifa kwa Serikali na matumizi ya Umma. Aidha Kamati ilielezwa kuwa programu hiyo inatelekezwa na Idara mbili ambazoi ni Idara ya Nyaraka na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Hivyo Kamati iliridhika na maelezo iliyopatiwa wakati wa kupitia bajeti na kuridhika jinsi ya fedha zilizowekwa kwa ajili ya kuendesha programu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kikao hicho Kamati ilisikitishwa sana na taarifa iliyopatiwa ya ukosekanaji wa fedha zilizoidhinishwa katika bajeti iliyopita kwa lengo la kufanya ukarabati wa nyumba ya Idara ya Nyaraka iliyoko Pemba. Kamati imeshangazwa sana na taarifa hizo na inapenda kupatiwa taarifa sahihi juu ya fedha hizo zilizoidhinishwa ambazo hadi sasa hazijaingizwa kwa ajili ya kufanyia ukarabati wa jengo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili la kuidhinishwa fedha na Baraza lako Tukufu kwa baadhi ya taasisi za Serikali na baadae fedha hizo kutojulikana zinakokwenda limekuwa ni sugu, kutokana na malalamiko ambayo Kamati imekuwa ikiyapata, hivyo, Kamati inamuomba Waziri husika atupe taarifa sahihi fedha hizi zinazoidhinishwa na baadae kutopatikana hupotelea wapi?

**KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA**

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utumishi wa Umma katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 imepangiwa kusimamia programu mbili ambazo ni programu ya usimamizi wa mifumo ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma na programu ya utawala na uendeshaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu hizo ni kuhakikisha kuwa uimarishwaji wa mifumo ya uendeshaji na usimamizi wa rasilimali watu inafuatwa kwa mujibu wa sheria zilizopo. Aidha, watumishi wa Umma watapata nafasi ya kujengewa mazingira mazuri ya kazi ambayo yatawawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi. Kutokana na umuhimu wa programu hizo, Kamati yangu inachukua nafasi hii

kuwaomba Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi waipitishe bajeti ya Wizara bila pingamizi yoyote.

**CHUO CHA UTAWALA WA UMMA**

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Utawala wa Umma kwa mwaka wa fedha 205/2016 kinasimamia programu moja ya mafunzo na maendeleo ya rasilimali watu. Lengo kuu la programu hiyo ni kuhakikisha kuwa watumishi wa umma pamoja na wananchi wote kwa ujumla wananufaika na elimu inayotolewa chuoni hapo kwa kuwapatia elimu yenye kiwango cha hali ya juu. Aidha, programu hii imetengewa jumla ya shilingi 2,405,200,000/= kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, jamii yoyote ile inayapata maendeleo yake kwa kasi huwekeza katika elimu kwa kuwasomesha watendaji wake ili waweze kutumia utaalamu wao katika maendeleo ya nchi yao. Hivyo, Kamati ina imani kubwa kuwa utekelezwaji wa programu hii utasaidia kupatikana kwa wataalamu watakaolisaidia Taifa kuwa na misingi imara ya utawala wa umma ambao utapelekea kuwa na viongozi waadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na imani hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwashawishi Wajumbe wenzangu wakubaliane na bajeti hii iliyopangwa ili fedha hizo ziweze kutumika katika utoaji wa elimu ambayo itawasaidia wananchi wetu.

**OFISI KUU PEMBA**

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba ni kiungo muhimu cha Wizara katika kuratibu shughuli mbali mbali za Idara za Serikali. Aidha, katika maeneo taasisi ambazo zinakumbwa na changamoto nyingi na kukosa utatuzi wa haraka, Afisi Kuu Pemba ni moja ya taasisi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto zinazoikumba Afisi Kuu Pemba ni suala zima la ukosefu wa bajeti za kuendeshea shughuli za kiofisi. Katika kikao na Kamati, Wizara ilieleza kuwa Ofisi Kuu Pemba imepangiwa bajeti finyu ambayo haitoshelezi kutekeleza malengo yaliyopangwa katika ofisi hii. Aidha jengo linalotumika kwa ajili ya shughuli za kiofisi ni dogo sana na haliwatoshi watendaji waliopo jambo ambalo linapelekea baadhi ya huduma kwa baadhi ya wakati kukosekana kutokana na ukosefu wa ofisi.

Mhe. Mwenyekiti,  baadhi ya huduma zinazokosekana katika Wizara hii kisiwani Pemba ni za kutoka katika Tume ya Utumishi Umma na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Taasisi hizi hutoa huduma zake kwa tabu sana kutokana na kukosa ofisi za kudumu zitakazowawezesha kutoa huduma hizo ipasavyo kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti,  Kamati yangu inachukua nafasi hii kuliomba Baraza lako tukufu kufanya juhudi ya kuviangalia vifungu vya fedha zilizopangwa katika programu mbali mbali, na endapo ikipatikana programu ambayo fedha zake na matumizi yake hayaendani, basi fedha hizo zilizoletwa katika Ofisi Kuu Pemba kwa Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma.

**HITIMISHO**

Mhe. Mwenyekiti,  Mwisho naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala katika Baraza lako Tukufu. Pia niwashukuru Wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha Hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, ninawaomba Wajumbe wote waliopo katika Baraza hili wachangie bajeti hii, watoe mapendekezo yao panapohitajika na hatimaye kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoziibua wakati wa mjadala.

Mhe. Mwenyekiti,  naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante muwakilishaji ambaye umewakilisha vizuri ripoti yako. Sasa ni nafasi ya Wajumbe, kama kawaida yetu tunaanza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, lakini huku sina jina jengine zaidi ya hilo. Wale ambao wanahitaji kuchangia naomba walete majina na nitakapokuwa sina nitamkaribisha Mhe. Maalim Haroun Ali Suleiman ili a-*wind up.(Makofi).*

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana ninashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kunipigia makofi, inaonesha wamenikubali nianze mimi, ninashukuru sana na hii ni ishara tosha kwa leo Mhe. Waziri amekuja na *style* yake mpya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri na timu yake yote wazee kutoka Kae, wapo hapa nishukuru sana hili jambo ambalo ni moja katika dawa na

moja kulitilia ufanisi mkubwa sana ili kuonesha umahiri wake kwa wananchi wake, hiyo ndiyo utawala bora unavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kitendo hicho, jamani wazee wangu karibu sana na nyinyi ndiyo muliojenga historia leo katika Baraza la mwisho hili kuja hapa kwenye Baraza la Wawakilishi, ninawashukuru sana wazee wangu, karibuni sana.

La pili Mhe. Mwenyekiti, leo na wewe ulikuja na *style* yako mpya, ukasema hata Wizara yake ime-*perform* vizuri sana. Nalo hilo ninashukuru sana wamejaa katika viti, *row* nimeona ile na hiyo ndiyo uzuri mheshimiwa, lakini la kusikitisha nikija katika *row* ya Mawaziri watu hamna, ni jambo ambalo nalo linasikitisha. Waziri mmoja waliobakia Manaibu na Mawaziri wasiokuwa na Ofisi Maalum na nyinyi ninakupeni hongera nisikuvunjeni moyo. Lakini hata hivyo viti kidogo vimepungua, ukija kwa Wajumbe ninashukuru kama kawaida yetu imo *just* ku-*run*, unajua saa nyengine Wajumbe wanakaa muda mwingi, sasa nao niwape vile vile kuwa wametumia haki yao ya kutembea kuniachia nijibu vizuri. Wajumbe ninakushukuruni sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa baada ya baraka hizo niingie katika ufanisi. Mhe. Mwenyekiti, mimi niingie katika hapa sehemu ya kifungu hichi kwenye ukurasa wa 12; sehemu ya Idara ya Mipango na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa ni hivyo ninashukuru sana kwa sababu lazima hii iwe ina *plan* hasa kwa wafanyakazi, ni Idara kubwa sana *include* na mambo ya utumishi, mambo ya utafiti, mambo ya nini. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, amesema kuwa hapa alikuwa na mikakati mizuri ya upangaji wa fedha na mambo mengine sana.

Lakini ningemuomba Mheshimiwa atakapokuja kujieleza atuoneshe sasa katika hiyo mikakati ambayo hasa hii historia ya nyuma, na sasa hivi kwa kuwa tuna hii *PBB*, inaonesha zaidi atakuwa na mikakati zaidi mizuri. Ningemuomba hapa Mheshimiwa mikakati yake imefikia katika lengo la asilimia ngapi ili tuone jinsi gani alivyokakamaa katika utekelezaji hasa katika kitengo hicho. Kwa sababu hapa ndipo panapo Wizara yenyewe, hapa ndipo kunako mipango kamili ambayo ya utendaji na kuweza kufanikisha na nini. Hilo Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba kwanza hapo aje kunielekeza vizuri kutokana na jitihada alizozifanya kutokana na hali halisi na kuweza kuimarisha katika sera hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nione hapa katika Ofisi ya Waziri, nimeona *alhamdulillah* hapa katika utetezi alivyojiandaa vizuri, na utaratibu wa shughuli mbali mbali za kimaendeleo na kijamii, nayo hii nimpongeze sana amefika pahali pazuri sana na kuonesha jinsi gani watu ambao waliokuwa kwenye mahafali, kwenye mambo ya Umoja wa Kimataifa, warsha za mafunzo. Kwa kweli Mheshimiwa hapa inastahili sifa, pengine kuna nchi nyengine labda umezisahau, ningeomba na hapa kidogo Mheshimiwa kama zipo umezisahau katika kuja kutujibu naomba kuna nchi; zipo nyingi nyengine umezisahau basi ili ukamilishe *CV* yako vizuri zikumbuke tena Mheshimiwa utuletee hapa ili tuweze kukusaidia zaidi na kuweza kukupongeza zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niingie katika masuala ya utumishi. Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa huu wa 20 amenieleza vizuri sana Mheshimiwa wangu jinsi ambavyo Idara ilipanga na kuthamini tathmini za ufuatiliaji, utekelezaji wa miundo ya utumishi kwa Wizara na taasisi zote za umma.

Mhe. Mwenyekiti, hilo mimi ninakubaliana nalo lakini bado ningeomba sana ili kwa kuweka ufanisi zaidi hasa kwenye Idara hii, kwa sababu unajua kunako utumishi ndipo kwenye utendaji. Kwa sababu hapa wanatakiwa watu waweze kufanya kazi kwa vizuri, ili kuweza kufanikisha lile lengo la azma ya nchi katika kuleta maendeleo na kupata wafanyakazi bora.

Lakini kidogo Mhe. Mwenyekiti, niweze kuzungumzia suala la kuongeza muda. Mhe. Mwenyekiti, hili suala la kuongeza muda tuangalie kwa *style* ya aina yake. Unajua sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wanaongezewa muda, kwa kweli hawastahiki kwa sababu vijana tunao wengi sana. Vijana sasa hivi wamesoma wapo nje kwa wingi sana.

Sasa mimi ninafikiria tuwe na *style* ya kusema kuwa hawa tutakaowaongeza wawe wenye taaluma. Maana yake wawe na fani ya utaalamu ambayo kuikosa kwa ghafla na muda umeshafika itakuwa ni vigumu. Mimi naona Mheshimiwa hawa tuwape nafasi hizo ili kwa kuweza kufanikisha ile hali halisi tunayokwenda nayo, tusiwaongezee tu, Wakurugenzi nao tusiwaongezee tu kwa sababu hapana taaluma yoyote pale Mheshimiwa.

Kwa hivyo lazima tuweze kuwa na watendaji ambao wana taaluma nzuri sana. Mheshimiwa tufanye vitu kama hivyo, ningeomba na tuangalie kama sheria ipo hiyo basi iweze kurekebishwa vizuri ili kufika lengo ambalo tunalitaka.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 22 kwenye suala la nyaraka. Hapa iliundwa Tume na Mhe. Mwenyekiti mwenyewe aliyetoa hoja pale. Lakini niseme Mhe. Mwenyekiti, hatujapata ripoti ya Serikali inasemaje. Ningemuomba Mhe. Waziri kwa upole kabisa na unyonge ili atakapokuja hapa atuletee ripoti ile. Lakini nilisikia kulifanyika ziara ya kwenda watu Oman, sijui wamefikia wapi. Mimi ninafikiria Mhe. Mwenyekiti, *just briefing* tu, kidogo tu utwambie hili suala tumefikia wapi kwa upole kabisa ili wananchi na viongozi wa umma waweze kuridhika.

Mimi ninaamini Mhe.Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Waziri yeye ni mwalimu, unajua jinsi gani ya kuweza kui-*present* hiyo hoja ambayo iliyopita hapo nyuma, ijapokuwa ilizua hoja kali sana lakini isikushitue kwa sababu ni moja katika kuonekana umahiri wa kazi zako zinavyokwenda. Ndiyo maana Rais akaweza kukuchagua na kuonesha ufanisi, kwa sababu ingekuwa umahiri wako haoneshi, basi Mhe. Rais asingekuchagua. Lakini alikuchagua kutokana na *experience* yako, umahiri wako kwa utendaji. Hilo mimi nikupongeze sana na nikushukuru. Kwa hivyo na hii ripoti Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukaileta kwa *style* ya aina yake humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, niingie ukurasa wa 31 kwenye Kamisheni ya Kazi. Mhe. Mwenyekiti, hapa ndiyo nyimbo yangu inapata kufikia hapa, watu wa *hansard* waweke vizuri na ninaomba wanisikilize ninavyozungumzia. Hapa ndiyo hasa ninapotaka kufikia katika ule uteuzi wangu wote ufikilie hapa.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni Kamisheni ya Kazi, lakini binadamu mapungufu anayo, binadamu ukamilifu anao. Hii yote tuseme binadamu Mwenyezi Mungu kampa, na yote, na yote si mabaya kwa Mwenyezi Mungu haya, lakini kwa binadamu utaona mojawapo baya au zuri ataliona baya, hiyo ndiyo tulivyo binadamu, tunavyodhania katika nchi na tunavyoishi. Lakini mimi hapa naomba leo niseme Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kama Kanuni inawezekana iwekwe kando nizungumze kwa Kiingereza. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, nimegundua sana Mswahili unapomueleza Kiingereza anafahamu upesi kuliko mtu ukimueleza Kiswahili, na hasa kama Mswahili mwenyewe anavyochowea Kiswahili.

Sasa mimi ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kuwa nimenong'onezwa hapa Kanuni na Mheshimiwa Naibu hapa Dimwa anasema Kanuni hainiruhusu kwa kuzungumza Kiingereza, basi naomba niseme kwa Kiswahili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hasa watendaji wakuu hebu tueleweni nini tunachokizungumza, nini ushauri wetu, kwa sababu Mwakilishi hii ndiyo kazi yake, Mwakilishi anawakilisha wananchi. Wengine wanakasirika wanasema aah! Mheshimiwa anatuingilia kazini. Mimi ninashangaa leo hapa ninakuingilieni lakini ndiyo utaratibu, tena ndani ya Katiba siyo, wacha Kanuni, ndani ya Katiba. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nimeekewa *special* kuwa sisi ndiyo kazi yetu kukutengenezeeni, kukutafutieni na kuipanga bajeti kukuleteeni nyinyi ili iwe na mwelekeo kwa mujibu wa utaratibu. Sasa mimi mtu akiniambia aah! mheshimiwa anapenda kutuingilia kazi yetu, mimi aisee! ninashindwa kumfahamu. Mimi ninamtengenezea yeye kwa sababu mimi nimeshaona, wananchi wanalalamika. Sasa wanapolalamika, mimi nifanye nini, nitie mikono mifukoni. Hawatonikubali wananchi hata siku moja, na hawatonisikiliza nini ninachowaambia.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tuna ile sehemu moja mule inaitwa *DHU*. Hichi kitengo Mheshimiwa kwa kweli ni kizuri sana. Mhe. Waziri hichi kitengo ni kizuri sana na hichi tunakipa mzigo mkubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, tukubali hichi tunakipa mzigo mkubwa sana. Sasa ndiyo maana nikasema mimi ninataka kuzungumza Kiswahili kwa sababu munielewe kuwa mimi sitaki ushauri wa kulipwa au vipi, tukikubaliana na mukinisikiliza Mheshimiwa, basi hatuji kusema maneno mengine hapa. Lakini mtu anauwacha ushauri ule wa mwakilishi, kwa kuwa nani fulani, Mhe. Makame Mshimba kasema jambo lile. Akija mzungu akisema kwa Kiingereza anaona hii *well and good.* Tena anasema *yes well and good*, ametoa kitu kizuri sana pale. Lakini Makame Mshimba akisema pale porojo.

Sio porojo. Mimi mwenyewe naji-*evaluate*. Mhe. Mwenyekiti, mimi naji-*evaluate*. *Brain* yangu mimi kwanza inaniambia siwezi nikaropokwa kitu kama sijaki-*dilute*. Naingia nayo kwenye *labour* yangu nali-*dilute* lile neno, hili litaisaidia serikali, hili litasaidia wizara, hili litasaidia wananchi. Hiyo ndio *brain* yangu inavyoniambia. Sasa nikisema hapa kitu kitakuwa na *options* mbili. *Option* ya kwanza itasaidia wizara kuweka mikakati mizuri, la pili wananchi litawaokoa katika lile ninalolizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema juzi *DHU* kwa kweli ina wataalamu nakubaliana nalo. Ushauri wangu tena *very simple* kabisa, wala sitaki USA *dollar*, T.*shillings*. Hata T.*shillings* yenyewe siitaki.

Mhe. Mwenyekiti tunaweza tukawapunguzia mizigo hawa *DHU* kabisa, pindipo idara husika wakawa na plan ya kwenda katika kuwaondoa migogoro halafu baadae ikaweza kupungua. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe radhi Kamishna wangu, hata kama yeye anajizimua kufanyakazi, lakini bado Maafisa wake wako *very poor,* kusema kweli bwana haistahiki. Nina sema kwa ushahidi tosha.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri lazima sasa atoke kabisa aende akafanye kazi katika maeneo humo ni lazima akacheze nayo, kwa sababu atakapokuwa na *strong time*, ni mtu kuweka *time* yake vizuri tu akawa na *special programme,* maana yake lazima tuwe na *programme* katika utekelezaji, kwa sababu kuna sehemu nyengine wanatumwa watu hawana mikataba. Yeye hajui pengine maskini ya Mungu, kumbe hajatengenezewa kwa program maalum au hawajaweka datas za kufanyisha, kama makampuni au sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wanafanya, wanaita shop nini pale Kwerekwe, limenitoka kidogo hilo. Watu wana miaka mitano au sita vijana hawana mikataba kabisa. Sasa tunafanya vipi, hawajui pakwenda maskini ya Mungu, kazi wanazitaka na mikataba hawana, kila siku wanadanganywa, basi itakuwa kila siku tunalilia mikataba tu.

Mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti. Hawa wakitoka hapa ndio wanakwenda kule kwenye hiyo DHU, wanakwenda pale tunawapa mzigo. Sasa ubaya wake, wataalamu wenyewe hata mishahara yao midogo na ule utumishi wenyewe wanao humu humu. Anafanyakazi ya kumsikiliza tajiri ana mamilioni. Niwashukuru sana Mwenyezi Mungu awajaalie wasighilibike, kwa sababu kumsaidia mnyonge ni pepo moja kubwa sana.

Kwa hivyo, niwaombe sana watu wa *DHU* na niwape pole sana. Wana mtihani mkubwa sana hawa. Lakini huo mtihani mkubwa tunawaingizia sisi na tunawaingizia kwa sababu kama nilivyosema kuwa Makamisaa hawa, kama wangekuwa wanafanyakazi zao vizuri kwenye mahoteli, basi hawa lazima waweze kupumzika, kwa sababu wao wangeweza ku- *defend* nao kuzizuwia zile kesi wakaweza kusuluhishwa wakafuatilia mikataba. Leo mikataba inakwenda kuzungumzwa kwenye *DHU*. Mhe. Mwenyekiti, suala hili linatia aibu sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hii suala mimi nitowe ushauri wangu, kwa sababu namba inazidi kukua wana kazi nyingi sana kesi hawajazimaliza. Kuna kesi zile za kiwandani mheshimiwa, sasa wafanye nini. Nasema kuwa sijui serikali tunakuwa tukoje. Lakini mimi naomba niseme watu nataka wanifahamu, kwa sababu lengo kubwa ni kuondoa umaskini wa wananchi, sio kuwakandamiza wananchi au sio kuwafanya watumwa wananchi katika ardhi zao.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kiwanda nimesema sana. Kiwanda cha Miwa kuna wafanyakazi kwa muda mwingi sana. Siku hiyo Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko walisema watafanya ziara na Mhe. Waziri muhusika. Sasa leo ningeomba kama ile ziara imefanyika basi utakapokuja kusema Mhe. Waziri basi naomba sana njoo uje unipe taarifa ambazo mmefikia. Sijui watu wa *labour* kama wamekwenda Makamisaa kama wamekwenda huko.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nataka tufikirie sana Mhe. Waziri, kwa sababu migogoro inakuwa mikubwa sana, pamoja na suluhisho linalofanywam, hawa ndugu zangu wa *DHU*, kwa kweli bado haijatufikia katika muafaka mzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana, kwa sababu mpaka sasa hivi bado vijana wetu wanasumbuliwa sana na makampuni. Makampuni wanaona sasa hivi hapa Zanzibar bado wale wakubwa. Wanavyosema wenyewe, toba sikio siwezi kusema mimi. Wanafika pahala wanasema kwamba alaa! Kamishna wangu mwenyewe nimemuweka hapa. Wewe unamjuwaje Kamishna, lakini ndio mbinu wanavyotumia. Pengine wala hamjui Kamishna, wengine wala hawamjui Kamishna ni nani.

Sidhani kama Kamishna wangu anaweza akachukua pesa za kwenda kuwadhalilisha wananchi wake. Pengine na yeye iko siku atataka kugombea jimbo na yeye, sasa *query* itakuwa hapa, lakini sidhani kama anaweza akafanya utumbo kama huu, hata siku moja mimi siamini. Lakini kwa kuwa wale watu wanafanya *technique* mbinu za kuwavunja moyo hawa wahusika.

Mhe. Mwenyekiti, tayari zilikuwepo kwenye mahoteli. Mimi nilisema jamani Wazanzibari Watanzania tunakosa nafasi wanakuwepo watu, sheria hapa nilisema jamani hebu tuigeuze, sheria tuione. Huyu mwenye nyumba ndio apewe nafasi ya mbele, zile zao wao hatukatai mbili au tatu wapewe, lakini tena mpaka kwenye kukosha masufuria anawekwa mtu wa nje, hawa watafanyakazi gani.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana tujaribu kutafuta sheria, tatizo letu ni sheria zimepitwa na wakati. Sasa kama sheria zimepitwa na wakati Mhe. Waziri weka kabla hujaondoka hapa kumaliza na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakujaalia, wazee wangu wale watakuleta tu hapa. Watu wa Makunduchi bwana ni wasikivu sana watakurudisha tu, mimi wala sina wasi wasi nao.

Nina imani kubwa, kwa sababu mheshimiwa umefanya jitihada kubwa kwenye jimbo haki ya Mungu, maana yake niseme ukweli kwa sababu na mimi nina sehemu moja ya Makunduchi nikuambie. Makunduchi saa zote mimi huwa nakwenda kule natembea, nazungumza wananijua hakuna asiyenijua kule.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naye marehemu baba yangu wakimwita tumbo tumbo, wananijua pale Kijini nilikuwa nikikaa sana. Sasa lakini Mhe. Waziri pamoja na hayo hebu hili suala tuliweke sawa, kwa kweli wananchi wetu sheria sasa hivi tuitizame. Mahotelini huko Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu wananyanyaswa. Nilisema pale *Zanzibar Resident*, kule sehemu ya kuendea upande wa Kusini huko, nilisema kule kuwa wananchi wetu wanadhalilishwa. Sasa sijui kama Kamishna aliliona hilo na kulifuatilia.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine na yeye nimpe hongera sana Kamishna ambapo baadhi ya mambo mawili au matatu niliyojaribu kufanya nao kazi, wamepata kusaidiwa vijana wale wa *Sunflower* pale, wamelipwa kidogo lakini mambo mengine hawajalipwa. Wale wasimamizi wanatupiga maboya wanatuambia nitakuja saa 8 kumbe haji wakati ule, anakuvizia ukishaondoka wewe ndio anaingia, ndio utaratibu ulivyo.

Sasa mimi ningeomba na wao waweze kujisawazisha yale ambayo tuliyozungumza, kwa sababu na wao leo wanazaa na watoto wao watakuwemo mule na wakati huo sasa wewe umeshachoka, anadhalilishwa mwanao kwenye hoteli, anadhalilishwa mwanao kwenye makampuni sijui utalia na nani. Kwa sababu wewe tayari umeshachoka huwezi kufanyakazi tena.

Sasa mimi ndipo ninaposhangaa Mhe. Mwenyekiti, jamani tusiwe wabishi, tusipende kupokea mikono mirefu, kuna leo na kesho, ukichoka wewe mwanao anataka kuingia kwenye mahoteli. Mhe. Mwenyekiti nataka niseme suala hili sina mantiki mbaya lakini lugha watanifahamu nini ninachokizungumza. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuwe *serious* katika masuala haya, ili kuweka mustakabali mzuri wa hichi chombo kama nilivyosema.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki niingilie kwa sababu kile chombo cha *DHU* kama nilivyosema ni *full* mahakama, kwa sababu wale watu wao wote wamesoma sheria. Niwaombe ushauri wangu, kwa kuwa muda umekuwa mwingi na wale watu wameshafukuzwa kazini walitegemea kuwa wanakazi, lakini wanachukua muda, naomba sana Mhe. Waziri waangalie wale mawakili wa upande mwengine kwa yule mwekezaji, kwa sababu wanawapotezea muda. Wanawapotezea muda kwa sababu keshaona anashindwa na anajua wazi kuwa mimi nashindwa hapa, lakini anatumia mbinu ya uwakili ili kuweza kupoteza muda. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana. Mhe. Mwenyekiti, bado hakuna mtu niachie.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kutokana na hali halisi ilivyo kuwa hawa watu wajaribiwe kuweza kufanya ile kesi. Naam.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe una dakika tano za ziada.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Zitanisaidia hizo mheshimiwa. Hakuna mtu utafunga Baraza mapema sasa hivi, haya. Sasa mimi ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili suala wawahimize ili kuweza kufanikisha kazi vizuri sana. Pia niwaombee mishahara iangaliwe katika kitengo hiki ili kuweza kufanikisha kazi vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kusema siku moja hapa kwamba tutafungua Kampuni ambayo itakayowasaidia vijana katika wimbi la kuondoa umaskini. Mhe. Mwenyekiti, Kampuni hiyo tayari *Zanzibar Life Opportunity*, ina mashirikiano mazuri sana na wizara ya Mhe. Waziri, niwapongeze sana mheshimiwa Kampuni hiyo umeipa baraka zote na nguvu zote kwa mujibu wa sheria zilizoundwa katika nchi hii.

Kwa hivyo, niwapongeze sana na wanaijua na kazi yake wameshaanza kufanya na imo inahangaika vizuri kutafuta ajira za wananchi nje na ndani. Hii wakiitumia itaondoka na lile suala la vijana kunyanyaswa na kudhalilishwa, ina wataalamu wazuri, washauri wazuri na ina wanasheria wazuri Kampuni hii. Hivyo, ningeomba sana Mhe. Waziri azidi kujikumba na kujiweka karibu na kampuni hii ili kuleta ufanisi mzuri ndani ya Kisiwa hiki cha Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Kampuni hii imejieleza katika *foreigner*, halikadhalika hata kwenye wizara nyengine Wizara ya Fedha inajulikana Kampuni hii niwashukuru sana na wao wametupokea kwa vizuri kabisa, na Inshaallah Mwenyezi Mungu awabariki na kuwapa kila la kheri na wao na awaongezee mafungu yenye heri na wao.

Mhe. Mwenyekiti, nimalize. Kwa kumaliza kwangu, target yangu ya kumalizia. Naomba kuwe na mashirikiano kati ya wizara ya kazi na watu wa uhamiaji na wanawake na watoto, ili wafanikishe suala hili la zoezi la kuweza kuondoa matatizo katika mahoteli. Mhe. Mwenyekiti, wakishikamana watu hawa pamoja na Kamisheni ya Utalii, wakikamatana hawa mheshimiwa basi mimi naamini unyanyasaji katika mahoteli itakuwa hakuna na hii itakuwa basi kabisa.

Mhe. Waziri sijui umelisikia hilo suala, walikuwa wanakuzungumza wazee najua wanakupa vitu hapo. Nilisema na narudia tena niiombe Hansard ikae sawa. Mhe. Mwenyekiti, ushirikiane na uhamiaji, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ili kufanikisha azma ya kuondoa migogoro mheshimiwa hasa katika hizi kampuni pamoja na mahotelini, kwa sababu mkijumuika kwa pamoja basi na hili tatizo linaondoka wala hatuwapi kazi tena wale watu wa DHU, hatuna kazi hatutowapa kazi mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tumuunge mkono mwalimu wetu, tumuunge mkono waziri wetu, tumpe kila ushirikiano na sisi kwa mujibu wa sheria na tuipitishe kwa mwaka huu, kwa sababu mwaka huu hatuna kifungu cha kumkamata, isipokuwa tumuombee dua arudi na mwaka kesho katika hiyo *programme* yake ya *PBB* alivyoiweka tuingie huko. Nilimsikia juzi Waziri wa Fedha alisema kuwa sasa hivi hapa sio rahisi na ni kweli.

Kwa hivyo, tukijiingiza humo ovyo ovyo Mhe. Waziri atatubana, unamjua kazi yake mara anakupiga hivi hivi anakuweka sawa Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Spika, amepata mgeni na mgeni huyu yupo katika chumba chetu kile pale *gallery* juu, na ni Balozi wa Malawi, Mhe. Hawa O. Mbilowe. Kwa hivyo, nitamuomba asimame. Madam Hawa *you may stand-up*. *(Makofi)*

*You are most welcome to our House of Representatives here, and we are in the session now. Thank you very much. You may sit. Thank you. (Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kwishakupokea ugeni wetu huo. Sasa nina hamu ya kutaka kuendelea tena, lakini nasikitika sina jina jengine. Majadiliano yanaendelea. Mhe. Marina Joel Thomas na baadae Mhe. Mohammed Mbwana Hamad. *(Makofi)*

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma, Mhe. Haroun Ali Suleiman. Pia Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nitowe mkono wa pole kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein, kwa kufiliwa na mdogo wake. Mwenyezi Mungu ampe subra, awape faraja wale wafiwa wote na Mwenyezi Mungu amjaalie roho ya marehemu awekwe mahali pema peponi, amin.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe fursa hii kuipongeza serikali kwa kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Katika hotuba ya Mhe. Waziri ameeleza kwenye kitabu chake hicho suala zima la maboresho ya wafanyakazi, ambapo mwaka 2011 Mhe. Mwenyekiti, mishahara ya kima cha chini iliongezwa kutoka 100,000 hadi 125,000. Katika mwaka 2013 pia serikali imechukua jitihada ya kuongeza mishahara kwa wafanyakazi wa kima cha chini kutoka 125,000 hadi 150,000. Hii ni hatua nzuri kwa serikali inahitaji kupongezwa kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, na ukiangalia kwenye sekta binafsi, pia serikali imejitahidi kupandisha maslahi ya wafanyakazi, kutoka mshahara wa kima cha chini shilingi 70,000 katika sekta binafsi hadi 145,000, kama ni ongezeko la asilimia 107. Mhe. Mwenyekiti, hapa pia napenda kuipongeza serikali kwa moyo wa dhati kabisa kwa jitihada hii kubwa iliyoifanya.

Vile vile ukiangalia katika miaka ya nyuma kilio kilikuwa kikubwa cha wafanyakazi kuhusu maslahi yao. Hata hivyo, serikali ijitahidi, kwa sababu mahitaji yanaongezeka siku hadi siku na ikiona ina nafasi nzuri pia inaweza ikaongeza mishahara kwa sababu mahitaji ni mengi, na kila kukicha mishahara inahitajika kuongezeka. Kwa hivyo, naomba serikali ikiona hali inaruhusu basi iwaangalie tena wafanyakazi hao wa taasisi na hata sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika Idara ya Usalama Kazini. Katika hotuba yake Mhe. Waziri ameeleza ukaguzi katika maeneo mbali mbali ya sekta katika suala la usalama kazini. Ameeleza Mhe. Waziri kwenye kitabu chake katika ukurasa wa 27, ametaja kama maeneo 180 ambayo wamefanya ukaguzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi huu naishauri wizara iendelee kukagua, kwa sababu kuna sehemu nyengine wanayo matatizo katika suala zima la usalama wao. Kuna taasisi nyengine wanafanyakazi katika mazingira magumu kwa hivyo naomba ijitahidi kuendelea kukagua ili kugundua yale matatizo ambayo yako katika taasisi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda *page* 22 kuhusu suala zima la ufungaji wa CCTV kamera katika jumba letu la nyaraka, kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa suala hili na Wizara kwa jumla kwa sababu suala la nyaraka lilizungumzwa sana kipindi kama cha wiki mbili tatu zilizopita wizi wa nyaraka, lakini kutokana na hatua hii nahisi inaweza kusaidia kupunguza suala zima la upotevu wa nyaraka hizi, naomba niipongeze pia Serikali kwa hilo.

Pia wamesema Wizara inaendelea kuhifadhi hizo baadhi ya nyaraka na katika kiambatanisho nambari tatu (a) wameeleza baadhi ya nyaraka ambazo zimehifadhiwa yaani pia ni hatua nzuri, kwa sababu kuhifadhi vitu kama hivi muhimu vya Serikali inaweza kusaidia hata vizazi vyetu vya baadae kutumia nyaraka hizo.

Mhe. Mwenyekiti, tarehe 12 niliulizia katika siku ya uuguzi duniani na katika malalamiko yao wauguzi hao walitoa kama malalamiko matatu, nao walisema kuhusu suala zima la maposho ambayo wanapata hayaligani na elimu yao kwa hivyo suala zima la maposho kwa wauguzi kulingana na elimu yao kilikuwa ni kilio chao, pamoja na mishahara hailingani kutokana na elimu waliyokuwa nayo.

Kwa hivyo Mheshimiwa Wizara hii ya Utumishi kama ndio inayodili na maslahi ya watumishi naomba Mhe. Waziri nalo hili waliangalie, ili waweze kuboresha hawa wauguzi maslahi yao ambayo ni kilio chao ambacho walikitoa siku ya wauguzi duniani.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika suala zima la Chuo cha Utawala wa Umma napo hapa katika vyuo vyetu hivi nimejitahidi kutoa taaluma, lakini kuna baadhi ya changamoto ambazo zipo na kuhusu wafanafunzi suala zima la mikopo, najua ina-*deal* na Wizara ya Elimu lakini kama Wizara ya Utumishi nayo iangalie ni jinsi gani ambavyo itawasaidia hawa wanafunzi mbali mbali wanaohitaji mikopo na wengine wanaendelea kusoma, lakini katika vyuo mbali mbali kama hivi wanakuwa katika hali ngumu ya kuendelea na masomo yao, kwa hivyo kama Wizara ya Utumishi nayo iliangalie suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia suala zima la ajira, ajira ni tatizo na Mhe. Waziri ameeleza ajira ambazo zimetolewa kwa kipindi hiki, lakini sasa hivi mahitaji ni makubwa ya ajira ukilinganisha na nafasi zenye fursa zenyewe ambazo zipo za ajira, lakini hata hivyo Wizara imejitahidi kwa ajili ya wafanyakazi ambao kwenye kitabu sihitaji kwa ajili ya kuokoa muda ametaja hizi ajira ambazo wamezitoa katika taasisi mbali mbali.

Kwa hivyo, naomba Wizara nayo isichoke na ijitahidi kwa sababu mahitaji ni mengi vijana wapo wengi kwa hivyo Serikali naomba ijitahidi hata kuzidisha huo mfuko wa kujitegemea ambao unasaidia vijana wetu kujiendeleza kwa shughuli mbali mbali za kijamii. Kwa hivyo naomba iongeze wigo kwa vikundi mbali mbali na vijana wetu, ili waweze kujishughulisha katika kuendeleza shughuli zao mbali mbali, hatimae kupata kipato katika kuendesha maisha yao.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la maboresho ya mishahara kama nilivyosema, lakini kuna hawa walimu ambao kuanzia miaka kumi mpaka kumi na tano imeelezwa maslahi ya 14 April 2015 yaliongezwa maslahi ya walimu, lakini katika wale waliofanya kazi katika miaka kumi na sita hadi ishirini na tisa.

Naomba Mhe. Waziri suala hili alifanyie kazi awaangalie waalimu hao katika miaka hiyo waliyofanya kazi. Kwa sababu kuna malalamiko ambayo nimeyapata kutokana na uzoefu wao wa kufanya kazi, kuanzia miaka kumi na kumi na tano waliangaliwa maslahi yao katika Mwezi wa April, 2014 lakini katika miaka hii ya 16 mpaka 29 naomba Mhe. Waziri aifanyie kazi, ili kuona kwamba kama kuna ukweli na kama kuna ukweli naomba hili suala alifanyie kazi, ili apate kuwaboreshea maslahi yao walimu hao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono bajeti kwa asilimia mia moja. Ahsante sana *(Makofi)*

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu subuhanahu wataalla kwa kutujaalia mchana huu kuwepo katika Baraza lako kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Lakini la pili nikupongeze kwa kunipa nafasi ya kuchangia na mimi ijapo kwa muhtasari hotuba ya bajeti iliyopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Waziri Mhe. Haroun Ali Suleiman kwa uwasilishaji wake wa hotuba ya bajeti ambayo iko mbele yetu ya mwa mwaka 2015/16 ya Wizara yake Afisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi pia nichukue nafasi ya kumpa pole Rais wa Zanzibar kwa kifo cha dada yake ambacho kilitokea jana, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi na pia awape moyo wa subira wafiwa wote, huku tukijua kwamba *innalillahi wainna ilayhi raajiuuna*. Kwa tamko hili litawaliwaza wale wafiwa pamoja na wasikilizaji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu ukurasa wa sita kifungu cha kumi na tisa, naomba ninukuu kumuhtasari. "Katika kutekeleza ahadi hizo za ilani ya CCM kama ilivyoelezwa hapo katika kifungu cha 18 Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha mifumo ya utumishi wa umma inayozingatiya sera sheria na kanuni za kazi pamoja na mikataba ya utoaji huduma, ili kuhakikisha kwamba inajenga mazingira mazuri kwa watumishi na kuhakikisha watumishi wa umma wanatekeleza wajibu wao ipasavyo kwa vya kuwatumikia wananchi". mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nilizungumze hili kwamba watumishi wa umma wanatakiwa watekeleze wajibu wao ipasavyo vya kuwatumikia wananchi, Mhe. Mwenyekiti, haki na wajibu ni watoto pacha mtu anapotekeleza wajibu wake anastahiki kutekelezewa haki zake, kwa masikitiko makubwa kuna watumishi wa umme kutoka Wizara ya Elimu, waalimu kadhaa baada ya marekebisho ya mishahara ya mwaka 2011 ilikosewa mishahara yao na wakapeleka malalamiko yao Wizara ya Utumishi Serikalini na tumelizungumza hili hata katika Baraza lililopita, kwamba walimu hawa kuna miezi mitatu wengine miezi miwili hawakulipwa pesa zao baada ya marekebisho.

Kwa hivyo nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Utumishi wa Umma atwambie alikuwa na mikakati gani ya kuhakikisha kwamba watumishi hawa kama walimu wamekosa maslahi yao na huku wanatekeleza wajibu wao.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo na ni tatizo kubwa sana walimu ni miongoni mwa wafanyakazi wanaofanya kazi ngumu, wanaolipwa maslahi ambayo hayatoshelezi leo walimu hawa wamekwenda na kurudi lakini hadi leo mishahara yao hii baada ya marekebisho mikato yao ya miezi mitatu au miezi miwili hawajaingiziwa hadi leo hii.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Waziri wa Utumishi wa Umma atwambie na huku tukiwa tunaendelea na bajeti na huku tukiwa tunamaliza baraza la miaka mtano hii ambayo tunaendelea nayo tokea 2010, anawahakikishia nini wafanyakazi hawa duni ambao wamekwama hawajui waende wapi na mdomo wa wafanyakazi hawa ni Wizara yao ya Elimu pamoja na Wizara ya Utumishi wa Umma.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atueleze kwa kina ili waalimu hawa wasikie juu ya kupata haki yao hii ambayo wameshaifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa saba kifungu cha 21 naomba ninukuu, kinasema;

" Mhe. Spika, kwa upande wa maslahi mwaka 2011 Serikali ilipandisha mishahara ya watumishi wa umma kutoka kima cha chini cha mshahara wa Shilingi laki moja hadi shilingi laki moja na ishirini na tano kwa mwezi, sawa na ongezeko la asilimia ishirini na tano. Serikali pia ilifanya marekebisho ya vianzio vya mishahara ya wataalam mbali mbali wakiwemo madaktari na walimu wa sayansi katika mwaka 2013 Serikali ilipandisha kima cha chini cha mshahara kutoka T. Sh. 125,000 hadi 150,000 sawa na ongezeko la asilimia ishirini. Pamoja na kurekebisha mishahara ya watumishi wazoefu waliotumikia utumishi wa umma kwa miaka kumi na tano na zaidi ambao wana mishahara kati ya 150,000 hadi 225,000".

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri Serikali kuwapandishia mishahara watumishi wake kwa asilimia ishirini, lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie jinsi ya maisha yalivyo hivi sasa maisha ya Wazanzibari bado ni magumu na yanapanda siku hadi siku hivyo mfanyakazi wa Serikali ya Zanzibar unamlipa shilingi laki moja na hamsini atumie nini, na nguvu zake zote, akili yake yote iko kazini kwake anashindwa kufanya majukumu mengine isipokuwa anafanya majukumu ya kulijenga taifa hili.

Kwa hivyo naomba pamoja na ongezeko hili ambalo Serikali imejitutumua lakini bado ongezeko la kima cha chini cha mshahara kwa shilingi laki moja na hamsini bado wafanyakazi wapo katika hali duni.

Niiombe Serikali kwa vyovyote ifanye mipango endelevu watumishi wa umma angalau basi wafikie kiwango cha chini angalau hichi cha shilingi laki mbili na

hamsini, sio laki mbili na ishirini na tano au laki moja na hamsini, angalau laki moja na hamsini ili waweze na wao kujitononowa.

Mhe. Mwenyekiti, fedha inashuka kila siku na fedha zinaposhuka matumizi yanapanda kwa hivyo tusiangalie kwamba tunamlipa mfanyakazi shilingi laki moja na hamsini tukaona kwamba mfanyakazi huyu tumemuweka katika mazingira mazuri, fedha hizi tunazowalipa wafanyakazi wetu zinahitaji kwao mambo mengi ikiwa ni pamoja na chakula chao na familia zao, lakini pamoja na huduma za kuwasomesha watoto wao, pamoja na huduma za kuwatibu watoto wao. Laki moja na hamsini ni pesa ndogo sana ambayo haiwezi hata kidogo kuweza kumtatulia matatizo mfanyakazi huyu ambae hivi sasa tunategemea kwamba awe ndiye anayeliendeleza taifa hili kwa kupatikana ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo niende katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/15 kifungu cha 53 naomba ninukuu.

Kifungu cha 53 kinasema hivi " Kwa mwaka wa fedha 2014/15 Idara imefanya utekelezaji wa kuwapanga watumishi katika miundo ya utumishi yaani *Scheme of Services* kwa Wizara, hatua za ukamilishaji wa Wizara mbili zilizobakia zinaendelea, ni mategemeo ya Wizara hii kwamba mwanzoni mwa mwaka mpya wa 2015/16 watumishi wote watakuwa wamepangwa katika madaraja yao kwa mujibu wa miundo ya utumishi".

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba Mhe. Waziri kwanza aniambie hizo Wizara mbili ambazo hazijapangiwa *Scheme of Services* ni Wizara gani na Wizara gani, lakini pia nimuulize Mhe. Waziri Wizara 14 zimeshapangiwa *Scheme of Services* na inategemea kwamba wanalipwa mishahara yao kwa mujibu wa uzoefu wao wa kazi.

Je, hizi Wizara mbili ambazo hadi leo hazijapangiwa hapo watakapopangiwa muundo wao wa utumishi wataanza kulipwa mshahara huu mpya sambamba na hao waliokwisha kufanyiwa *Scheme of services* au wataanza kulipwa mshahara mpya pale tu watakapoanziwa *Scheme of services*, lakini kama watalipwa mshahara mpya pale watakapoanziwa *Scheme of services* hawa hatuoni kwamba tumewabagua kwamba wenzao tumewafanyia *Scheme of Services* katika kipindi cha mwaka uliopita na tumeanza kuwalipa, hawa tuwafanyie *scheme of services* katika mwaka ujao na tuwalipe pale mwaka ujao. Je? hatuoni kwamba hawa itakuwa tumewabagua.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mchango wangu niende katika Idara ya Nyaraka na kumbu kumbu za kitaifa ukurasa wa 22,  Mhe. Mwenyekiti Idara ya nyaraka na

kumbu kumbu za taifa ni idara muhimu sana kwa sababu idara hii imebeba kumbu kumbu historia, uelewa wa mambo mbali mbali ya taifa hili.

Sasa basi kwa kuwa katika baraza lililopita kulikuwa na hoja ile ya wizi wa nyaraka alizungumza Mhe. Mshimba hapa kiuchache na mimi nizungumze kiuchache nimuombe Mhe. Waziri aje atueleze Serikali imechukua hatua gani juu ya michango mbali mbali ya kamati ile teula pamoja na michango mbali mbali ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kipindi kilichopita. Lakini Mheshimiwa niipongeze Idara hii kwamba imefunga CCTV kwa mujibu wa maelezo hili ni jambo zuri na litalinda ule wizi ambao ulitokea katika kipindi kilichopita.

Jengine ambalo nataka nilizungumzie katika Idara hii kwamba katika michango yetu mbali mbali iliyopita tulikuwa tunasema kwamba kuna nyumba ya raia ambayo ipo karibu sana na idara hii imo ndani ya senyenge ya idara hii, na Serikali tuliishauri mara nyingi ili ionane na mwenye nyumba huyu wakubaliane watakavyokubaliana, lakini vyovyote kwamba hapa kuwe na utaratibu maalum wa eneo hili lisiwe na nyumba ya raia karibu.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atueleze wamefikia hatua gani ili kujua kwamba Serikali inalitumia vipi eneo lile pamoja na nyumba hii ya raia ambaye anakaa pale.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 25 niende katika Idara ya Ajira. Mheshimiwa Idara ya Ajira kuna mambo mengi ambayo yanahitajika hapa yafanye kazi. Kwanza ningemuuliza Mhe. Waziri kuna kundi kubwa la vijana wetu wa Kizanzibari ambao wamesomea uwalimu miaka karibu saba iliyopita lakini mpaka leo walimu hawa hawajaajiriwa katika ngazi ya cheti.

Je, Idara hii ya Ajira ina mpango gani kuwaajiri walimu hawa, walimu ambao wanahitajika kila siku kwa sababu tunaupungufu mkubwa wa walimu katika maskuli mbali mbali. Je, Wizara ya Utumishi wa Umma kupitia Idara yake ya Ajira ina mpango gani ya kuwaajiri vijana hawa ambao wameshasomea uwalimu kwa kipindi kirefu sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumzia katika Idara hii kwamba katika kipindi cha miaka mitano hii 2010 mpaka tunamalizia sasa hivi 2015 ni wafanyakazi wangapi ambao wameajiriwa katika Utumishi wa Umma na mgao wake Kiwilaya na Kada zao ulikuwa namna gani.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wa wafanyakazi walioajiriwa katika kipindi hiki cha miaka mtano na pia anipe mchanganuo wa kada mbali

mbali pamoja na mgao katika Wilaya mbali mbali ambazo tunazo katika Zanzibar yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huu niunge mkono hotuba hii kwa asilimia 90 na asilimia kumi nitaziingiza pale tu nitakapopata ufafanuzi juu ya yale ambayo nimeyatakia ufafanuzi. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Asante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutujaalia afya njema na uwezo wa kutoka katika maeneo yetu mpaka katika jengo hili lenye heshima kubwa Baraza la Wawakilishi tukiwa hai, tena kwa miguu yetu bila ya kushikiliwa. Hii ni hazina kubwa aliyetujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti. Pamoja na kwamba natoka katika mambo ya ugonjwa ugonjwa lakini ukaamua kunipa nafasi hii ya kuchangia nafasi ya pili katika mchango huu wa leo. Mimi naamini wenzangu wengi wapo wameshaleta lakini umenipa miye kwa kunijali na kwa kunipenda. Kwa hivyo kwa heshima kubwa nasema asante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri ambaye ametuletea hii hotuba yake Mhe. Haroun Ali Suleiman.

Napenda nimpongeze sana, sio tu kwamba hii hotuba yake imetayarishwa vizuri. Lakini hata katika utaratibu aliotusomea kwa kweli alikuwa makini sana katika kuitiririsha hii hotuba katika mambo ya vina pamoja na vibwagizo. Kwa kweli amejitahidi sana Mhe. Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma na ameonyesha umahiri wake na umakini wake katika mambo, nasema asante sana Mhe. Waziri.

Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa nadhani niende moja kwa moja sasa katika hotuba ya Mhe. Waziri. Mimi sio msemaji sana Mhe. Mwenyekiti, katika masuala haya ya Utumishi wa Umma mimi si msemaji sana katika maeneo haya, maeneo yangu ya utaalamu ni katika mambo ya viumbe hasa miti, lakini katika mambo ya Utumishi wa Umma sio mtaalamu sana, lakini nitatia nyalio tu kidogo ili pengine Mhe. Waziri zinaweza zikamuweka sawa nyalio hizi katika suala zima la kuendesha Ofisi yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nizungumzie suala hili la ajira. Mhe. Mwenyekiti, tumeona katika ukurasa wa 5 katika ibara ya 16 kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kusimamia na kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi

(CCM) katika sekta mbali mbali kwa lengo la kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilikuwa naomba Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla ione kwamba ajira ni miongoni kwa keki ya taifa (*national cake*) kwa hivyo kila Mzanzibari angehitaji kupata hii keki ya taifa aweze kumung'unyuwa na yeye afaidike nayo hiyo keki ya taifa, tena bila ya kujali rangi, bila ya kujali kabila, wala kujali wapi anatoka, kila mtu anastahiki kupata ajira.

Mhe. Mwenyekiti, humu Mhe. Waziri katangaza kwamba takriban kuna ajira 5667 zilizotolewa za serikali, hizi ndio nitahoji tena za binafsi na ajira nyengine sio za kuzisemea sana. Lakini nilikuwa nazungumzia hizi ajira 5667 hizi za serikali ambazo waajiriwa hawa huwa wanatumia hela za walipa kodi katika kulipwa mishahara na mafao yao mengine.

Sasa hizi Mheshimiwa nilikuwa naomba atakaposimama anieleze ajira hizi 5667 ngapi zilitolewa hapa Unguja na ngapi zilitolewa kule kisiwa chengine upande mwengine wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu nimejaribu kufanya tafiti nyingi sana katika nchi mbali mbali, nikaona katika kugawa hii keki ya taifa ya ajira wanatoa *priority* kwa wazawa nchi mbali mbali, hata hizi zilizopo katika Jangwa la Sahara Mhe. Mwenyekiti. Mimi nimejaribu kufanya kuangalia zile nchi za Huba nikaona kwamba maslahi ya watumishi wa serikali baadhi ya nchi zile za Huba ikiwa zinatofautiana sana baina ya wazawa na wageni. Ajira katika nchi zile za Huba wanaopewa *priority* ni wazawa ukilinganisha na wageni.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba baada ya tafiti za kina imeonekana kwamba ajira katika Zanzibar zina tatizo kidogo. Kwa sababu huwezi kupata ajira katika nchi hii kama huna kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, huwezi. Kuna Wazanzibari wengi hapa hawana vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi, ni tatizo. Sasa Mheshimiwa unapotangaza ajira anapoambiwa upeleke kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi huna na wewe unalipa kodi katika nchi na wewe unalipa kila kitu katika nchi hii, unajikutia unakosa ajira kwa sababu huna kitambulisho cha Mzanziari Mkaazi.

Mimi nadhani ili kuwafanya Wazanzibari tusiwabaguwe katika mambo haya basi tufanye jambo moja. Aidha, wote wapate vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi ili ikija ajira apate au yaondoshwe masharti ya Mzanzibari Mkaazi katika hii fani ya ajira. Kwa vile ukishakuonekana kwamba ume-*qualify* katika mambo yanayotakiwa pale basi hiki kitambulisho cha Uzanzibar Mkaazi kisitiliwe maanani. Wengi sana Mheshimiwa hawana na kwa kweli ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia suala la maslahi kwa watumishi wa umma hapa nchini. Maslahi kwa watumishi wa umma nayo ni tatizo vile vile. Kwa mfano ongezeko alilotoa Mhe. Rais kipindi kile cha 25,000/- kwa kila mtumishi wa serikali, ilikuwa *equal distributed* kwa watumishi wa umma hii 25,000/-.

Kwa bahati Wizara nyengine wale wafanyakazi walipata kwa wakati ule ule pengine mwezi wa pili au watatu baada ya tangazo lile la kuongezwa ajira zile. Lakini kuna baadhi ya wizara wamechelewa sana kupata zile 25,000/- si dhani kama zimemaliza zote kupewa 25,000/- Wizara hizi.

Mheshimiwa inasikitisha sana kuona kwamba kuna watu wamechelewa kupewa na *areas* zao mpaka sasa hivi hawajapata. Kwa mfano ZBC, wafanyakazi wengi wa ZBC wananung'unika sana kwamba zile *areas* zilichelewa kutolewa lakini mpaka zilipotolewa ni juzi juzi tu zimetolewa lakini *areas* zao hawajapata.

Hili ni tatizo Mheshimiwa naomba uwafatilie hawa, hawa jamaa zetu wa ZBC wanajitahidi sana katika kuutumikia umma ikiwa ni pamoja na sisi kwenye hili Baraza letu wanajitahidi kuchukua habari, lakini unakuta kuna viposho vyao kama hivyo *areas* zao mpaka leo hii hazijapatikana, Mheshimiwa hilo ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, serikali lazima ikubali kwamba posho na mishahara ni kama *catalyst* kwa mfanyakazi. *Catalyst* nimetumia neno hili lakini ni kichocheo, Mhe. Waziri anafahamu kwamba *catalyst* ni kitu chochote kinacho-*speed reaction* katika *chemical reaction*. Sasa ukimlipa vizuri mfanyakazi, ukimpa mshahara mzuri, ukimpa posho vizuri, basi ninachoaamini Mhe. Waziri mfanyakazi huyo atakupatia utumishi uliomakini sana na wenye kutukuka.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona kwamba ukiviangalia viwango vya mafao ya watumishi wa umma katika nchi mbali mbali ni vizuri. Sisi tumefanya tafiti sana tukaona Zanzibar tuko nyuma sana. Watumishi wa serikali sasa hivi katika nchi hii wanaishi katika mazingira mazito, kwa sababu ya viwango vidogo vya maslahi yao. Mheshimiwa pamoja na kwamba mmejitahidi kuongeza mafao lakini hayaowani na hali ya maisha ya sasa. Hivi sasa mfanyakazi hawezi kupata hata nusu ya mahitaji yake ya siku kutokana na hili.

Ukiangalia watumishi wa nchi tuseme nchi za Huba wana-*afford* kila mtumishi wa umma anausafiri. Sisi huku Zanzibar hawezi ku-*afford* hata kununua viatu, achilia mbali kupata usafiri ha-*afford* kununua buti. Mtumishi wa umma ukimuangalia chini anakwenda na yeboyebo, hawezi kununua buti, hili ni tatizo. Nadhani Mhe. Waziri katika hili una haja ya kuri-*view* maslahi ya watumishi wa umma na hali ya maisha ilivyo kwa sasa.

Wenzetu wanavyowajali watumishi wao hakuna *public transport* katika nchi hizi za Huba kwa mfano kama pale Oman huwezi kuona *public transport*, kila mfanyakazi ana usafiri wake na wala hanunui anakopeshwa na serikali. Sasa huku wewe kweli utatumia shilingi laki mbili na elfu hamsini halafu mtu huyo umkopeshe gari atalipa? Mhe. Mwenyekiti, katika hili naomba kwamba maslahi yako chini na naomba sana yaangaliwe upya.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu maposho sasa. Maposho posho la mfanyakazi humfaa pale ambapo posho lile analihitaji. Lakini inasikitisha sana Mheshimiwa kwamba kuna baadhi ya wizara wafanyakazi wanafanya kazi na wanastahiki maposho lakini maposho hayawafikii kwa wakati. Kwa mfano hivi juzi, sio juzi tena karibu miezi tisa iliyopita, wafanyakazi wa Mafunzo ya Amali, walimu wa Unguja na Pemba walipata safari ya kwenda Iran. Walimu wale walikwenda Iran kwa ajili ya safari ya kimafunzo karibu mwezi mzima kule.

Tatizo lilokuwepo Mheshimiwa wale *allowance* waliambiwa subirini, tutakuja kuwapa na nini wakawambia kopeni mkirudi mtakuja kupewa. Lakusikitisha Mhe. Waziri Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar wamekwenda Iran, wamerudi huu ni karibu mwaka hawakupata posho lao hadi leo hii.

Haki ikichelewa kutolewa Mheshimiwa basi ni sawa sawa na kama haikutolewa kabisa. Sasa mimi nataka Mhe. Waziri aje anieleze hapa kwamba wale walimu wa Mafunzo ya Amali waliokwenda Iran mwaka jana walistahiki kupewa posho la kutoka nje au hawakustahiki. Kama walistahiki kupewa kwa nini hadi leo hawajapewa posho lile, hilo la kwanza.

La pili Mheshimiwa kuna utaratibu wa kuwapandisha mishahara watumishi wetu kila baada wanapomaliza kozi zao za mafunzo, huu ni utaratibu sio wa nchi yetu tu ni wa nchi mbali mbali. Lakini inasikitisha kwamba katika Mawizara kadhaa wafanyakazi huwa wanamaliza mafunzo yao bila ya kurekebishiwa mishahara yao au wanachelewa sana kurekebishiwa mishahara yao.

Mimi namjua mfanyakazi wa Wizara ya Elimu pale Pemba, yeye yupo katika kitengo cha Uhasibu anaitwa Ali Ali Khamis. Huyu bwana kamaliza Masters *Degree* katika masuala haya ya *financial management* Chuo kimoja hapo Dar-es-Salaam ni Chuo kinachotambulika na NECTA ni cha zamani. Lakini inasikitisha sana mfanyakazi huyu pamoja na kuhangaika sana ndugu Ali Khamis huu ni karibu mwaka wa pili tangu amalize *Masters Degree* yake hadi leo hii hajarekebishiwa mshahara wake, tatizo liko wapi? Mhe. Waziri tatizo liko wapi mpaka huyu kijana hajarekebishiwa mshahara wake na yeye keshamaliza.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili nimelieleza muda mrefu sana kwa sababu vijana wamekaa miaka mingi sana. Sasa wataalamu wanapotea sana kwa dharau, tunawadharau watumishi wa umma. Yaani tunawadharau pale wanapomaliza masomo yao kurekebishia mishahara, tunawadharau na kwamba Sera ya Utumishi wa Umma haiipi kipaumbele kwa wataalamu ndio ikabidi wanatukimbia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimetembelea hospitali moja ya binafsi pale kuna gynecologist mmoja alikuwa hapa Wizara ya Afya Zanzibar, yupo katika *private* hospital sasa hivi. Anasema mimi siwezi kurudi kule, yaani hapa nimepewa gari hii, na napata karibu milioni mbili nikikusanya marupurupu yangu yote. Hapa eti mwalimu wa sayansi tunamrekebishia shilingi laki mbili na elfu hamsini. Mwalimu wa sayansi laki mbili na elfu hamsini? Tatizo. gynecologist analipwa shilingi laki sita, laki tano hapa, kule milioni mbili na zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hetu tujiangalie tatizo lipo wapi. Lakini mimi nilikaa nikatafakari weeeeh! nikaona tatizo kumbe nimeshalijua. Kumbe ilani inayosimamia mambo haya ya ajira ni ile ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo nawaambia wafanyakazi na watumishi wa umma wa nchi hii msiwe na wasi wasi, tatizo hili litakapofika mwezi wa Oktoba tukijaaliwa uhai na uzima mwezi wa kumi, ilani hii ya Chama cha Mapinduzi tunaiweka pembeni mujitahidi kabisa kuingiza ilani ya Chama cha CUF kusudi utumishi wa umma uweze kuwa makini na mtajisikia vizuri na mtarudi katika nchi hii.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri, asante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Asante sasa ni nafasi ya Mhe. Ashura Sharif Ali na baadaye Mhe. Salma Muhammed Ali.

**Mhe. Ashura Shariff Ali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia uhai lakini pia akatupa na uzima na akatuwezesha kuwepo kwetu hapa kutekeleza majukumu yetu, lakini haya yote ni kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia nami fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika bajeti hii iliyoko mezani wakati huu. Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe fursa hii kumpongeza mwalimu wangu Mhe. Waziri Haroun kwa uwasilishaji wake na maneno yake ya fasaha sana ya kitabu hiki. Pia niwapongeze watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni wizara ambayo imebeba dhamana ya utendaji wa shughuli mbali mbali za Serikali kwa ajili ya kuleta ufanisi wa shughuli za

kihuduma za jamii katika mambo yetu mbali mbali kwa taasisi zetu zote za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika bajeti hii nianze kuchangia kuanzia Idara hii ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa. Nataka niseme kwamba Taifa na Nyaraka ni mambo muhimu sana, wenzangu walitangulia kusema hapa kwamba Baraza hili hili iliundwa Kamati Teule ambayo ilikwenda kushughulikia upotevu wa nyaraka zetu. Bahati nzuri mambo mengi ambayo Kamati ilikuja nayo na mapendekezo nilikuwa natarajia kwamba utekelezaji wa hayo ningeyaona katika kitabu hiki, pamoja na maelezo mafupi sana, ambayo Mhe. Waziri ameyasema katika kitabu chake hiki, nilikuwa nadhani kwamba kutaonesha waziwazi kwa mambo mbali mbali yale ambayo yaligusa na ikawa ni athari kwetu kupotelewa na nyaraka zetu muhimu ambazo ndio taifa misingi yake mikuu na utaratibu mzima ambao unalionesha kwamba taifa letu ndio uhai wake.

Ningemuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze basi katika yale mapendekezo ni yepi hasa yaliyofanyiwa utaratibu ya kuweza kutekelezwa, humu tumeona kwa jumla jumla lakini pia atueleze mbali na yale mengine kuna mabadiliko gani katika taasisi ile, kwa utaratibu ule uliojitokeza pale atueleze tuweze kujua. Kwa sababu tumeona kwamba kuna mambo ambayo yalikuwa ni watendaji waliofanya ubadhirifu wa makusudi au walifanya uzembe katika shughuli zile, tuweze kujua basi Serikali katika hili ime-*react* vipi.

Mhe. Mwenyekiti, nije tena kuhusu fedha za bajeti ambazo Pemba hazikwenda katika ukarabati wa jengo. Niiombe Serikali ituambie hivi kuna sababu zipi za msingi mara nyingi taasisi zile za Pemba zinapoingiziwa fedha huwa haziendi. Hebu tuambieni kila bajeti inayokuja mara nyingi ufinyu tunaukuta ama kwa Afisa Mdhamini Pemba ama utakuta ni Taasisi ambayo iko kule Pemba hebu tupeni hasa, kuna nini katika mgao wa fedha hizi mpaka zinakuwa hazifikii kule.

Hizi ni Taasisi zilizo sawa na Taasisi ziliopo hapa, kwa hivyo ni vyema mgao huu ukawa unakwenda kwa usawa kabisa, kwani tunapoona kuna ufinyu wa mambo sisi tupo katika misingi ya kufuata sheria na utawala bora katika taifa letu. Iweje leo Taasisi nyengine ziwe finyu hazifanyiki kazi na nyengine ziwe zinapewa pesa, kuna mambo yanakuwa kidogo hayaleti raha na wafanyakazi nao hawajisikii na wao pia kuishi katika majengo mazuri wanahisi raha. Mhe. Mwenyekiti, hiyo ninaiacha hapo.

Sasa nije hapa kwenye ajira kwa vijana ambayo Mhe. Waziri ameitolea ufafanuzi wake katika kitabu chake kwamba kuna nafasi hizi za miaka 4 karibu kumi na tisa elfu mia saba na hamsini na nane kwa miaka 4 ambao watu wake wameajiriwa vijana hawa. Lakini ningependa kupata ufafanuzi kidogo niweze kuelewa kwamba

hao vijana walioajiriwa Serikalini ni Taasisi zipi hizo hasa walizoajiriwa vijana hawa, tuzielewe na ni wangapi hao walioajiriwa katika kila hiyo taasisi.

Pia wamesema kwamba kuna watu wameajiriwa katika mashirika ya umma nao pia tungependa kujua ni mashirika gani hayo ambayo wameajiriwa watu hao na idadi yao pia tuweze kuipata kwa kila hiyo taasisi yenyewe shirika lenyewe la umma, lakini kuna ajira zisizokuwa rasmi. Mheshimiwa tunaomba utupatie ufafanuzi tuzielewe wazi hizo ni zipi hasa zilizotoa ajira hizo ambazo haziko rasmi na idadi ukawa unayo, lakini ni kazi zipi hizo ambazo wameajiriwa tungependa kupata ufafanuzi wake.

Jengine ni kusema kwamba taifa letu kwa wakati huu tuna vijana wengi ambao wana uwezo wa kufanya kazi. Mhe. Waziri pamoja na haya ambayo umeyaeleza ya miaka 4 na ukaona miaka 4 mengine mpaka 2018 nimeona hapa kwamba umesema hivyo. Hebu tuambie ni Taasisi gani unazofikiria tunaweza tukaweza kuzalisha ajira na vijana wetu tukawaajiri, hususan hawa wanaomaliza vyuo.

Mhe. Waziri ningependa kusema kwamba  umefika wakati sasa kwa Serikali kuandaa hasa utaratibu wa uzalishaji wa hizi ajira zenyewe si yale mambo tu ya mas-hara ya kurukia rukia. Kwa sababu haya yote hayaoneshi kwamba kuna mpango madhubuti unaoonesha kwamba vijana watakapomaliza masomo yao basi watakwenda kwenye hili na hili kwa kuonesha kwamba tunazalisha hizo ajira.

Inaonesha wazi kama labda tungekuwa na mipango pengine ya uvuvi wa bahari kuu, pengine tungejua ni vijana wangapi tunaweza tukawaajiri kwa sababu ni malengo yetu tumejiwekea. Lakini pia tukaona kwamba tunataka kuweka viwanda, viwanda hivyo vitakuwa vingapi na vitakuwa na uwezo wa kuwachukua wangapi tungeona na tungekuwa tuna uhakika kwamba hizo ajira ambazo tunazihitaji zitawafikia kweli hao na kama haikufikia asilimia hiyo, lakini tuna hakika ya vijana wetu pengine wangeweza kufikia huko.

Mhe. Mwenyekiti, nije hapa katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma nazigusa hapa kuna maslahi ya wafanyakazi jambo ambalo kimekuwa kilio kikubwa kwa wafanyakazi hususan wa mahotelini. Hawa Mhe. Waziri kwa upande wako wa takwimu zako hizi ambazo wanatupatia katika kitabu chako hiki cha bajeti, hebu tusaidie mbona tuna matatizo mengi ya vijana wetu katika ajira, je zinapitia kwako wewe ndie mtu wa kazi.

Hawa mara nyingi wanakuwa mikataba yao haifungwi na ikifungwa haiheshimiwi wapo watu wa kuhangaika hangaika tu. Leo hapa unafanyakazi miaka mitano, sita, saba lakini hatimaye wanatimuliwa na mara nyingi wanakosa haki zao.

Mhe. Waziri kwa kuwa sasa hivi taifa letu limeingia katika uwekezaji na utalii na ajira nyingi zinapatikana huko hebu tuambie hawa vijana wanaoajiriwa hasa mahotelini mikataba yao hasa hii nani anaishughulikia unaifahamu kwa kina mikataba yao hawa na kama unaifahamu ni kwa sababu gani inatokea migogoro baina yao na hao watendaji wa mahotelini au hao wamiliki wa mahotelini. Nini kinasababisha hayo mara nyingi tumeshuhudia wengi wao wakiwa wanawake, maskini wanafanya kazi lakini ukifika muda basi maskini wanafukuzwa kiholela holela na haya nimeyashuhudia juzi *Sea Cliff Hotel*, walijenga wakahangaika wakasoneneka wamefukuzwa bila ya kujali mikataba hiyo wako nje.

Ninakuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa unipatie hilo na kwa sababu nia ya uwekezaji wetu ni utalii kwa wote ndio sera yetu, basi kama kwa wote hawa ambao wamepata fursa ya kuajiriwa wadumu katika ajira hizi ili kuondosha hayo makali ya maisha waweze kumudu maisha yao, sio kuajiriwa siku 3 ya 4 wametoka nje. Mheshimiwa naona hili kwanza ulisimamie kwa kina.

Jambo jengine ambalo nataka kulizungumzia ni wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari, huko jamani kuna matatizo, Mhe. Waziri unajua kulikoni watu wanaofanya kazi ambao hauheshimiwi na wala haki za msingi za binaadam, hata kama umepewa eneo la kufanyia kazi baada ya muda fulani ufike kama umemaliza kazi uondoke unaambiwa huwezo kuondoka muda wa saa 11 ifike. Huku wakiwa wanahangaika hata na hiyo mishahara yao ni usumbufu Mhe. Waziri naomba na hili unipatie jibu.

Si hapo tu kuna wafanyakazi wa Kichwele ambao wapo huko Kitope juu, Mheshimiwa kuna tatizo pengine hamzijui lakini sisi kwa kuwa ndio wasemaji wao sisi ndio midomo yao tunakwamba Mhe. Waziri wafanyakazi wa Kichwele wana matatizo tena mengi na makubwa.

Taasisi yako hii ni Taasisi ya Serikali ione kwamba inachunga haki za msingi za wafanyakazi hawa. Naliunganisha hili pamoja na posho la walimu wanaokwenda likizo, hizi ni haki zao za msingi wao tumesema ni wafanyakazi kama walivyo wafanyakazi wa taasisi nyengine, hivi kulikoni jamani kwa walimu au kwa kuwa wengi ni wanawake, maana yake walimu wengi ni wanawake maana yake matumizi hawayajui.

Mhe. Waziri nataka nikwambie katika taifa hili nguvu kazi ya taifa kubwa inafanya na wanawake. Ukija kwenye taasisi za Serikali na ukiingia katika mambo ya uzalishaji kwenye wakulima taifa hili linapata mafanikio yake kupitia wanawake. Uweje walimu hawa waende likizo au wasahiishe mitihani wafanye kazi na miezi 6 baadae ipite au mwaka halafu ndio wapewe haki zao, kulikoni. Mhe. Waziri ni

Taasisi yako ambayo inagusana na hilo. Ninakuomba sana Mhe. Waziri uliangalie kwa kina.

Halikuishia hapo Mheshimiwa kuna manesi wetu hawa, hawa bwana ni mtihani wa aina yake, *uniform* zao imekuwa balaa maana yake hakuna sasa hivi hata hiyo kupana *uniform* atoe mwenyewe, hakuna kiatu kwao hakuna chochote. Lakini hata maposho yao ya kisheria hayapo Mheshimiwa na kuna watu bado mpaka leo hawajapata hayo.

Ninakuomba sana Mhe. Waziri mwaka huu wa fedha hilo utakapokuja hapa unijibu limo au yamo. Kwa sababu hawa hatuwezi kufikia ufanisi wa kweli na uzalishaji wa kweli na kufikia maendeleo ya kweli katika taifa kama hatukuwaheshimu hawa ambao wanafanya kazi katika hizo taasisi za Serikali kutoa huduma kwa jamii na ndio maana hasa na malengo ya Serikali.

Iweje leo mfanyakazi ni mwalimu wa shule au pengine anafanya kazi katika taasisi fulani lakini *wallahi* ikifika saa nne anatoka anakwenda kwenye miradi yake, kwa nini. Hata hiyo mishahara haikidhi haja, imefika wakati Serikali mjitathmini, mjiulize na mfikie pahala mutoe mishahara inayoendana na haya maadiliko ya mifumko ya bei na maisha yanavyokwenda katika taifa letu.

Nayasema haya nikiwa na ushahidi kwamba kuna nyongeza 2011 ambayo aliifanya Rais akasema ametia kiwango cha kwanza ilikuwa ni laki moja akasema ametia hiyo robo 25.

Mheshimiwa nikuulizeni nyinyi mkitoka hapa 125,000/= mnatumia nini, hebu tuulize polo ya mchele, tuulize na huduma za kijamii twendeni hivyo dunia ndivyo inavyokwenda ili kustawisha taifa na wananchi kuishi katika shughuli za kimaendeleo na kuweza kufikia ufanisi na maendeleo ya kweli katika taifa ni kuboresha huduma za kijamii zikiwemo hizi za wafanyakazi kuwawezesha kumudu maisha yao.

Leo walimu, madaktari pamoja na taasisi nyengine wanafanya kazi mbili mbili lazima afanye biashara, lazima akafanye na kazi nyengine, saa 4 ukenda hayupo ufanisi wa kazi uko wapi, uzalishaji uko wapi, huduma za kijamii zinapatikana wapi. Unakwenda nesi hayupo, daktari katoka, mwalimu naye huduma inaondoka, ndio kwa sababu mishahara haikidhi haja. Nasema tena mabadiliko ni suali la msingi la kuangalia na kutathmini na kuona hasa hii mishahara tunayoifanya kweli inakidhi haja kulingana na maisha tuliyonayo wakati huu, huo ndio msingi.

Kama tutamudu haya nina uhakika hata uzalishaji, hata huduma za kijamii zitapatikana kwa ufanisi, haya ninayokwambieni kama mnaona mas-hara basi

sawa. Lakini ninakwambieni ni kweli kabisa tumepoteza muelekeo wa taasisi zetu kufanya kazi kwa ufanisi kwa sababu ya tatizo la maisha, badilisheni hayo muone. Tumieni hilo ongezeko la fedha kama kweli tumezidisha kupata pesa za kodi kwa kuangalia hawa wafanyakazi, ili tuzalishe kwa ufanisi zaidi na kazi zifanyike na huduma za kijamii zifikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo sasa niseme kwamba kuna lile posho maalum kwa taasisi mbali mbali ambazo Mhe. Waziri na wewe umezitaja hapa nataka kujua, umetaja posho maalum na mapitio tayari mmeshafanya Serikali imeshakubali.

Kwanza fedha hizo ni kiasi gani, lakini je, tumeona taasisi nyingi mnazipatia hizi fedha, hili posho maalum mmefanya mabadiliko mbali mbali mmesema. Nataka nielewe kuna taasisi bado zinalalamika kutokupata posho hili maalum, halafu unifahamishe ni lipi na ni kiasi gani posho hili maalum, wale ambao wafanyakazi wanaofanya Taasisi za viongozi wetu wakuu watatu bado wana malalamiko ya posho maalum, hususan Ofisi ya Makamu wa Kwanza tunaona kwamba hivi vitu havipo.

Hebu twambieni kwanza ni kiasi gani na ni zipi hizo posho maalum na ni nani wanaostahiki kuzipata hasa, maana hapa kwenye kitabu chako umechanganya mengi mengi. Mhe. Waziri naomba hilo nije nipate ufafanuzi.

La mwisho kabisa kuna moja nimelibakisha, Mheshimiwa kwenye Chuo cha Utumishi wa Umma ambako tunazalisha na kutotoa mambo maalum ambayo yanaleta ufanisi katika kazi kwenye Chuo cha Utumishi wa Umma, hebu niambie kwa sababu tunataka twende vizuri je, wana usafiri, tumewaona wengi wao wanakuwa ni wanawake na mara nyingi wanahangika kwenye madala dala na kazi zinakuwa ngumu kidogo. Kwa nini kusiwe na utaratibu na mpango maalum wa kuwepo basi la pamoja kwa sababu Chuo kiko nje ya mji likawa linawapeleka na kuwarejesha Mhe. Waziri, naomba sana kwamba chuo kile kwa kuwa ndio chemchem ya kuzalisha wafanyakazi watakaokuwa bora basi naomba hilo nalo uweze kulifikiria.

La mwisho kabisa Mheshimiwa katika ukurasa wa 57 ambapo umeonesha katika kiambatanisho chako hapa umesema kuna fedha za miradi miwili. Katika miradi hii umeweka tu kuna fedha milioni 100 na milioni 200 kwa mradi wa pili naomba Mheshimiwa uniambie fedha hizi ni za Serikali, fedha hizi ni za wahisani? Kwa sababu nimeona umeziweka kama *figure* tu lakini hazikuonesha fedha hizi zinatoka kwa wahisani ama fedha hizi zitatoka Serikalini. Naomba nipate ufafanuzi huo.

Baada ya kuyasema hayo Mhe. Mwenyekiti, ninaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia 80 na asilimia 20 nitazimalizia baada ya kupata ufafanuzi wa kina kwa Mhe. Waziri. Ahsante.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na tukawepo hapa kufanya majukumu yetu.

Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu mdogo na utakuwa mdogo sana, kwa sababu mambo mengi nilikuwa nataka kuyachangia wenzangu wameshayaeleza, lakini na mimi nitatilia mkazo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yake, lakini naomba pia nianze mchango wangu kwa kumpa pole Mhe. Waziri kwa namna wizara yake ilivyoshindwa kutimiza malengo yake na kwa kiasi kikubwa imewavunja moyo Wazanzibari na kuwakatisha tamaa hasa vijana wetu walioko vyuoni wanaosoma hawajui nini hatima yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa 6, *page* ya 18 Mhe. Waziri anajigamba ametekeleza vizuri ilani ya CCM, ikiwa ni hivyo lazima Mhe. Mwenyekiti tufanye tathmini na Mhe. Waziri awaeleze wananchi utekelezaji huo wa ilani ya CCM umeweza vipi kutoa majibu ya matatizo magumu ya sekta ya ajira katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri ajipime katika mambo haya mawili, kwanza upatikanaji wa nafasi za kazi. Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri hawezi kujisifu kwamba utekelezaji wa ilani yake ya CCM umefanikiwa katika eneo hili, kwa sababu kuna vijana wengi waliomaliza elimu ya Chuo Kikuu au vijana kwa maelfu waliomaliza elimu ya diploma na vyeti vya fani mbali mbali hawajapata ajira.

Mhe. Mwenyekiti, hata likitolewa tangazo la ajira ni nafasi moja ya kazi ambayo vijana kwa mamia huwa wanapeleka maombi kwa nafasi hiyo moja. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili ni jambo linalosikitisha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna baadhi ya nchi kazi zinatafuta watu wa kuwaajiri hapa Mhe. Waziri ana lipi la kujisifia kuna vijana wamemaliza masomo wamekata tamaa na kupata kazi wazee wao wamewalipia elimu lakini kazi hapana. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, haya ni mambo ya kusikitisha. Je, Mhe. Waziri atajitapa vipi kuwa amefanikiwa kuwapatia ajira wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika sekta ya utalii shughuli ya kuwapatia vibali wafanyakazi kupata ajira katika mahoteli ya utalii yako chini ya wizara yake. Hivi sasa Mhe.

Mwenyekiti kuna malalamiko kila uchao kwamba ajira mahotelini wanapewa wageni, huku vijana wetu Mhe. Mwenyekiti waliomaliza diploma ya Chuo cha Utalii wakiwa hawana kazi wamekuwa mzigo kwa jamii na waziri Mhe. Mwenyekiti analijua hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimuulize Mhe. Waziri Maalim Haroun ni vipi utekelezaji wa ilani ya CCM ulivyofanikiwa katika kuwafanya vijana wetu waliomaliza diploma ya Chuo cha Utalii wakiwa hawana kazi katika nchi yao ambayo ina mahoteli ya utalii yanayozidi 400.

Mhe. Mwenyekiti, kama kweli ilani ya CCM imefanikiwa kama alivyosema Mhe. Waziri kusingekuwa na vijana waliomaliza na wana vyeti vya masomo ya utalii wakikaa bure bila ya kupata kazi katika nchi yao ambayo kuna mahoteli mengi. Mhe. Mwenyekiti, namuomba nimuulize Mhe. Waziri je katika kufeli huku kwa ilani yake yeye ana mchango gani, na wananchi wamuhukumu vipi.

Mhe. Mwenyekiti, ingalikuwa waziri hakujigamba hapa mimi nisingetanabahi kuwa hapa tumefeli, lakini ile kujigamba kwake Mhe. Mwenyekiti ndipo kuliponiamsha kuwa hapa tumefeli.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine nina taarifa ya kuletewa na kijana mmoja aliyekuwa akifanya kazi katika Hoteli ya Chavda na amenilalamikia. Mhe. Mwenyekiti, kijana huyo ni mwenyeji wa Wilaya yangu ya Chake-Chake kwamba yeye na wenzake walifukuzwa kazi na mmiliki wa hoteli hiyo kinyume na utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kulalamika bwana huyo alitoa kauli kama waende popote yeye ni mwenyeji kuliko wao. Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa wa Kizanzibari walikwenda kushtaki na kuandika barua. Idara ya Kazi Mhe. Mwenyekiti, waliwapuuza bila ya kuwasaidia kumbe ni kweli Meneja wa Chavda maneno yake aliyasema kama yeye ni mwenyeji serikalini.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, ninaomba maelezo ya Mhe. Waziri kwa nini Idara ya Kazi haikuwatendea haki vijana wale. Na vile vile namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo yatakayoniridhisha hapa ikiwa sitoridhika nitazuia fungu la *programme 03* la uratibu wa uzalishaji na upatikanaji wa ajira za staha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu mdogo huo nasubiri majibu ya mwalimu wangu Maalim Haroun ili nipate kuunga mkono hotuba yake. (*Makofi*)

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipatia nafasi hii na mimi yakuweza kuchangia katika hotuba hii ya

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma katika kipindi hiki cha bajeti cha mwaka 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimuombe Mwenyezi Mungu anipe pumzi na aniwezeshe katika kuchangia bajeti hii, na vile vile namuomba Mwenyezi Mungu aniondoshee jazba ya kuweza kusema maneno machafu niweze kusema maneno mazuri ili Wazanzibari wanielewe. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu mkubwa leo itakuwa ni pongezi. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na vile vile nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia 95.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Nina sababu za kusema hivyo na kujigamba kwa sababu mwenye macho haambiwi tizama, sote ni mashuhuda maendeleo tunayaona kwa hiyo huyo mwenye kusema hayo Mhe. Mwenyekiti macho yake hayaoni. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tukisema serikali, serikali naamini kwamba ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa maana hiyo tukisema serikali imefeli basi wamefeli wote.

Mhe. Mwenyekiti, naanza na ukurasa wa 6, naomba ninukuu Mhe. Mwenyekiti.

"Katika hotuba ya ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi Novemba, 2010 kwa upande wa Sekta ya Kazi na Utumishi wa Umma, Mhe. Rais wa Zanzibar alitoa ahadi mbali mbali zikiwemo kuongeza nafasi za ajira na kuimarisha maslahi ya wafanyakazi ili kujenga utumishi uliotukuka".

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa maslahi ni mazuri kwa sababu nasema hivi ni mazuri kwa sababu gani? Kila mtu anakwenda kwa ubavu wake na maslahi yanakuwa mazuri kutokana na inategemea hali ya uchumi wa nchi, ikiwa uchumi wetu ni mzuri Mhe. Mwenyekiti wafanyakazi wetu tukiwemo na sisi tutalipwa maslahi mazuri. Lakini sasa kama uchumi wetu ni mdogo Mhe. Mwenyekiti hatuwezi tukamuiga Juma kwa kuwa analipa wafanyakazi wake juu na sisi tukasema hivyo, hapana Mhe. Mwenyekiti kwa sababu serikali ina mambo mengi yakufanya ukiangalia wafanyakazi na kuna mambo mengine kama afya ni muhimu kwa wananchi. Kwa hiyo, kwa jambo hili Mhe. Mwenyekiti mimi naipongeza sana na nampongeza Dkt. Ali Mohammed Shein na vile vile nimuombe Mhe. Waziri anieleze katika kipindi hiki cha uongozi wa utukufu wa Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kiasi gani kwa upande wa ajira tumeweza kuvuta hatua ukilinganisha na miaka ya nyuma iliyopita. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri akija anieleze sasa

hivi tuko wapi na tumetoka wapi mambo kidogo kidogo Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naenda ukurasa wa 8 kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti naomba kidogo ninukuu.

"Katika juhudi za kuimarisha uhusiano mwema kazini, ofisi imeanzisha Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Mambo ya Kazi ili kuharakisha maamuzi ya migogoro ya Kazi".

Mhe. Mwenyekiti, hili kwanza niseme nampongeza Mhe. Waziri na vile vile nichukue nafasi hii kutoa wito katika maofisi yote kuunda kitu kama hiki ili kuondosha migogoro katika sehemu zetu za kazi.

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba katika sehemu zetu za kazi kila mtu na hulka yake na tabia zake, kunatokea mambo mengi ya sisi wenyewe wafanyakazi kwa wafanyakazi kwa maana hiyo kama kutakuwa na chombo kama hiki, tutaweza wenyewe kusuluhishana na kufikia mahali pazuri tukaweza kufanya kazi zetu na kupeleka mbele Taifa letu kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi leo ni pongezi tu kwa sababu mambo ni mazuri. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda tena ukurasa wa 9 kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu za Taifa, ofisi imeweka mtambo wa *CCTV* katika jengo la Nyaraka na kuanza utekelezaji wa mradi.

Mhe. Mwenyekiti, hili pia ni jambo zuri la kujisifia, basi vile vile nichukue nafasi hii kuiomba serikali uchumi utakaporuhusu na pesa tutakapokuwa nazo basi ifanye hivyo kwa mawizara yote ili kulinda huu uharibifu na uibaji wa nyaraka zetu. Kwa sababu kama leo imetokea wizara hii kesho kutwa itatokea wizara nyengine, kwa hiyo niiombe serikali naamini kwamba serikali yetu ni sikivu na ina nia njema kwa watu wake isipokuwa ni hali yetu ya uchumi tu Mhe. Mwenyekiti hakuna mtu asiyetaka kwamba watu wake wale vizuri au waishi vizuri. Lakini ukiangalia mfuko kama hauruhusu huwezi kwenda kuiba Mhe. Mwenyekiti, wewe mwenyewe Mhe. Mwenyekiti unapokuwa na pesa nyumbani kwako siku hiyo unaamka si unakula vizuri.

Kwa hiyo, naamini serikali yetu Mwenyezi Mungu atujalie hii amani yetu na utulivu tuizidishe ili tuzidi kuzalisha mambo yetu mazuri mazuri ili nchi yetu nayo iweze kufanya mambo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi mchango wangu utakuwa si mkubwa, mchango wangu ni mdogo na ni mchango wa kupongeza tu serikali pamoja na Mhe. Waziri naamini kwamba hujafeli unakwenda vizuri. Kwa hiyo, nikuombe tu ukaze buti Mhe. Waziri ili tusonge mbele ili kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa tu mwisho Mhe. Waziri nimalizie kwa kuuliza hili swali. Mhe. Waziri hebu unieleze hii hatma ya walimu hawa wanaodai hizi pesa zao Mhe. Waziri naona imekuwa kelele nyingi, tafrani nyingi hebu liweke sawa Mhe. Waziri utakapokuja hapo tufahamu, ili hili bughuza liondoke. Naamini kwamba Mhe. Waziri kwamba hili jambo limefanyiwa kazi kwa kiasi, lakini unajua tena akiwa mmoja hajakamilishiwa inakuwa tatizo, hebu ukija liweke *open* Mhe. Waziri watu wote walielewe, jambo dogo lisichukuliwe kuwa kubwa Mhe. Waziri. Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamkaribisha Mhe. Panya naomba haya makofi tuyapige kwa nidhamu, kwa sababu wale wenzetu ndani wameweka vidude katika masikio yao, sasa mkipiga makofi kwa hivyo mnawaumiza masikio yao. Naomba twende kwa utaratibu maalum.

**Mhe. Panya Ali Abdallah:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii nikasema machache katika wizara yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana mahala hapa. Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi kubwa na inayofanywa kwa umakini kabisa ili kuweza kutupatia huduma mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu katika hii Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu.

"Idara ilipanga kuwajengea uwezo watumishi 35 ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, kuimarisha na kuweka mazingira mazuri ya kazi yatakayorahisisha utekelezaji wa kazi za wizara kwa wakati; kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na manunuzi wa wizara; kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli za wizara, ili kuelimisha na kujenga taswira nzuri kwa umma na kuhakikisha haki na maslahi ya watumishi yanapatikana kwa wakati".

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze wizara kwa kuliona hili, lakini mimi nilitaka nitoe ushauri kwa kumwambia Mhe. Waziri ili kuhakikisha haya kama haki na

maslahi ya wafanyakazi yanapatikana basi ni kufanya ziara za mara kwa mara katika taasisi zetu hizi ili kuhakikisha kero na changamoto ambazo wanazipata wafanyakazi wetu. Ni kweli changamoto zipo lakini wanashindwa hawajui wazipeleke wapi, lakini Mheshimiwa utakapofanya ziara basi ukikaa na wafanyakazi utaweza kuzipata changamoto hizi.

Mhe. Mwenyekiti, niende pia katika Idara hii ya Miundo ya Utumishi. Mhe. Mwenyekiti, idara hii pia imejipanga kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji kwa wizara na taasisi zote za umma ambazo zoezi hili halijakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi pia niwashukuru na niwapongeze kwa hiyo kazi ambayo wanataka kuifanya, lakini pia niombe ni sababu zipi ambazo za msingi zinazofanya wengine waweze kufikia katika hii miundo kwa urahisi na wengine waweze kuchelewa, ni sababu gani ambazo zimecheleweshа. Pia labda niombe ni kwa nini kusitolewe muda maalum ambao ukatakiwa taasisi hizi zote ziwe tayari zimeshakamilisha utaratibu huu ili kama ni kufaidika basi waweze kufaidika watu wote kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Chuo cha Utawala wa Umma. Pia nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wana chuo hiki kwa kazi nzuri yakuibua mafunzo mbali mbali ambayo yanawasaidia wafanyakazi wetu kuongeza ujuzi wao hali ambayo pia itaongeza maslahi ya wafanyakazi. Lakini niiombe serikali kuendeleza ujenzi wa chuo kwa sababu inaonekana kuna wimbi kubwa la wasomaji ambao wanajiandaa katika kuingia katika vyuo hivi kwa ajili ya kujiendeleza. Sasa nafasi inawezekana ikawa ndogo kwa wao kuweza kushiriki katika masomo yale.

Kwa hiyo, niiombe wizara iendeleze ule ujenzi ichukue hatua ya kuiendeleza ule ujenzi, ili waweze wanafunzi kila wanapohitaji kuingia basi waweze kufanikiwa kujiendeleza.

Pia nilitaka kuulizia hapa kulikuwa na mpango wa kuanzisha chuo kile cha udereva ambacho hapa ilikuwa kwetu hakuna na watu walikuwa wanakwenda kusoma Bara. Ni hatua zipi ambazo zimefikiwa katika kulianzisha hili ili na madereva na wao waweze kujiendeleza katika ujuzi wao.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara hii ya Ajira. Mhe. Mwenyekiti, pia idara hii niiombe serikali iangalie sana hasa katika sekta binafsi. Sekta binafsi wafanyakazi wanafanyishwa kazi kinyume na taratibu zote za kisheria. Kwa hiyo, Mhe. Waziri kama wanavyojipanga basi wajipange katika kutembelea hizi sekta binafsi kuhakikisha wafanyakazi wetu wanapatiwa yale mahitaji yote ambayo wanapaswa kuyapata kama wafanyakazi, hasa ikiwemo kuangaliwa kiafya kwa sababu sekta

hizi binafsi watu wanapopata tatizo la kiafya basi huwa haziwajali. Hilo niombe kuwa waangalie sana juu ya hilo.

Halafu pia katika Chuo chetu cha Amali. Chuo hiki kilipoanza wale wanafunzi wa mwanzo ambao walitoka katika chuo basi serikali iliahidi kuwapatia mikopo, ili waweze kuendeleza fani zao ili iwe ni sehemu ya kujiajiri na kujipunguzia umasikini. Nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze vijana hawa lini wataweza kupatiwa mikopo hii, ili waweze kujikimu na kuendesha maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu hautakuwa mkubwa lakini napenda nichukue fursa hii kuipongeza sana serikali kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa ilani. Serikali imejitahidi katika kutekeleza ilani ambayo imetokana na Chama cha Mapinduzi, lakini tu nichukue fursa hii kusema shida kwa mwanadamu hazishi.

Sifa ya mwanadamu ni mapungufu, ili uweze kuwa kamili itakuwa hiyo sifa sio yako wewe tena, shida kwa mwanadamu zitaendelea kuwepo kuanzia alipozaliwa mpaka atafika kutiwa kaburini. Kwa maana hiyo, serikali inapojitahidi tushukuru kwa pale ilipofanya, sisi wenyewe tu binafsi serikali ni chombo kikubwa ambacho kinaangalia watu wote, lakini sisi tuangalie katika familia zetu tu. Je, mahitaji tunayoyataka yote tunayatimiza kwa wakati mmoja? (*Makofi)*

Kwa hivyo, tusichukue fursa tu ya kuilaumu serikali ambapo wakati mwegine imeweza kwa asilimia kubwa kupeleka huduma kwa wananchi. Tunazo barabara na zinatumika kwa watu wote zipo zimetekelezwa, tunayo maji safi na salama na tunakunywa sote, kuna umeme vijijini umepelekwa tunatumia huduma hizo kwa sote, serikali inajitahidi kwa kiasi chake lakini na mzigo nao unakuwa mkubwa na kuangalia hali ya uchumi wa nchi yetu. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwisho katika kipindi hiki cha asubuhi ya leo. Mimi nataka nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma namna anavyojitahidi katika kusimamia kazi na utekelezaji bora.

Mhe. Mwenyekiti, michango yangu mimi baada ya kutoa shukurani hizo ni midogo sana, nina michango kama miwili mitatu tu, ambayo miwili nitaelekeza kwa Mhe. Waziri husika lakini mmoja nitauelekeza kwa Mjumbe mwenzangu ambaye hivi sasa ametoka humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Waziri kwamba tunajitahidi kuajiri na serikali inajitahidi kutengeneza mafao kadiri inavyoweza. Lakini bado ningemuomba Mhe. Waziri ajaribu kuangalia, tulijaribu kuongeza mishahara katika kada ya wasomi lakini serikali nayo ikakaa na kutafakari kuongeza mafao mazuri kwa wazoefu wa muda mrefu. Lakini kuna kada ya watu wa kawaida hizi *gape* namna zilivyopitana tunahisi kwamba kuna *gape* kubwa baina ya wasomi, wazoefu na kada ya watu wa kawaida na ndio maana Wajumbe wengi wanajaribu kupiga kelele huu mshahara wa chini kwamba ukiuangalia mshahara wa chini na mahitaji ya wananchi ya kila siku bado kuna tofauti kubwa.

Sasa niiombe serikali, kila hali ya nchi ya kifedha itaporuhusu basi kuangalia wananchi wetu ili kuwaongezea mishahara siku hadi siku kadiri ambavyo serikali uwezo itakuwanao, kwa sababu pasipo na uwezo nafikiri hatuwezi kufanya lolote. Lakini nina imani kwa sababu matumaini tunakuwa tunayapata kupitia Wizara ya Fedha kwamba ongezeko la ukusanyaji wa mapato linaongezeka basi namna yanavyoongezeka mapato basi nafikiri kuna haja na kuangalia maslahi ya wafanyakazi wetu. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilitaka nimtahadharishe Mhe. Waziri alisaidie na kulifanyia kazi kwa makini kabisa. Kwamba mara nyingi tunapokuja katika vikao vyetu na serikali inapotoa taarifa huwa inatoa taarifa namna ya mzigo mkubwa tuliokuwa nao wa vijana na ambapo vijana wengi wamesha-*graduate* lakini uwezo wa serikali wa kuajiri umekuwa mdogo.

Sasa athari zake ni kwamba kila mwaka vijana wana-*graduate* ina maana wanapo-*graduate* kila mwaka inabidi idadi ya wasomi inakuwa kubwa lakini idadi ya kazi inazidi kupungua. Tahadhari yangu natoa kwa Mhe. Waziri kutafuta namna mbadala ya kuanza kuweka mikakati katika suala zima la ajira katika sekta binafsi.

Ni vyema serikali ikatafakari kuchukua maamuzi magumu katika suala hili, kwa sababu tukiangalia kama tunategemea sekta binafsi tu za matajiri au wawekezaji hii ina hatari yake. Kwa sababu mwekezaji ndio mwekezaji kaja kuwekeza fahuwa-lmuradi, hakuja kuwekeza vijana wetu watakuwa bado wanaendelea kuteseka kwa kutokupata ajira katika nchi yao.

Sasa lengo na madhumuni ya kuzungumza hapa ni kuiomba serikali kuchukua maamuzi magumu ya kutafuta njia mbadala katika suala zima la kuanzisha viwanda vidogo vidogo katika nchi yetu. Najua tukiamua tunaweza, tulichukua maamuzi magumu sana hapa ya kuhakikisha kwamba tunanunua meli ya serikali, ili kuwaondoshea matatizo wananchi wetu. Hili limewezekana katika kipindi kifupi tangu kutoa tamko na mpaka serikali ilivyoamua kutekeleza suala lile.

Sasa ni vyema basi serikali ikaangalia kutafuta namna mbadala kama tulivyoweza kuinunua meli ya serikali basi tukanunua meli za uvuvi, ili tukaanzisha sekta nyengine ya uvuvi na vijana wetu wakapata kuajiriwa katika sekta hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, hio ni sehemu moja tu unajua kuna sehemu nyingi tumekuwa tuna wazalishaji wakubwa. Sote tumekuwa ni mashuhuda kipindi kifupi tu watu wameanza kujiimarisha kutumia kilimo cha *green house; watermelon* zimekuwa zinavunwa kwa wingi. Sasa kama tutaamua kuanzisha viwanda vya kwenda kusindika matunda basi nafikiri tunaweza tukapiga hatua na kuwasaidia vijana wetu katika maeneo mbali mbali ya ajira.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia ni suala zima la ajira kwa walemavu. Mimi nahisi kuna haja sasa hivi kwa serikali na Mhe. Waziri atapokuja basi anisaidie kwamba serikali kupitia wizara yake imeandaa mikakati gani ya kuhakikiha kwamba walemavu wana *privilege* maalum katika suala la ajira.

Mhe. Mwenyekiti, ulemavu kuna wa aina nyingi na tuna vijana wengi ambao sasa hivi wanajitahidi kusoma na kwamba ni walemavu. Sasa mimi nafikiri kuna haja katika kila maeneo ambayo serikali itatangaza ajira kama kuna mlemavu basi kuna haja ya kupewa kipaumbele. Lakini tatizo labda linabakia hapa, tunaweza tukatangaza ajira lakini ushirikiano ndio jambo la msingi, nafikiri kuna haja ya serikali, wizara inayoghulika na masuala ya ajira kushirikiana na Idara ya Walemavu kupitia Mkurugenzi wake ili kumuulizia au kuweka *list* maalum ya wasomi ambao ni wizara inapotoa taarifa za ajira tuone kwamba katika kada hii tunao walevu ambao wana uwezo katika fani hii ili kuwapunguzia mzigo.

Mhe. Mwenyekiti, hili nimeliona kupitia Bodi ya Mikopo. Bodi ya Mikopo imekuwa na ushirikiano mkubwa sana na Idara ya Walemavu, ili kutoa nguvu kuwasaidia walemavu basi *list* yao wanakuwa wanapewa kutoka Idara ya Ulemavu. Bodi ya Mikopo wanapotoa mikopo yao wanajua ambao wana *list* ya watu ambao wanahitaji mahitaji maalum na wanawapa kipaumbele katika suala zima la kule kuajiri.

Kwa sababu tusipompa kipaumbele mtu ambaye ana ulemavu yeye kutafuta riziki katika maeneo mengine inakuwa ni ngumu kwa sababu yeye ana mapungufu, mtu ambaye ana ukamilifu wa viungo vyake anaweza kujiajiri katika maeneo mengine ya hali ile ama kubeba, lakini wenzetu hawa wanahitaji fursa ya pekee ya kusaidiwa ili kupata wepesi katika shughuli zao za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, la kumalizia tangu tumeanza vikao hivi nashukuru kwamba tulikuwa tunakwenda katika mazingira mazuri ya kuchangia kinachohitajika na tukichangia wizara husika katika kuelekeza, kuisimamia na kuishauri.

Leo yameanza kujitokeza mambo hapa, Mhe. Mwenyekiti, sio kama tunafunga midomo au sio kama hatuwezi kusema lakini tunahisi muda huu siwo. Huu ni muda wa kutekeleza yale ambayo yametuleta hapa kuja kuwasimamia wananchi wetu, kuja kuishauri serikali na kuielekeza ili kuondosha kasoro zilizokuwepo ili wananchi wetu wapate kufarijika.

Mhe. Mwenyekiti, unapoanza kuchangia hotuba ya waziri ukasema kwamba mifumo ambayo inapeleka nyuma suala la ajira ni mfumo mbovu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Mhe. Mwenyekiti, huyo mtu ana mapungufu katika akili zake. Kwa nini niseme hivyo? (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambacho ndio chama kinachoendesha serikali hii kimefanya mambo mengi na mambo ambayo tunatumia sisi kama watu wa Chama cha Mapinduzi na wenzetu wa upande wa upinzani pia mambo hayo wanayatumia. Sitegemei kama kuna mtu anatembea angani, hatembei katika barabara ambazo Chama cha Mapinduzi kimetengeneza barabara zile.

Sitegemei kabisa kama kuna watu hivi sasa wanakunywa maji ya chumvi wanaacha kunywa maji ambayo yameletwa na Chama cha Mapinduzi. Sitegemei kama kuna watu hawahitaji huduma mbali mbali za nchi hii. Chama cha Mapinduzi kina ilani nzuri ilani ambayo inatekelezeka, ilani ambayo wanatumia wananchi wetu wa nchi hii Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la ajira ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezeka kwa uadilifu na kwa imani kabisa kwa pande zote za wananchi wa nchi hii. Kwa nini niseme hivyo? Kuna ajira huwa zinatangaziwa moja kwa moja kwamba anayestahiki ajira hii basi aombe nafasi hii, lakini kuna ajira zinakwenda *specific* katika maeneo. Kuna ajira hutangaziwa kwa upande wa Pemba na kuna ajira hutangaziwa kwa upande wa Unguja, lakini chama hiki hiki ambacho kinaambiwa kwamba ilani yake ina upendeleo mimi nafikiri hawa watu hawajalipima hili. (*Makofi)*

Namuomba Mhe. Waziri katika suala zima la utumishi anapotangaza ajira kwa upande wa Pemba na kwa upande wa Unguja awe makini, kwa sababu sisi kama wana CCM tumeanza kuwa na masikitiko katika hili. Kwa nini nasema hivyo? Zinapotangaziwa ajira Pemba wanaoajiriwa wanakuwa ni watu wa Pemba peke yao, lakini tunapotangaza ajira kwa upande wa Unguja bado kuna matatizo;

Muunguja anaingia na Mpemba anaingia. Sasa hili linapelekea kwamba Pemba yao Unguja yetu sote.

Sasa hili namuomba Mhe. Waziri tuwe makini kwa sababu tunatangaza ajira kwa kuangalia maeneo, baadhi ya ajira kwamba hizi tunawapa wenzetu kama Pemba, basi hatuna matatizo kama Pemba wazitumie kwa upande wao. Lakini kwa zile ambazo tunazitangaza hizi kama za watu wa Unguja basi na sisi watuachilie watu wa Unguja tutumie nafasi yetu Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba Chama cha Mapinduzi hakina matatizo na wananchi wake wala hakina ubaguzi na kama wanataka kufanya utafiti basi waanze kulifanyia utafiti Baraza la Wawakilishi. Katika kipindi cha miaka miwili idadi ya Wapemba na Waunguja wepi walioajiriwa na ndio maana tukasema sisi hatuna ubaguzi katika suala la ajira.

Hatuna ubaguzi kumuangalia huyu katoka wapi, wala huyu ana sifa gani, tunachoangalia ni sifa ya kazi katika maeneo ambayo yanahitajika. Serikali hii haimbagui mtu wala haina kisasi na mtu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana. (*Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe katika meza yangu sina mtu mwengine ambaye ameomba, lakini naona watu wawili ambao wanataka kuongezea. Kwa hiyo, naona mkono wa Mhe. Hija Hassan Hija na mkono wa Mhe. Fatma Mbarouk Said pale, lakini pia naona mkono wa Mhe. Abdi Mosi Kombo basi mtaendelea kuleta majina baadae.

Kabla ya kusitisha shughuli zetu nina tangazo, Mwenyekiti wa Uwawaza anawatangazia Wajumbe wa Kamati Tendaji ya Uwawaza wakutane kesho saa saba baada ya kikao, sio leo ni kesho baada ya kikao.

Kwa hiyo, baada ya matangazo hayo sasa tunasitisha shughuli zetu hizi hadi saa kumi na moja za jioni kwa kuendelea na michango katika wizara hii. Ahsanteni.

*(Saa 6:56 Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Abdi Mosi Kombo:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kutufikisha tena hapa jioni ya leo na nakupongeza Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya mwanzo katika jioni hii na mimi kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaelea kidogo tu katika ukurasa wa 25, Ibara ya 62 kuhusu Idara ya Ajira. Mhe. Mwenyekiti, naomba kununukuu;

"Idara ya Ajira ilipanga kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa upelekaji wa taarifa ya Soko la Ajira kuimarisha shughuli za ukuzaji wa ajira nchini na kuimairisha mashirikiano baina ya serikali na sekta binafsi".

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi naipongeza serikali yetu ya Zanzibar inayoendeshwa na Umoja wa Kitaifa kuweza kuiweka Wizara ya Kazi kwa sababu Wizara ya Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma ni Uti wa mgongo wa wananchi, Wizara ya Kazi ndio itakayokusanya mambo ya kazi kwa wananchi wote wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mataifa yote ya duniani na wananchi wake wanategemea sana ajira, aidha ikawa ajira za serikali au ikiwa ajira za binafsi. Mhe. Mwenyekiti, na mimi naipongeza serikali yetu tena kwamba inajitahidi sana kufungua milango ya ajira kwa vijana pamoja na wananchi kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kila tunapozidi huwa maendeleo na watu huwa wanazidi, takwimu za binaadamu zinazidi na matatizo yanazidi, hasa sasa hivi vijana wetu wengi wanasoma wanamaliza mashule wengine wanafika kidato cha tatu, cha nne, cha sita na wengine mpaka Vyuo Vikuu. Lakini sasa tatizo kubwa tulilokuwa nalo vijana wetu bado hawajafundishwa fani. Fani mwanafunzi ikiwa nayo ikiwa amesomea fani fulani kwa mfano mwanafunzi amesomea fani za umeme sasa akitoka Chuoni tu anajua nikamate nyanja ya umeme, kwa sababu serikali inaweza ikachukuwa vijana wengi mpaka ikabidi nafasi zimekwisha, lakini kijana ikiwa ametoka na fani yake katika Chuo basi anafungua fani tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba serikali iweke fani katika maskuli. Wenzetu wanaweka mpaka fani za kujifundisha magari, kuunda magari. Kwa

hivyo, ili kupunguza wimbi la ajira serikali naiomba kupitia Wizara yake ya Kazi iwe na mfumo huo.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda hapa hapa katika ajira katika dunia nchi zote wanakimbilia kuwaajiri vijana wao wazalia au wenyeji. Namuomba Mhe. Waziri wa Kazi ahakikishe kwamba vijana wetu bado wanapata ajira ndani ya sekta hizi tulizoziweka, kwa mfano kuna mahoteli na leo tuna mahoteli mengi tunayo *Alhamdulillah*. Lakini kuna lalamiko vijana wetu wanaweza kwenda kule kwenye mahoteli wakapatishwa tabu, hawapati zile ajira na sisi tumeweka mahoteli haya yatusaidie.

Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Kazi ihahakishe kwamba vijana wetu wanapata ajira ndani ya mahoteli, ndani ya sekta nyenginezo ambazo zitaweza kuwasukuma na kuwapunguza tatizo vijana ambao tuliokuwa tunasomesha kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, katika nchi yetu kuna akina mama wengine wana matatizo, wengine wajane hawana waume. Kwa hivyo, hawa wote wanahitaji wawezeshwe waangaliwe na naiomba wizara hasa ifanye sensa ya kuwatambua hasa wale ambao wana matatizo ya ajira ili wawafungulie nyanja za ajira, wawakusanye na wawawezeshe kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda katika ukurasa wa 27, Idara ya Usalama na Afya Kazini. Mhe. Mwenyekiti, kuna sehemu nyengine ndani ya nchi yetu hii hawana usalama wa afya kazini, utawakuta kuna watu wanafanyakazi ya mitaro hata *gloves* hawana, wanafukua mitaro. Kwa hivyo, usalama wa afya kazini pale utakuwa hapana.

Kwa hivyo, naiomba wizara ihakikishe kwamba sehemu kama zile zinazochimbwa mitaro ile inayopita maji machafu kwa wale wafanyakazi ambao hawana hata zile *glaves* zile, kwa hivyo, pale itakuwa hapana usalama wa afya.

Mhe. Mwenyekiti, ningeliomba vile vile wizara ihakikishe kwamba ndani ya Maofisi mule ijapokuwa wiki kwa siku mbili au siku moja basi wafanyakazi wanapimwa afya kazini, wanachekiwa afya zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama nilivyosema kwamba sina mchango mkubwa, naiomba serikali ihakikishe wafanyakazi nao vile vile wanaajiriwa wanapata maslahi mazuri ndani ya kazi.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kuna baadhi ya sehemu nyengine au majimbo yetu

mengine vijana wengi wanakosa ajira hasa majimbo yetu kama kule Matemwe vijana wengi wanakuwa hawana ajira.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atuelekeze au atufahamishe vijana wetu tuwafanyie utaratibu gani katika wizara yake angalau na wao kidogo watu wa Matemwe wajikwamue katika ajira hizi hasa za serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napongeza wizara tena nashukuru Wizara ya Kazi angalau kutuletea Idara hii ya Ajira na tunawahakikishia wananchi wetu kwamba kuna Idara ya Ajira tunayoizungumza, kwa hivyo, Idara ya Ajira ihakikishe inawaajiri watu hasa majimbo yetu kule Matemwe kule nao vile vile wanamatatizo makubwa ya ajira.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi nikachangia machahe katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Awali ya yote kwanza nimshukuru mwenyewe Mhe. Waziri, kwa kuwasilisha hotuba yake hii nzuri na vile vile niwashukuru watendaji wake kwa pamoja na wakaweza kutuletea kitabu hiki cha bajeti ambacho kwa upande wangu kwa niaba ya wananchi wa Amani nakiunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa wa 7 nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kutuonesha namna gani anawajali wafanyakazi na hii ni pale ambapo baada ya kila kipindi kulikuwa na ongezeko la mishahara. Ni kweli kama walivyosema wenzangu mishahara hiyo bado haikidhi lakini haba na haba hujaza kibaba.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuona kwamba kila mara kulikuwa kunaongezwa hata maposho kwa sekta mbali mbali na wafanyakazi mbali mbali ambayo kulifanywa marekebisho hayo ya maposho kwa kutokana na sifa za kila mtu ambaye anastahiki kuanzia madereva, makatibu muhtasi na Mahakimu. Kwa kweli hili ni jambo la msingi kabisa kwa sababu unajenga hamu ya yule mfanyakazi kufanyakazi kwa ufanisi zaidi. Kwa hivyo, nimshukuru Mhe. Waziri, kwenye kitabu chake hichi cha bajeti kimeelezea mambo mengi.

Mhe. Mwenyemkiti, nikienda ukurasa wa 8 kifungu cha 25, nimeona Mhe. Waziri katika kuimarisha uhisiano mwema kazini Afisi imenzisha kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro, hilo ni jambo muhimu penye mkusanyiko wa watu changamoto hazikosi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, nikupongeze kwa

juhudi zako hizo pamoja na vitengo vyako mbali mbali ambavyo yote haya ni mambo ya kawaida panapokuwa na watu lazima matatizo hayakosi na lazima kuwe na vyombo ambavyo vitasimamia mambo mbali mbali katika wizara hii.

Mhe. Waziri pia, nikupongeze kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama na uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa kuweka *CCTV* katika jengo la Nyaraka. Mhe. Waziri, kwa kweli tunasikitika sana kwa nyaraka zile ambazo zimeibiwa na zikanufaisha wachache. Kuna watu walifanya suala hilo kwa kutokujijua wao ni nani, lakini vile vile kuna watu kwa makusudi wale wale wapinga maendeleo ambao tunajua vizuri sana wamezichukuwa nyaraka hizi kwa lengo lile lile la kuidhoofisha serikali yetu na ndio wale wale wanaokaa wakasema kichaka gani, kichaka mavi, kichaka mkojo, lakini matokeo yake wanazichukuwa nyaraka hizi na kuziiba kwa mitazamo yao kwa kudhoofisha serikili yetu.

Lakini Mhe. Waziri, nimeona bajeti kufikia hadi Machi mwaka 2015 kwamba fedha zilizotarajiwa ni bilioni nne milioni mia nane na tisini na nane mia tatu na arubaini na tisa ndizo zilizotumika kwa utekelezaji wa shughuli za kawaida ambapo bilioni mbili milioni mia mbili na hamsini na sita mia mbili na hamsini na moja mia nane na sitini na nne ni malipo ya mishahara ambayo yamefanya kuwa asilimia 77 na bilioni mbili mbili mia nne na tahamanini na sita ni kuwa ni matumizi mengineyo yamefanywa makadirio asilimia sitini na tano mpaka kufikia Machi.

Mimi niombe serikali kwamba ile bajeti inapoombwa basi ni vizuri ikawatimizia kwa sababu kunakuwa na malengo ambayo wizara imejiwekea lakini kutokana na upungufu wa pesa kwa kweli fedha ile inakuwa haitoshi na yale malengo yaliokusudiwa yanakuwa hayafikiwi. Kwa hivyo, ni vizuri sana kunakuwa na makisio ambayo wao wenyewe wizara yanakisia, lakini kwa bahati kuna *ceiling* ambayo imewekwa lakini basi hata hizi ili ile athari ya kibajeti isitokee basi ni lazima fedha zile wawe wanapewa kwa ukamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye malengo makuu ya Afisi niipongeze sana wizara pamoja na mshikamano wao waliokuwa nao wa pamoja kwani "Umoja ni Nguvu na Utengano ni Udhaifu" na kila mmoja akijua wajibu wake ni nini, basi lazima kunakuwa na mafanikio. Kwa hivyo, niwapongeze kwa kuongeza upatikanaji wa fursa za ajira za heshima kwa wananchi hususan vijana na vijana ndio nguvu kazi.

Kwa hivyo, naishukuru sana wizara hii kwa fursa hii ambayo wameitoa, pia, kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi, usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kazi, kama nilivyosema kwenye watu migogoro inatokeza chungua nzima. Kwa hivyo, ni lazima kuwe na mkakati wa kuondosha hiyo migogoro.

Vile vile, kwa sababu inasimamia mipango endelevu ya upatikanaji wa rasilimali watu wenye sifa. Kwa hivyo, hili pia waziri kupitia wizara yake wamelisimamia na mambo mbali mbali ambayo tumeona katika kitabu hiki. Mimi niwaambie ni wafanyakazi wa wizara wazidi kushikamana na kumsaidia Waziri wao ambaye ni mtu hodari na shupavu na yeye ni mwalimu. Kwa kweli mwalimu ni mtu mwenye sifa sana, bila ya mwalimu basi sote hapa tusingekuwepo leo.

Serikali imejitahidi, sote tunafikiria wengi tumesomeshwa na Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tumo humu kwa vifua vipana, tunazungumza mengi na mengine ni mazuri ya kuzungumza, lakini mengine pia kwa vile ni demokrasia tunasema maneno mengi. Lakini tusimalize maneno midomoni, pale linapokuwa linafanyika zuri basi tusifie na pale linapofanyika baya vile vile ni kazi yetu sisi Wawakilishi kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi ambao wametuchagua. (*Makofi*)

Kwa hivyo, hili ni jambo zuri ambalo Serikali inasimamia kupitia wizara hii na "penye nia pana njia". Ninajua kwamba Serikali ina mambo mengi, si Idara moja karibuni tuna Wizara kumi na sita na zote zinahitaji matumizi na kuna sehemu nyengine ni sehemu nyeti zaidi; kuna mambo ya afya, maji, lakini na Wizara hii nayo imo katika Wizara hizo kumi na sita na ina Kamisheni zake za Kazi na mambo mengine. Kwa hivyo, yote haya kwa msimamo wao na Waziri huyu kwa kweli ninaipongeza sana Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikenda mbele zaidi huku kuna Idara hii ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi. Nimefanya mapitio ya posho mbali mbali zinazotumika sasa kulingana na gharama za maisha. Posho hizo zinajumuisha posho la safari ndani na nje ya nchi, posho la mazingira maalum, posho la Maafisa Sheria, Makatibu wa Mawaziri na watumishi wa SMZ waliohamishiwa Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, kwa kweli jitihada ni kubwa ya kuwajali wenzetu hawa. Mimi niseme kwamba Serikali ni watu na kwa ajili ya watu. Kwa hivyo, sote tushikamane na sote tuna nia ya kujenga nyumba moja. Hivyo, ni lazima tushikamane pale penye msaada tusaidiane.

Sisi Wawakilishi wa wananchi, tuna mambo mengi ambayo tunatakiwa na sisi kama Wawakilishi tusaidie majimboni kwetu. Mimi niseme na hata mule majumbani mwetu, basi mtu anashindwa saa nyengine kukamilisha yote, lakini tunajua kwamba Serikali inajitahidi na kwa jitihada zake hizo Mwenyezi Mungu ataivusha nchi hii kwa salama na amani na hasa tukijua kwamba tunakwenda kwamba tunakwenda kwenye uchaguzi; Mwenyezi Mungu

*Inshaallah* atasimama na Serikali na hii ili tuweze kupata tena ushindi wa kishindo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe wasia tu baada ya kupita bajeti hii, nimeona mapungufu mbali mbali ambayo yanajitokeza hasa kutokuzifuata Sheria za Fedha, Sheria za Manunuzi na tunataka kuwe na usimamizi mzuri wa fedha, *internal control* lazima iwepo ili kile kidogo kinachopatikana basi kuwe na *value for money*, pia na kuona kwamba mazingira ya fedha yenyewe inavyotumika.

Mwenzangu juzi alitafsiri mazingira Mhe. Mosi Abdi Kombo, alikwenda mbali kuhusu mazingira akafungua mpaka lishe, akasema hiyo yote ni mazingira. Kwa hivyo, fedha hii tunayoipata basi tuitumie kwa vizuri kufuata Sheria za Manunuzi na kile kidogo kinachopatikana basi kitumike kwa ufanisi na kwa uwazi ili tuweze kufanikiwa hasa tukitambua kwamba safari hii tumekwenda na mfumo wa ku-*reform* hii bajeti. Hivyo, ni lazima kama tumekwenda huko basi ni lazima baada ya mwaka huu tuone kwamba ni namna gani *reform* hii imefanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache kama nilikwisha kusema kwa niaba ya wananchi wangu walio wengi walionichagua na hata wale waliokuwa hawakunichagua ambao wapo katika Jimbo la Amani na nina imani kwamba mwaka wa uchaguzi watanirejesha tena.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe. Sasa nimalizie kwa Mhe. Hija Hassan Hija na baadae Mhe. Salma Mussa Bilal.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaomba nitoe mchango wangu kama ambavyo nitajaribu kuchangia kwenye kitabu hichi kizuri cha Mhe. Waziri, mwalimu wangu Mwalimu Haroun Ali Suleiman.

Nimeona hapa kwenye gamba hili wamevaa matenge yaliyo sare na Mhe. Rais, ninadhani anaashiria siku ya wafanyakazi. Nipongeze kwa jinsi walivyovaa vizuri na bila shaka ndani yake mutakuwa na mambo mazuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka nianze mchango wangu kwa kunukuu ukurasa wa 6, Aya 18 kama ifuatavyo:-

"Mhe. Spika, taarifa hii fupi inatoa maelezo ya ufafanuzi wa ilani ya CCM kama ilivyoahidiwa na Mhe. Rais, kutekeleza katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba, 2010 ambapo Chama cha Mapinduzi kilishinda".

Mhe. Mwenyekiti, haya ni maneno ya Mhe. Waziri ambayo nimeyanukuu na ninataka nianzie hapo kwamba lolote ambalo ni zuri kwenye hotuba hii, maana yake imezingatia ilani ya CCM. Lolote ambalo ni baya na limekosewa, maana yake ilani ya CCM haikuzingatiwa. (*Makofi*)

Kwa hivyo, wewe kataa, bingirisha, nenda unakotaka lakini huo ndiyo ukweli. Sasa wale ambao wanaoona taabu kukosolewa ilani, basi pia waone tabu kusifiwa ilani. Maana inayoongoza nchi hii ni Serikali ya *GNU*, lakini inayoongoza chini ya ilani ya CCM na ndiyo ambayo miaka yote mitano humu ndani watu wanaitungia bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimshauri Mhe. Haroun Ali Suleiman, tufungue darasa la watu wazima utusomeshe nini ilani za CCM na CUF. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, inawezekana watu wanazungumza ikawa hawajui nini msingi wa haya mambo. Sasa humu ndani muna mwalimu, wewe mwenyewe ulikuwa mwalimu, ulikuwa mwalimu mkuu, ulikuwa katibu mkuu, ulikuwa Waziri wa Elimu. Sasa tufungue darasa kidogo tusomeshane ili mtu anapojenga hoja asiseme kwamba ametukwana, kusifikiwa ni jambo kwa mtu anaona sifa, lakini unapomkosoa mtu anaona vibaya. Ndiyo changamoto za kazi Mhe. Mwenyekiti.

Sasa mimi hapo kwenye ilani ya CCM, kwenye utengenezaji wa bajeti ya 2014/2015. Mhe. Mwenyekiti, kwenye bajeti ya kawaida ya Kiambatanisho Nam. 1A, ukiangalia Mhe. Waziri alivyoeleza fedha ambayo ameipata, fedha ambayo aliomba ni shilingi bilioni sita nukta saba na fedha ambayo aliipata ni shilingi bilioni nne nukta saba. Hii sawa sawa na asilimia sabini ya fedha aliyoomba mwaka 2014/2015.

Kwa hivyo, ukilinganisha na Wizara nyengine mbali mbali; Wizara hii haikuwa na tatizo kubwa la fedha. Asilimia sabini ya fedha siyo nzuri sana lakini siyo mbaya, ni kiwango ambacho unaweza kusema kwamba fedha katika Wizara hii ziliingia na kwa msingi huo ndiyo Wawakilishi wanapaswa wapime sasa, fedha iliyoingia na ufanisi wa kazi ambao Mhe. Waziri, alisimamia.

Sasa mimi naomba nianzie hapo kwamba fedha kwa Wizara Mhe. Mwenyekiti, kwa kadiri ya Wizara zetu mbali mbali za SMZ, Wizara ya Mhe. Waziri kwa kweli ilipata fedha ya wastani, haikuwa nzuri sana zile asilimia thamanini,

lakini haikushuka asilimia sabini. Kwa maana ya kwamba ufanisi wa kifedha kwenye Wizara hii nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha kwamba aliwaangalia kwa jicho la huruma na kwa kweli fedha walipata. Zipo Wizara ambazo zina asilimia hamsini na tano, asilimia arobaini tano, asilimia sitini. Lakini Mhe. Waziri Mwalimu Haroun Ali Suleiman alipata asilimia sabini ya kazi za kawaida. Kwa hivyo, kazi za kiofisi maana yake zingefanyika ipasavyo kwa asilimia sabini ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa fedha ya maendeleo, ukiangalia bajeti ya maendeleo, fedha ambazo zimepatikana ni asilimia hamsini na mbili. Hapa kidogo ninaweza kusema kwamba fedha za maendeleo haikupatikana ipasavyo, kwa sababu ni karibu asilimia hamsini tu ndiyo iliyopatikana. Na asilimia mia moja ilipatikana kwenye Mradi wa Ajira Mbaya za Watoto. Tena ni kwa sababu gani, kwa sababu ni milioni kumi na tano tu, ni pesa ya njugu. Hii Serikali iliona tuwatilie ili wakamilishe asilimia mia moja.

Lakini fedha imepatikana asilimia ya Mradi wa Ajira Mbaya za Watoto, lakini ni milioni kumi na tano. Na ndiyo maana bado wimbi la ajira za watoto lipo, kwa nini, kwa sababu iliyotengwa ni ndogo ingawa *performance* yake ni kubwa imepatikana asilimia mia moja.

Lakini asilimia mia moja hii ya ngapi, ya milioni kumi na tano. Haiwezi hata kuhudumia jimbo moja kwa ajira mbaya za watoto. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ufanisi kama huu kwa fedha kidogo kupatikana zote, halafu vitabu vinaonesha kwamba fedha zimepatikana asilimia mia moja, eti Wawakilishi wapime idara hiyo kwamba idara hii imefanikiwa, ninaona ni mzaha.

Kwa hivyo, ufanisi unaonekana ni mzuri kwa asilimia mia moja lakini hiyo ya milioni kumi na tano ambayo nina hakika Jimbo la Magogoni ambalo lina vijana ambao wanazurura, Jimbo langu la Kiwani ambao lina vijana wanazurura, Jimbo la Mkoani ambalo vijana wanafanya kazi pwani, Jimbo la Chwaka la Mhe. Gavu ambalo watu pia wanafanya kazi pwani, haliwezi kuondosha ajira mbaya kwa milioni kumi na tano.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo naomba niseme kwamba fungu lolote ambalo linaashiria ajira za watoto kwenye bajeti hii, kama hazikupandishwa fedha hizi, mimi nitazuia kuanzia hapo. Mhe. Waziri, naomba uanze ku-*note* hiyo buti yangu ya kwanza. Ikiwa hukuweka fungu zuri la kuondosha ajira mbaya za watoto nchini kwetu na bado watoto wanaendelea kuhangaika Pemba na Unguja, hapo ninaanza kukuhesabia kwamba nitazuia fungu hili mpaka fedha tupunguze kwenye utumishi na uendeshaji, mishahara yao tupunguze na

tupunguze kwenye Idara ya Mipango na Sera ili tuwapelekee watoto wetu wasiathirike na ajira mbaya za watoto.

Mhe. Mwenyekiti, fungu la pili ni mageuzi ya utumishi wa umma. Milioni zilizoombwa ni milioni sabini, zimepatikana milioni ishirini na tisa, sawa na asilimia arobaini na tatu. Ndiyo maana kila siku taasisi zote za Zanzibar, migogoro kati ya taasisi na utumishi wa umma ipo. Hapa nyongeza haijapatikana, miundo haijakubalika, fedha za madeni zipo kwa sababu hawa watu hawakuwezeshwa kupata fedha za utendaji.

Mhe. Mwenyekiti, na hapa Mhe. Waziri, naomba uhesabu kwamba nitazuia fungu hili mpaka upandishe fedha hizi ili utumishi wa umma wapate fedha ya kutosha kwa ajili ya kuondosha matatizo na migongano ya wafanyakazi katika Idara za Serikali mbali mbali na taasisi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala jengine ambalo ninataka niseme kwa mradi wa maendeleo ni mradi wa *e-government*. Fedha iliyoombwa ni milioni tisini, lakini iliyopatikana milioni ishirini sawa na asilimia ishirini na mbili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niiombe Serikali kwa heshima kubwa waache kutufanyia mzaha. Kwanza mradi wenyewe wa *e-government* hakuna mradi, tunadanganya tu. Wananchi wametiwa hasara zaidi ya bilioni thalathini za mkopo, nitalipa mimi, mtoto wangu, mjuu wangu. Lakini leo Waziri ukimwambia huo mradi wenyewe wa *e-government* uko wapi, hakuna, ni usanii tu. Na ndiyo maana kama huu mradi una ufanisi mzuri wala wasingetenga milioni tisini zikapatikana milioni ishirini. Ni kusema kwamba hakuna mradi.

Nimesema mara kadhaa kwamba Kamati yangu ya Fedha ilipokwenda Ofisi ya *e-government*, baada ya kutoka tukaambiwa pale kwamba kompyuta zenyewe zimeazimwa. Ni usanii tu kwamba watu wanadanganywa hakuna ambalo lipo. Kwa hivyo, Wazanzibari wametiwa bilioni thalathini za mkopo ndiyo maana Serikali imeshindwa kuekeza fedha kwa sababu hakuna mradi. Na Serikali itofautishe baina ya miundombinu ya *e-government* na *e-service*. Hapo watu wanachanganywa tu. Miundombinu ni zile waya na mikonge iliyosambazwa, lakini malengo ya mradi huu ni *e-service*, ni huduma za mtandao.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, hapa anatwambia kwamba taasisi hamsini na tatu zimefungiwa huduma ya mtandao. Naomba basi ututajie ni zipi hizo na je, tangu kufungwa huduma hizo, huduma ya *e-service* tayari zimefanya kazi? Maana yake kwamba mfanyakazi yeyote kwenye Ofisi aweze kuwa na uwezo wa kufanya kazi na ofisi yake bila ya kuhangaika. Ndiyo malengo ya mradi huu.

Lakini hadi hii leo watu wanatembea na ma-*files*, wanatembea na mifuko ya fedha, wanatembea na *documents* mbali mbali kutoka ofisi hii hadi nyengine kwa sababu hakuna huo mradi wenyewe. Kwa hivyo, Mhe.Mwenyekiti, mimi niwashawishi wenzangu mradi wa *e-government* fedha yote iondoshwe, hakuna mradi wa *e-government*. Ikiwa bilioni thalathini zimefeli kuonekana, eeh! ufanisi wa milioni mia zipatikane. Wenzangu Wawakilishi ninawashawishi sana kwamba mradi wa *e-government* fedha isitengwe iondoshwe, ni sawa na kuweka sukari ndani ya bahari au ni kuweka kijiko cha sukari ndani ya bahari.

Mhe. Mwenyekiti, niwashauri sana wenzangu mradi huu tuuondoshe. Serikali wajipange tena, walete majibu kwa nini fedha za mradi huu hazikutumika kwa ufanisi upasavyo na kwa nini *thirty billions* za mkopo leo zimeingia hasara kwenye Serikali na badala yake zinatengwa milioni mia, milioni mia ishirini lakini hakuna ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa hebu nikuombeni sana kwamba mradi huu kwa vyovyote ulifeli, hakuna ufanisi na lazima Serikali itupe majibu ya kina kwa nini hakuna ufanisi kwenye mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, ninalinganisha sasa bajeti ya mwaka 2014/2015 na 2015/2016. Kwa mfano, Idara ya Mipango na Sera mwaka 2014/2015, fedha iliyoombwa ni milioni mia moja hamsini na sita nukta saba, mwaka huu waliomba milioni mia moja sitini na nne, ni nyongeza ya milioni kama tisa. Lakini Utumishi, Uendeshaji mwaka jana walitengewa fedha milioni mia tisa na kumi na moja nukta, mara hii milioni mia tisa na thalathini na tatu. Zimeshuka kwa milioni hamsini.

Sasa ikiwa hukushiba kwenye harusi, ushibe kwenye matanga, hushibi. Ikiwa Mhe. Haroun Ali Suleiman amealikwa harusi na kaka yangu Mhe. Omar, hukushiba, akipata msiba wa kufiliwa utashiba. Ikiwa hukufikia ufanisi kwa milioni mia tisa thamanini na moja mwaka jana, uje ufikie ufanisi kwa mia tisa thalathini na tatu mwaka huu. Zimeshuka kwa milioni hamsini.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Nyaraka. Mwaka jana ilikuwa ni milioni mia tatu na sabini na tano kwa sita, mara hii mia tatu sitini na nne nukta moja, imeshuka kwa zaidi ya milioni 11. Mwaka jana ufanisi ulikuwa hakuna fedha kubwa, mara hii fedha ndogo wanategemea ufanisi. Lakini Idara ya Ajira, mwaka jana milioni 126.2, mara hii milioni 117. Ikiwa mwaka jana watu hawakuajiriwa kwa sababu ya fedha hakuna, mara hii wataajiriwa kwa sababu ya fedha ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Teknolojia mwaka jana milioni 700.9 kwa jumla, mara hii 583 milioni, chini ya milioni 200 zimepungua. Ikiwa mwaka jana hatukufanya

mradi wa teknolojia Zanzibar, mara hii chini ya milioni 500 tutafanya mradi huo? Kwa hivyo, ni bajeti ya kudanganyana au ya kutiana tamaa. Lakini fedha hii haiwezeshi hata siku moja, wataalamu wetu wale walifanya kazi chini ya bajeti ya mwaka jana. Ikiwa mwaka jana fedha kubwa hatukufanikiwa, mara hii imeshuka kwa asilimia 20 fedha baadae uambiwe wataalamu wetu wataweza kufanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, nadhani hili ni jambo ambalo halifurahishi na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, bajeti hii ichambuliwe kwa kina na hizi *data* zina maana yake na tafsiri yake.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ajira Mhe. Waziri hapa amesema kwamba vijana 19,768 wameajiriwa na kati ya hao ni 5,667 wameajiriwa serikalini. Maana yake nini, maana yake kila wilaya kati ya wilaya 10, maana yake kwa mwaka wanaajiriwa watu 1,417. Kwa wilaya 10 maana yake ni miaka hiyo minne watu 142, maana yake kama ile ya Mkoani kwa mfano majimbo matano, wameajiriwa watu 30 kwa kila jimbo. Aniambie Mwakilishi mmoja tu hapa katika jimbo lake ambapo wameajiriwa watu 30 kila jimbo, aniambie mmoja tu. Anyanyuke Mhe. Mwakilishi mmoja hapa aniambie kwamba watu wameajiriwa jimboni kwangu mimi Chambani watu 30, aniambie mmoja tu.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana watu wakasema kwamba hizi ajira zinakwenda wapi, kweli watu wanaajiriwa kutoka Unguja na Pemba, lakini mara kadhaa watu wameshuhudia kwamba askari polisi, mfano jeshi anaambiwa ni Mzanzibari lakini kumbe ni Mtanganyika na kama hilo ni uongo aniambie Mwakilishi mmoja hapa na hasa wa Pemba, jimbo gani wameajiriwa wafanyakazi wake 30 serikalini. Kwa hivyo, hakuna ajira.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sekta binafsi Mhe. Waziri anasema kwamba ni watu 7,256 leo mashirika ni 6,835. Sasa hii ukijumlisha ni 27,158. Mhe. Waziri, amesema ni 19, lakini ukifanya mjumuisho wa zote hizi ni 27,158. Sasa niambie ni Mwakilishi gani jimbo lake watu wamefika 30 kuajiriwa. Sekta kubwa hapa Zanzibar ni elimu ambayo ndio inaajiri watu wengi katika majimbo yetu, hebu niambie ni jimbo gani wameajiriwa walimu 40, niambiwe hapa.

Kwa hivyo, watu wasije hapa wakaongea *data* kijuu juu, wakafurahishana hapa na wengine wakaambiwa hawana akili na wengine wanaakili. Huu ndio uchambuzi wa *data*. Wewe mwenye akili tuambie jimboni kwako kuna watu wangapi wameajiriwa, wewe mwenye akili ya *genius* tuambie watu wangapi jimboni kwako wameajiriwa? Huu ndio uchambuzi wa *data* na hakuandika maalim Saleh mgonjwa wa akili, ameandika mtu mwenye akili. Kwa hivyo, tusizungumze *data* kijuu juu, tukasema Wazanzibari huku hawatuelewi. Wazanzibari wanatuona wawakilishi wao ni dhaifu sana kwamba wanatetea mambo ambayo hayana msingi wowote.

Mhe. Mwenyekiti, suala la maslahi ya wafanyakazi. Mimi nataka nitowe siri leo. Mwaka juzi wawakilishi humu walikuwa wana malimbikizo ya pesa yao shilingi 50,000, sisi tunakumbuka humu, serikali ilitukata 50,000 hapa nyote mnakumbuka. Wajumbe wote humu ilikuwa ni fujo humu mpaka tume imekwenda kwa Rais kwa 50,000. Leo walimu wanadai nyongeza zao na wataalamu wanadai nyongeza zao mnashindwa kuwatetea. Leo walimu wanadai nyongeza zao za miaka mitano mnashindwa kuwatetea. Nyinyi shilingi 50,000 tume ilikwenda mpaka kwa Rais hapa zogo hoo! 50,000, ni aibu. Kwa hivyo, wafanyakazi wetu wanatuona sisi ni watu maslahi tu. Ikiwa shilingi 50,000 ya Hija Hassan leo ni *issue*, lakini shilingi 200,000 ya mtaalamu sio *issue*, ni aibu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nazuwia fungu la mshahara wa waziri, atuambie kwa nini nyongeza ya walimu 2012 walipewa Unguja, Pemba hawakupewa tuambiwe kwa nini. Je, ni ukosefu wa fedha, je, ni ubaguzi, au je, ni dharau. Kwa hivyo, msitetee mambo kijuu juu. Ikiwa wewe shilingi mia inakuuma mwenzako shilingi hamsini kubwa. Mtaalamu anadharauliwa miaka mitatu, baadae unakuja hapa maana yake, maana yake inafahamu vizuri, walipeni.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nawashauri wajumbe wenzangu mshahara wa waziri tuuzuwie mpaka atupe majibu. Kwa nini walimu nyongeza zao za miaka mitatu hawajalipwa, na lini watapewa *areas* zao kwa mujibu wa maslahi ya waliopangiwa na kwa nini nyinyi wawakilishi shilingi 50,000 mfanye fujo, lakini wenzenu shilingi 200,000 wavumilie.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwaambia kwamba mimi pamoja na yote hayo naunga mkono hii hotuba. Nitaunga mkono hotuba hii, lakini mpaka Mhe. Waziri akubali masharti yangu kwamba maslahi ya wafanyakazi lini watalipwa. Naelewa kwamba Mhe. Waziri wa Fedha ametenga bilioni 15 za nyongeza ya mishahara na malipo ya madeni, lakini kwa nini kuwe na malipo ya madeni, mlikuwa wapi, fedha ilitengwa na ikawekwa, fedha iko wapi? Kwa hivyo, Mhe. Waziri, malipo ya wafanyakazi wote kwa Unguja na Pemba; vikosi, walimu, madaktari, wauguzi na wote walipwe haraka sana, vyenginevyo, sio utaratibu wa haki ya wafanyakazi tunaowafanyia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nimalizie kwa kusema kwamba Idara ya Ajira humu imejisifu sana kwamba wamefanya kazi kubwa ya kuwaajiri watu na wengine wako nje ya nchi. Lakini Wazanzibari wengi wanaokwenda nje ya nchi kwa kweli wanakuwa na mtihani mkubwa. Wamekuwa wakilalamika sana kwamba maslahi yao ni madogo, na kwa kweli wakati mwengine mikataba baina ya waajiri wa nje ya nchi na Idara ya Kazi ni mikataba ambayo ina mashaka. Imeonekana kwamba upo mchezo baina ya Idara ya Ajira na wale mawakala wa ajira za nje.

Mhe. Waziri, naomba hili uliweke sawa ili tuweze kufanya vitu vya kiungwana na vya uhalisia.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba Mhe. Waziri, atakapokubali kutoa maslahi ya wafanyakazi, sio zaidi ya tarehe 01 Julai, nitaunga mkono hoja hii na kama hatutokubaliana, mimi binafsi nitazuwia fungu hili na nawaomba wawakilishi wenzangu mradi wa *e-government* tuufute, hakuna mradi ni usanii tu na badala yake twende mbele. Nakushukuru sana.

**Mhe. Salma Mussa Bilal:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, Muumba Mbingu na Ardhi, kwa kuniwezesha jioni hii kuweza kusimama katika Baraza lako hili tukufu na kuchangia angalau machache hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia wakati huu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuweza kututayarishia kitabu hiki na leo hii tunakijadili mezani.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze naukurasa wa 10 kwenye malengo makuu ya ofisi. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa malengo haya, kuna malengo manane ambayo wametayarisha katika kitabu hiki. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri malengo haya wayasimamie vizuri, wayawekee mikakati mizuri na endapo yatafanikiwa basi tutaweza kuendeleza vizuri shughuli zetu na kuweza kuimarisha serikali yetu kwa umakini kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, kitabu chake kinasema, kuongeza upatikanaji wa fursa za ajira za heshima kwa wananchi hususan vijana. Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa na vijana wengi sana ambao wanamuamko mzuri wa kusoma na kupata elimu kwa madhumuni ya kuweza kupata ajira. Mhe. Mwenyekiti, lengo hili namuomba Mhe. Waziri, alisimamie vizuri ili vijana wetu badala ya kumaliza masomo yao waweze kupata ajira ili kuweza kuendeleza Taifa lao.

Mhe. Mwenyekiti, lengo jengine ni kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi, usuluhishi na uamuzi wa mgogoro wa kazi. Pia, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuweka lengo hili, kwa sababu panapo wengi pana mengi na tunapokuwa makazini kila mmoja anakuja na ghulka yake na tabia yake. Nathubutu kusema kwamba hata vikombe huwa vinagongana seuze sisi binadamu. Kwa hivyo, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuweka sheria hii ya kazi ya usuluhishi kwa

migogoro mbali mbali ambayo inatokea makazini, ili kuweza kuweka utaratibu mzuri katika ofisi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende katika lengo la tatu ambalo linasema, kuanzisha na kusimamia mpango endelevu wa upatikanaji wa rasilimali watu wenye sifa. Mhe. Mwenyekiti, hili nalo ni lengo zuri. Ukiangalia tumekuwa na Chuo cha Utumishi wa Umma, chuo ambacho kimekuwa kikitoa mafunzo ya aina mbali mbali, kinatoa mafunzo ya kada mbali mbali, kinatupikia vijana na wafanyakazi wetu ili waweze kufanyakazi vizuri na kwa umahiri katika ofisi zetu mbali mbali.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana lengo hili lisimamiwe kwa umakini ili tuweze kupata rasilimali watu wenye sifa nzuri. Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika upatikanaji wa rasilimali watu wenye sifa, niombe sana katika Chuo cha Utumishi wa Umma, kumekuwa na vijana na wafanayakazi wengi sana ambao wanakwenda kusoma, ambao wanaomaliza shule. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Moja ni tatizo la usafiri, vijana wetu wamekuwa wakisumbuka sana na usafiri.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kwa kupitia Mhe. Waziri wa Fedha, chuo kiweze kupatiwa usafiri maalum, ili vijana wetu wawe wanafika chuoni kwa wakati na kuondoka kwa wakati. Tuige mfano wa Chuo cha Chwaka. Chuo cha Chwaka na Chuo cha Afya Mbweni, wamekuwa na usafiri wa kuwasaidia wanafunzi wao ili waweze kufika kwa wakati na kuanza masomo kwa wakati na pia inawapunguzia hofu ya kwamba kila wakati mtu anahisi nitafika saa ngapi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, awatafutie gari la chuo ili aweze kuwarahisishia wanafunzi hawa.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika chuo ningeomba kwamba kuna vijana wetu wengi ambao sasa wanamaliza shule na vijana wengi sasa hivi wana mwamko wa kusoma na kuongeza elimu katika kada zao za kazi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeomba ifanywe juhudi ya makusudi ili lile jengo la chuo liweze kumalizwa na tuweze kupata nafasi nzuri za kupata vijana wetu kuingia kwenye kada hiyo ya masomo. Kwa sababu hivi sasa imekuwa chuo kinachukua wanafunzi lakini wengine wanasoma mjini, wengine wanasoma sehemu mbali mbali. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana wizara ichukuwe juhudi za makusudi ili iweze kumaliza chuo kile kupandisha ghorofa moja juu ili kuwe na nafasi nzuri ya wanafunzi wetu kuweza kusoma kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana wizara. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweka lengo hili la kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka za serikali. Mhe. Mwenyekiti, hivi

karibuni kama tuna kumbukumbu kwamba kumekuwa na upotevu mkubwa wa nyaraka za serikali. Nakufikia hadi kuunda Kamati Teule ili kuweza kuchunguza jinsi ya upoteaji huo na upatikanaji wa nyaraka zetu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba huu uimarishaji upewe kipaumbele. Pia, nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kuweka *CCTV* katika ofisi ya nyaraka, kwani hii itasaidia hili suala la upotevu wa nyaraka liweze kudhibiwa vizuri. Mhe. Waziri, naomba nikupongeze sana kwa suala hili.

Vile vile, niiombe serikali kwamba suala hili lisiwe tu kwa ofisi ya nyaraka, lakini iwe kwa ofisi zote ziwekwe *CCTV* ili kuzuwia upotevu. Mfano hai wa umuhimu wa *CCTV*, kuna ofisi fulani ilikuwa imetokezewa na tatizo la wizi wa vifaa vya ofisi, lakini kwa bahati nzuri kulikuwa na *CCTV*, wezi wale walipatikana kirahisi na ikajulikana, wakakataa na baada ya kukataa wakaoneshwa jinsi ya vile walivyochukua, kwa hivyo, ilisaidia. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba serikali iweke kipaumbele kwa ofisi zote ili kuondoa matatizo ya wizi katika maofisi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nina lalamiko kwa Mhe. Waziri. Naomba Mhe. Waziri awaangalie kwa jicho la huruma wafanyakazi na watendaji wa ofisi ya nyaraka, kwani wafanyakazi hao wanaathirika sana na madawa ya kutibu nyaraka. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, wafanyakazi hawa uwaangalie kwa jicho la huruma, ili wapatiwe huduma ya kuwasaidia ili wasiendelee kuathirika na madawa hayo ambayo wanatumia kwa ajili ya kutibu nyaraka.

Mhe. Mwenyekiti, lengo jengine amesema kwamba ni kuhakikisha wizara na ofisi zote za umma zinafuata miundombinu ya utumishi. Mhe. Mwenyekiti, hili lengo ni zuri, hivyo naomba hili suala alichukulie kwa uzito wa hali yake ili liweze kufanikisha na tuweze kuwa na miundombinu mizuri ya ajira.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuimarisha usalama wa afya kazini ili kuhakikisha hali bora ya usalama wa afya katika sehemu za kazi. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri na kubwa sana, kwa sababu bila ya kuwa na wafanyakazi wenye afya, sidhani kama kutakuwa na utendaji na utekelezaji mzuri katika ofisi mbali mbali. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana suala hili lisimamiwe vizuri, liwekewe mikakati mizuri ili wafanyakazi wetu waweze kuwa na moyo na hali ya kufanya kazi wakiwa na afya bora.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu chake alieleza kwamba kuna mikakati ya kuanzisha bima ya afya kwa wafanyakazi, kwa hivyo, naomba ichukuliwe juhudi za makusudi suala hili liweze kutekelezwa mapema iwezekanavyo ili wafanyakazi wetu waweze kupata matibabu kwa kutumia bima ya afya ili wawe na uhakika wa matibabu na waweze kufanya kazi kwa usalama zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, halafu jengine katika suala la ajira, nisisitize kwamba katika ajira zinazotolewa na mimi bado niendelee kuwatetea watu wenye ulemavu, kwamba waangaliwe vizuri sana katika upatikanaji wa ajira. Wakati zinapotokea ajira katika taasisi mbali mbali kuwe na mkakati maalum angalau kila ajira ambayo inatokea na kama vijana wetu wenye ulemavu ambao wenye sifa hizo ningeomba sana wapatiwe ajira hizo ili na wao waweze kusaidiwa na waweze kujisaidia katika maisha yao. Mhe. Mwenyekiti, niombe sana kwamba waangalie vijana wenye ulemavu waweze kupatiwa ajira na wao waweze kujisaidia katika shughuli zao za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mchango mkubwa sana kwa sababu mengi yameshachangiwa lakini kabla ya kumaliza mchango wangu naomba kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, niweze kuipongeza Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa ya awamu ya saba inayoongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Mohammed Ali Shein kwa utekelezaji wake wa ilani ya CCM kwa mambo mbali mbali ambayo imejipangia katika mpango huo wa ilani.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali na nimpongeze sana Mhe. Rais kwa utekelezaji wa ilani pamoja na viongozi wote na Mawaziri wote ambao wanatekeleza hii ilani ya Chama cha Mapinduzi, baada ya hayo naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa maboresho katika Wizara hii au hoja hii iliyoko mbele yetu, mimi nataka nianze na ukurasa wa irishini wa kitabu cha Mhe. Waziri pale kuna Idara ya Nyaraka, na nataka nizungumze kwa sababu ya uzoefu Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nyaraka ni taasisi moja muhimu sana katika nchi yetu na sio nchi yetu tu, yaani katika kila nchi idara hii ni taasisi moja muhimu ambayo inapaswa kutunzwa sana. Taasisi ambayo ndani yake mna kumbukumbu zinazotoa sura ya nchi yetu, zinazotoa historia ya nchi yetu, kwa hivyo, vizazi na vizazi hakuna pahala pengine pa kupata sura na historia ya nchi yetu isipokuwa kule kwenye Idara ya Nyaraka. Sasa mimi bado naendelea kusikitika kama ambavyo vikao vilivyopita niliwahi kusema kwamba idara hii imetelekezwa sana, Serikali haijaona umuhimu wa kuitunza hii Idara ya Nyaraka.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naangalia bajeti ya mwaka jana Idara hii tuliidhinishia kiasi gani cha fedha na ndani ya kitabu cha Mhe. Waziri, ripoti yake inavyosema namna pesa zilivyoingizwa, Idara hii mwaka huu unaomalizika tuliipatia shilingi milioni 375, 959,000/= lakini hadi kufikia Machi fedha ambayo Wizara ya Fedha imeitilia Idara hii ni Shs, 236,439,117/= kati ya hizo milioni 171 kwa ajili ya mishahara. Kwa hivyo, *OC* ambazo ndizo hasa zingeweza kuitunza na kuiendeleza

ile ofisi pesa zilizopatikana ni 64,000,000 pekee, wakati kwa mujibu wa tulivyoidhinisha mwaka jana ilikuwa zipatikane milioni 139,219,000.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo haijafika hata asilimia 50 ya *OC* ambayo tuliidhinisha kuipeleka katika Idara ya Nyaraka. Sasa kamati yangu ilikwenda kukagua pale, ukilinganisha mazingira yalivyo pale unaweza kuona kwamba tatizo idara hii haiwezi kufanya kitu kwa sababu fedha kwanza zilizoidhinishwa ni kidogo sana na hicho kidogo ambacho tuliwaidhinishia basi kilichopelekwa hata asilimia 50 haifiki. Kwa hivyo, hata tukimlaumu Mkurugenzi, hata tukiilaumu ile idara nzima kwa kweli tutakuwa tunawaonea tu.

Mhe. Mwenyekiti, idara ile majengo yake hayafai, ni mabovu sana, ukiingia mule ndani ile miundombinu ambayo inatumika kuhifadhia zile nyaraka, basi ni vichekesho. Tunakwenda sisi tunafanya ziara hapa mara nyengine tunakwenda nchi za watu na tunaona wenzetu wanavyotunza majengo yao ya namna hii. Ukienda China maana yake utafikiri lile jengo la *Archive* utafikiri ni Ikulu, safi kabisa na hali ya hewa nzuri, hapa wewe nenda kaingie kwenye kile chumba cha nyaraka ukae dakika tano utizame kama hutapata mafua, *condition* ni mbaya sana.

Sasa nyaraka zenyewe ni karatasi zile ambazo zinahitaji *temperature* maalum, zinahitaji kila kitu maana yake zitunzwe, ndio maana sasa zinanyambuka nyambuka. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia lile jengo lenyewe liko katika pahali ambapo hapana usalama wa aina yoyote, kuna nyumba pale ya mtu binafsi wana-*share* ule ukuta wa *fence* shirika na ile idara.

Kwa hivyo, ule mlango wa *fence* wa idara lazima ubakishe wazi kwa sababu yule mwenye nyumba lazima aingie nyumbani kwake. Tumepiga makelele wee, jamani huyu mtu ile nyumba ni ya dhahabu hata iliyokuwa hainunuliki. Serikali inashindwa kitu gani, ama kumuondoa yule jamaa, kumpa hizo pesa anazotaka akahama pale angalau lile jengo likawa katika usalama wa hali ya juu, lakini mpaka leo kimya, sijui tatizo liko wapi.

Kwa hivyo, kama Mhe. Hija, alisema yeye keshaweka buti moja kwa ajili ya Mhe. Waziri na mimi naweka ya pili, kama sijapata jawabu yule mwenye nyumba mule atahama lini. Fungu hili mimi nazuia leo, sijawahi kumfanyia waziri wangu ni mtu mmoja namuheshimu sana, lakini kwa sababu ya usalama na unyeti wa idara ile lazima sasa mtu yule pale ahamishwe. Serikali inafanya mambo makubwa makubwa ya pesa, tushindwe kuondoa kijumba kile kimoja pale, lazima tupate jawabu nzuri bwana, haiwezekani.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii watu wanaingia pale wanaiba nyaraka ovyo ovyo kwa sababu ya kutokuwa na usalama wa kutosha, baada ya makelele mengi ndio sasa

hivi wameweka ile *CCTV camera*, lakini wanaweka wakati punda ameshatoka bandani ndio wanafunga banda, yaani watu wameshaiba zamani. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Waziri, hivi sasa afanye mazungumzo na watendaji wake lakini ionekane mwenye nyumba aliyeko mule anahamishwa kama ni kupewa kiwanja, kama ni kupewa nyumba nyengine, nyumba za serikali bado zipo apewe lakini mule ahame ili tuone kama idara ile inakaa katika mazingira salama kwa ajili ya vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka kwenye idara hiyo, sasa nije kwenye sijui hii ndio Kamisheni ya Kazi maana yake hii wizara ina mambo yanayofanana sana; Kuna Kamisheni ya Utumishi, Kamisheni ya Kazi na mambo mengi ukiangalia yanafanana fanana zote zinashughulikia mambo ya ajira na utumishi, lakini yamegawana gawana idara tofauti. Sasa nilichokusudia kusema mimi Mhe. waziri, atajua akiweke katika idara gani. Lakini nakusudia kuzungumza matatizo wanayopata watu katika ajira za sekta binafsi, serikali haina uwezo wa kuajiri vijana wetu wote na ndio maana ina jaribu kutafuta ajira kila uchochoro mpaka nje ya nchi.

Sasa kuna wenzetu sekta binafsi wanatusaidia kuajiri vijana, nafikiri ni Kamisheni ya Kazi kama sikusei. Lakini sasa kinachowakuta vijana wetu kwenye sekta binafsi kwa kweli wanadhalilika sana, na Mhe. Waziri kama utakumbuka hii hoja ni kongwe maana kila mwaka wa bajeti ukifika suala hili tunalizungumza, na tukitoka pale katika utekelezaji kuna watu kadhaa wa kadhaa vijana wanatujia wanatwambia bwana mimi nimedhalilishwa hivi, sisi bwana pale tunahangaishwa hivi, sisi tunakoseshwa hiki, maneno mengi yanakuwa.

Sasa mimi nadhani kama sheria hazijakaa vizuri Mhe. Waziri, basi hebu sheria zikae vizuri lakini vijana wetu wanadhalilishwa sana, vijana wetu wanafanyishwa kazi bila ya mkataba, vijana wetu wanalipwa maposho yasiyostahiki, vijana wetu wanaachishwa kazi ovyo na mtu akishakuwa hana mkataba hasa muajiri ni hiari yake anamuachisha kazi bila ya kujali haki za yule kijana. Kwa hivyo, watu wanapata tabu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kijana alinijia lakini alinisaliza Mtume, msalie Mtume usije kunitaja. Nikamwambia sikutaji lakini nitasema habari yako. Kuna Kampuni ya *Runs Building Contractor* hawa nao wana *problem,* naomba sana serikali sasa iwakague hawa kama hawajenda kuwakagua basi ikawakague. Kuna watu hawajazishwi mikataba, watu hawalipwi ipasavyo, ushaona bwana, kuna watu waliajiriwa kama walinzi katika Kampuni ya *ZANTEL* ikatokea siku wakaachishwa kazi tu, kumbe watu wenyewe hawakujazishwa mikataba mpaka leo hawajalipwa haki zao. Naiomba sana serikali ishughulikie haya mambo, kuna Kampuni ya ulinzi hii ya *Ultimate* nayo siku zote makelele watu ukizunguka hapo mtu

anakwambia bwana sisi tunahangaishwa, sisi hatujazi mikataba, yako mengi Mhe. Waziri, ukienda mahotelini hali kadhalika ni hiyo hiyo.

Kwa hiyo, nafikiri kwa mujibu wa taarifa hizi ni kwamba hii idara yako inafanya ukaguzi katika sekta binafsi kugundua matatizo haya, lakini kwa nini bado yanaendelea. Labda adhabu inayotolewa kwa hawa waajiri haitoshi, kwa hivyo, nilikuwa nashauri sana kama ni kwa sababu ya sheria basi ilete sheria tuibadilishe hapa, tuiweke sawa lakini hawa ndugu zetu masikini za Mungu wanaotafuta ajira huko basi wasiendelee kukosa haki zao kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye taasisi nyengine na hii ni Kamisheni ya Utumishi nadhani  sina uhakika vizuri kama ninavyosema muna idara nyingi sana humu zinazofanana. Sasa hapa tatizo langu ni ajira za walimu.

Mhe. Mwenyekiti, bado tuna ukosefu mkubwa sana wa walimu hasa Kisiwa cha Pemba, na tukiyasema mara nyengine huwa tunapata jawabu kwamba labda walimu wako sawa mara nyingine tunaambiwa hivyo. Inawezekana kama wako sawa lakini Kisiwa cha Unguja, Pemba kuna *problem* na hapa Unguja pia basi labda kwenye hapa Mkoa wa Mjini Magharibi ndio unakuta walimu pengine wanakidhi haja, lakini ukienda mashamba pia kuna *problem* ya ukosefu wa walimu.

Sasa nilidhania Kamisheni hii kama ndio inayohusika na kutoa ajira au kuishauri serikali kuhusu ajira, basi ajira zikitoka zitoke kwa *priority*, tuangalie sekta ya elimu umuhimu wake na sekta ya vikosi. Hivi karibuni kulikuwa na kelele kubwa kweli kweli watu wanakwenda huku na huku kuna ajira za vikosi zinatolewa. Lakini wanatoa ajira za vikosi wanaacha ajira za walimu, sekta ya elimu mimi nadhani ni muhimu sana.

Sasa hizi ajira zikitoka kama ni chache, mimi najua ni chache, lakini tuangalie na *priority*, elimu na vikosi wapi na wapi, hebu watwambie kwa vigezo gani hata ikawa vikosi sasa hivi ina ukosefu wa watu mpaka waajiri watu karibu elfu ngapi sijui, lakini walimu hatuna watu vijana waliosoma wapo wamehama wengi wao wako Mikoani kule ukienda Tabora utakuta vijana wa Kizanzibari wako kule wameajiriwa tena ualimu wakati sisi tuna njaa ya walimu hapa. Sasa kama nafasi ipo kwa nini hawaajiriwi?

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo ni kero sasa katika nchi yetu ni kuhusu hawa watu ambao wamefika umri wa kustaafu, lakini anastaafu leo kesho unamkuta anarudishwa kazini, ukiuliza aah, kajazishwa mkataba wa miaka miwili. Hili limekuwa kero kwa sababu kuna watu vijana wetu wapya kabisa wana elimu nzuri sana za kutosha kuliko hawa ambao wanarejeshwa kazini wanahangaika na

matokeo yake ndio wanahama, lakini mtu anang'ang'ania. Hii iliwekwa kwa dharura labda taaluma aliyonayo mtu fulani hapa nchini haipo.

Kwa hivyo, kwa sababu hatuna mtu mwengine wacha tumshikilie angalau miaka miwili atusaidie dharura kama hiyo, lakini imekuwa hasa ni mtindo mtu akimaliza muda leo akistaafu akapewa mafao yake kesho unamkuta anarudi kazini aah, ajira ya miaka miwili, kwa nini wakati fani aliyonayo zimo tele hapa katika nchi kuna vijana wetu wanazo tele. Sasa naomba hili hebu lipunguzwe kidogo ili vijana wasiendelee kunung'unika wakiwa hawana kazi, hawa wazee bwana wameshatumikia muda mrefu, wameshafaidi sana katika nchi hii, hebu wapumzike wawaachie watoto wao tena.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine hapa nilisema niliguse kidogo ni kuhusu Chuo cha Utawala wa Umma na hapa wala sina jambo kubwa. Ukisoma hiki kitabu cha Mhe. Waziri, kinaeleza kwamba moja katika majukumu ya Chuo cha Utawala wa Umma ni kufundisha maadili ya kazi, kuwafundisha wale vijana wanaojiunga na kile chuo maadili ya utumishi. Sasa kama mtu atafanya utafiti mdogo tu anaweza akagundua kwamba watumishi wetu hasa Zanzibar basi hawana maadili wengi wetu. Unamkuta mtu anatoka kazini wakati anaotaka mwenyewe, unamkuta mtu ukienda wewe kuomba huduma pale hayo madaha na maringo atakayofanyia unaweza ukashangaa, aah, hivyo huyu kweli yuko *serious* tofauti sana na nchi za wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, nchi za wenzetu ukienda kutaka huduma basi unakuta watu wanakujali bwana, wanakujali kama aliyekuwepo hapa ni mtu na heshima zake na nini. Lakini hapa na hasa hasa hospitalini ndio kumezidi, ndugu zetu walioko hospitalini kwa kweli unafika pahali unahiari ukatafute mzizi wa mti ule kuliko kwenda pale Mnazimmoja kuomba huduma ya afya, sio utafanyiwa jeuri maana yake mpaka maneno machafu ya matusi pia utapewa wewe, tena hawajali kama huyu mtu ni kiongozi au vipi maana yake ah! Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli inakera. Maana yake unakwenda wewe kiongozi wanakudharau. Ikiwa wewe kiongozi wanakudharau eh! Je, mtu wa kawaida atafanywa nini. Sasa nilikuwa naomba sana hichi Chuo kiendelee kutoa mafunzo, lakini na sheria hebu zichukue mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mama mjamzito siku moja kafa, kenda kujifungua kafika pale anaomba wale wasaidizi waje kumsaidia kumpeleka huko wanapojifungulia watu hawaji, akalalamika mpaka akamuomba mja mzito mwenzake pale aje amsaidie kujifungua tena kwa lugha ya kutoa machozi, anasema; "Njoo unisaidie, nikishakujifungua na mimi nitakusaidia, njoo nakufa miye". Mpaka mama yule kakata roho, hakuna daktari aliyekuja kumsaidia.

Sasa haya ni maadili mabovu sana, na sio huko hospitali tu, takriban taasisi nyingi za serikali ndivyo zilivyo, unakwenda watu hata hawajali kama amekwenda mtu anataka huduma. Sasa Chuo kiendelee kutoa taaluma, lakini nadhani na wasimamizi, Wakuu wa Idara hizi kwa kweli wajitahidi ili na sisi angalau, tuonekane kama tunawajali watu. Maana yake mtu au binaadamu mwenzako ukimdharau unampa mawazo mengi sana.

Jengine na la mwisho kuna *indicator* Mhe. Mwenyekiti, ya kurudi nyuma. Nakumbuka zamani tulikuwa katika *stage* hii kiinua mgongo alikopwa mtu mpaka mwaka mpaka miaka miwili huko tunakotoka. Lakini hapa katikati utawala wa Dokta Karume hili liliondoka lote, ikawa mtu akistaagu anapewa pesa zake pale pale. Sasa *trend* inavyoendelea watu wanaanza kucheleweshewa tena mpaka wanaanza kunung'unika sasa hivi.

Namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, afanye fanye na ajiweke tayari ili haya manung'uniko yasiendelee kuwa makubwa, kwa sababu yakiendelea kuwa makubwa haya watu wataanza kuisema ilani ya Chama cha Mapinduzi na mimi sitaki nitaje hivyo kwa sababu nikitaja hivyo wenyewe wanakuwa wakali. Lakini kwa sababu serikali hii ni yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa inaongozwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, matokeo yakitokea basi watu watailalamikia ilani. Nafikiri sio vyema kufika huko.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, ajipange pange huko kwenye hazina yake ahakikishe kwamba watu wanaostaafu wasiendelee kucheleweshewa viinua mgongo vyao. Unamuondoa mtu kutoka kazini unampeleka katika maisha ya kiraia anakuwa mgeni katika sekta ya maisha ya kiraia, kama hujampa ule mshiko wake ukamsaidia kidogo utamfikisha pahala pabaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nina hakika Waziri wa Fedha kuanzia leo atakwenda kufanya kazi zaidi ili watu wasicheleweshewe mafao yao. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chonga mimi naunga mkono hiyo hoja, lakini buti ipo moja mpaka nipate jawabu nzuri.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kupata nafasi hii ya kuweza kuzungumza machache katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kama kawaida yangu. Nataka nimpongeze kwa kazi nzuri anazozifanya. Mhe. Waziri huyu simsifu kwa kuwa tu mwalimu wangu lakini kila sekta anayokabidhiwa basi

anakuwa anajitahidi sana kuisimamia kikamilifu ili kuhakikisha kwamba yule aliyemkabidhi ile dhamana hamuangushi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sisi kama Wawakilishi wa Wananchi nataka niseme kwamba serikali yetu, mimi najaribu kutathmini ndani ya kipindi cha miaka mitano. Kwa sababu hii ni bajeti ya mwisho katika awamu yake ya Kwanza serikali hii ya awamu ya saba. Kwa hivyo, ni lazima tukiri tumeona mabadiliko makubwa sana. Kitu nilichokuwa nakiangalia kwa sababu hawa Mawaziri wote wanafanya kazi ya mtu mmoja tu ambaye aliyewateuwa. Kwa sababu kazi hizi zote angelishindwa mtu mmoja kuzifanya yeye peke yake. Nilikuwa najaribu kuziangalia zile ahadi mbali mbali ambazo Mhe. Rais alizokuwa akizieleza wakati wa Kampeni. Lakini vile vile leo hii anakamilisha kipindi chake cha mwanzo cha miaka mitano kwa asilimia kubwa sana ameweza kutekeleza yale malengo yake aliyoyakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme na niwambie wenzangu kuongoza nchi sio jambo la masihara, wala sio jambo dogo. Kwa sababu Dokta Ali Muhammed Shein, amepokea serikali ambayo imeundwa katika mfumo mpya kabisa, kwanza ile hali tu ya kuituliza nchi mpaka kwamba leo tunaingia miezi michache kabla ya uchaguzi tunaishi kwa amani na utulivu tena na mapenzi makubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, huwezi ukatengeneza maslahi ya watumishi wako kama nchi haipo katika hali ya uvulivu na amani. Sisi sote mashahidi hapa tulikuwa tunaona jinsi gani ya maslahi ya watumishi wa umma yalivyokuwa yanaboreka kwa kusua sua. Lakini ndani ya miaka mitano hii Mhe. Mwenyekiti, hata Wawakilishi na wao sasa hivi hali zao tofauti na walivyokuwa huko mwanzo. Sasa naamini hii awamu ya mwanzo Mhe. Rais alikuwa anaweka miundombinu yake. Sasa naamini awamu yake ya pili basi kwa kweli hali itaboreka katika mazingira makubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki nitoe mifano labda kwa kusema nampendelea mtu fulani, hebu jiangalie wewe mwenyewe unapoingia jimboni, mwanzo katika hatua za mwanzo unakwenda, unasema na unapanga miundombinu, lakini hebu angalia unapoingia mara ya pili, angalia ile *speed*. Sasa Mheshimiwa, mimi nadhani lazima tukiri maslahi ya watumishi wa umma kabla ya serikali hii ya awamu ya saba yalikuwa yapo tofauti maslahi yalivyo hivi sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nitoe pongezi kwamba kwa kile Chuo cha Utumishi wa Umma kwamba sasa hivi chuo kimetulia na kinafanya kazi zake vizuri. Ulikuwa unatusikia siku zote Mwenyekiti hapa tukisimama, Chuo cha Utumishi wa Umma, Chuo cha Utumishi wa Umma. Mwanzo walikuwa wakikaa katika mazingira ambayo yalikuwa sio salama sana. Lakini kipindi kile tulimkamata sana Mheshimiwa Mwalimu wangu, maana mimi nina walimu wawili

humu; mwalinu wangu wa kazi Mhe. Haji Omar Kheri. Tulimkamata sana katika Chuo kile na kwa kweli kulikuwa kuna uchafu na aliusimamia kidete, sasa hivi uchafu umeondoka, sasa hivi Chuo kinakwenda.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo kile ndicho kinachowaboresha hawa watumishi wetu Mhe. Mwenyekiti. Huwezi kuwa na watumishi ambao mtu tokea anaingia, kama alikuwa anaingia na elimu yake mpaka anazeeka anabakia na elimu yake ile ile. Chuo kile tunashukuru sasa hivi watumishi wetu wanapata taaluma na vijana wengine wanakwenda pale wanapata taaluma, tayari wengine tumeshaona katika sekta mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kuna ile hoteli kubwa iliyofunguliwa hivi juzi, tayari kuna watumishi pale karibu sita au saba ambao wametoka katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Sasa Mhe. Mwenyekiti, haya ni matunda ambayo lazima sisi kama Wawakilishi wa wananchi tuweze kuisifu serikali yetu.

Jengine mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia hizi Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, hivi karibuni ulikuja Mswada wa sheria wa kuanzisha Sheria ya *PPP*. Mswada ule umekuja hapa Barazani ingawa ulipokuja Mswada ule mimi nilikuwa safarini, lakini nasikia Waheshimiwa kwa kweli muliupongeza sana. Muliupongeza inawezekana wengine kwa kujua nini kitakuja kuendelea baadae, lakini wengine waliupongeza kwa kuwa ule Mswada umekuja.

Sasa mimi nataka nikwambieni nchi zote duniani Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia ajira ya serikali sijui kama inazidi asilimia 25, ajira zilizobakia zote zipo katika *private sectors.* Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyezi Mungu na nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, *Alhamdulillah* nimetembea nchi nyingi sana duniani na nimekutana na Wazanzibari wengi sana duniani. Mhe. Mwenyekiti, katika Wazanzibari hao walioondoka hapa kwenda kufanya kazi nchi za nje basi unaweza kusema labda ni asilimia 0.1 labda ndio waliobahatika kufanya kazi serikalini, wote wanafanya kazi katika *private sectors*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mswada ule wa *PPP* ni Mswada ambao tunategemea nchi yetu itapata wawekezaji imara, wawekezaji wakubwa ambao watakuja kushirikiana na serikali katika kuanzisha kampuni mbali mbali na wataweza kuzalisha ajira nyingi sana hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, unajua mtu anaweza akataka kufanya jambo fulani lakini akitaka kufanya jambo lile lakini serikali haijatekeleza sheria ya kumruhusu kuweza ku-*penetrate* akaweza kufanya ile shughuli. Kwa hiyo, ile sheria ya *PPP* ambayo tuliyoipitisha Mhe. Mwenyekiti, tunaamini awamu ya pili ya serikali hii tunategemea itazalisha ajira nyingi sana, makampuni mengi yatakuja na vijana kitu

ambacho ninachowaomba sasa hivi tuondokeni vijiweni, sio wakati tena sasa hivi wa kukaa vijiweni. Sitaki kusema kwamba watu wasicheze karata na bao kwa sababu ule ni utamaduni. Lakini tuwaachie wacheze karata na bao wale ambao wamesharudi kwenye kibarua, kibarua kwa Kiswahili ni kazi au ajira, yoyote hata kama ya mtu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Waziri, anaeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma kwa sababu humu kuna mambo ya kazi. Naomba sana aingize mkono wake katika Vyuo vya Amali, wala asiseme kwamba vyuo vile viko chini ya Wizara ya Elimu. Vyuo vile Mhe. Waziri ulivianzisha wewe mwenyewe, tunataka uvilee na kama utaviboresha Mhe. Mwenyekiti, hayo makampuni yanayokuja malalamiko yatapungua, vijana wetu watakuwa wamepata *skill* pale wataingi katika hizo ajira nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, naomba sana, tunajua kwamba serikali mmegawana majukumu, kila mmoja kapewa mipaka yake lakini katika mipaka hii mnaweza mkasaidiana maarifa kuboresha eneo fulani ili kuweza kusaidia katika eneo jengine.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri akae na Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma akae na Mhe. Waziri wa Fedha, wazungumzie mikakati gani na Mhe. Waziri wa Fedha na yeye akae vipi na Mhe. Waziri wa Fedha ya Jamhuri ya Muungano katika kudhibiti upandaji wa dola. Mhe. Mwenyekiti, Rais wetu anaweza akafanya jitihada kubwa, lakini ile jitihada matokezeo yake wananchi wakawa hawaiyoni ile faida yake. Kwa nini nikasema hivyo?

Mhe. Mwenyekiti, tukishindwa kuudhibiti upandaji wa dola, serikali hata ipandishe mshahara kiasi gani, wananchi bado watahisi ugumu wa maisha upo pale pale. Kwa sababu kile ambacho alichotarajia kununua kwa thamani ya pesa ya wakati ule, dola ikipanda hawezi tena kukinunua kwa thamani ile ile, kwa hiyo, *automatically* utaona mshahara umepanga lakini matumizi au *purchasing power* ya ile fedha inakuwa inashuka. Sasa hili naomba sana, ni suala gumu kwa sababu Mhe. Waziri wa Fedha, peke yake hawezi kulitekeleza peke yake. Lakini naamini kwa mikakati ya pamoja basi Mawaziri hawa wanaweza wakaa na wakakaa na Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuangalia ni namna gani dola wanaweza wakaidhibiti upandaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, katika huu mwaka mmoja wa mwisho kwa kweli dola ilikuwa imepanda kwa kasi kubwa sana, ilikuwa inaanza kututishia amani. Hili nilikuwa naoma sana haya maboresho anayofanya Mhe. Waziri yanaweza yakaja yakakwazwa huko mbele tunapokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu niliwasikia wanazungumzia baadhi ya migogoro, wafanyakazi na baadhi ya wamiliki wa Mahoteli. Mimi nawaomba sana, hivi karibuni nilisikia kuna wafanyakazi fulani waliwahi kunipigia simu nikawambia kwamba utaratibu  mimi sina mamlaka yoyote ya kuingilia masuala ya Ofisi, isipokuwa leteni barua Barazani katika Kamati husika ili yaweze kuyashughulikia. Nafikiri Mhe. Waziri, naomba sana huu mgogoro wa wafanyakazi wa Hoteli ya *Residence* hetu naomba Mheshimiwa ufuatilie kwa karibu.

Nashukuru sana Mhe. Waziri, unanieleza kwamba tayari na ninavyokujua kwa kweli wewe mezani kwako hapakai taka. Kwa hiyo, maamini suala hili utaweza kulipatia ufumbuzi wa haraka. Kwa hivyo, naomba vijana wetu wenye mgogoro na yule Muwekezaji katika Hoteli ya *Residence* basi tulieni, Mhe. Waziri, ameshakubali ataweza kulitatua tatizo lenu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie Idara ya Ajira, Idara hii ya Ajira nimejaribu kuangalia katika hii programu ambazo unazokwenda nazo iko katika *Vote* E01 ambayo ni programu 03 inayoshughulikia masuala ya uzalishaji wa ajira.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina matumaini makubwa sana na huu mpango wa sasa hivi wa serikali. Wakati mwengine nilikuwa najiuliza serikali walikaa wakafikiria nini kuleta hii *programme basic budget,* kwa sababu hii fedha zinalengwa moja kwa moja kwenda kutatua tatizo maalum.

Sasa mpango huu ni mpango mzuri sana, lakini namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa mara nyengine tuangalie safari hii tuondoe tena ile mihali mihali ya kuoneana haya ya kufumbiana macho. Fedha tuhakikishe kwamba inakusanywa serikalini. Kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti na wewe Mwenyekiti mwenzangu tulimshauri sana tulipokuwa kwenye Kamati ya wenye viti Mhe. Waziri, namna gani ya ukusanyaji wa mapato na sisi tulimuahidi yale tulomshauri kama angaliweza kuyatekeleza ile bilioni 30 aliyetaka kukopa kwa kujazia bajeti yake hatoikopa tena isipokuwa ile *collection* atakayoweza kuikusanya itaweza kutekeleza hizi programu

Mhe. Mwenyekiti, programu hizi alizozieleza Mhe. Waziri, akiweza kuzitekeleza na akiweza kuingiziwa fedha kwa wakati, tunaamini bajeti inayokuja tutakuja kuwa tunazungumza masuala mengine tena. Kwa sababu ni fedha ambazo zimekusanywa s*pecifically* inakwenda kuangalia eneo fulani. Sasa hapa nimejaribu kuangalia zile *job centre* au zile Kampuni binafsi ambazo zinazohangaika kuwatafutia vijana ajira.

Mimi ninashukuru kwamba Kampuni zipo nyingi, sasa hivi na kweli kuna vijana wetu wengi sasa hivi wako nje ya nchi, hata hivi karibuni tulipokwenda Qatar

wengine tumekutana nao, tumezungumza nao na kama nilivyokueleza Mhe. Waziri kwamba tulipokwenda Qatar baada ya kuona zile fursa za ajira zipo nyingi basi na mimi nimehamasika hivi sasa hivi tayari nimeshaanza *process* ya kufungua Kampuni ya *Job opportunity* ya kuwahangaikia kuwatafutia vijana ajira ndani na nje ya nchi. Nikishakamilisha ule mpango kwa kweli nitakuja nipate msaada mkubwa hasa kwa hawa wataalam wako katika hii sekta ya ajira.

Hapa Mhe. Mwenyekiti, na mimi vile vile nategemea nitatoa ajira kwa vijana wa Vyuo Vikuu. Unajua tunakuwa tukiwalalamikia sana vijana wanamaliza Vyuo Vikuu hawana ajira, tunayo fursa sisi ya kutengeneza utaratibu hawa vijana wakitoka katika vyuo na wao wakaanzisha Makampuni. Mhe. Mwenyekiti, nikishamaliza mchakato nitaajiri vijana kama 6, vijana ambao Mwanasheria, nitaajiri *Human Resource Manager*, watu wa *accounting,* watu wa *research,* yaani watu mbali mbali ambao ninaamini wakiweza kuutumia ujuzi wao kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, kwa sababu hiyo Kampuni tukeshaianzisha itabidi lazima tutafute namna ya kuanzisha ile Kampuni na ule mtaji mimi mwenyewe *capital* ninayo ya kuanzishia.

Kwa hivyo, tunaamini vijana hawa wakiweza kufanya kazi yao vizuri, kwa sababu hapa nilieleza Mhe. Mwenyekiti, katika hizi ajira za nje ya nchi ambazo nyingi vijana wetu wamezipata, katika zile *connection* ambazo nilizokuwa nazo mimi bado hamjaingia katika soko hili; Mheshimiwa kuna soko la Canada sijaliona hapa, mimi tayari ninalo mkononi, kuna soko la Qatar hapa sijaliona, ninalo mkononi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii Kampuni ikianza tu na mimi nategemea ndani ya mwaka mmoja unaokuja basi katika kitabu chako itaweza kuonesha ukiacha hizi ajira ulizozitaja, kutakuwa kuna ajira nyengine mpya ambazo ziko katika nchi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati na mimi niliwahi kupata elimu ya ujasiri amali na nilipopata elimu ya ujasiri amali kitu ambacho nilichoambiwa kwamba usiwe mchoyo, unapotaka kutafuta usiwe mchoyo, tafuta na wenzako ambao waliokuzidi kielimu na taaluma uweze kuwapa kazi wataweza kusaidia na ndiyo *process* ambayo tuliyoianza.

Mhe. Mwenyekiti, katika mipango hiyo Mhe. Waziri, ninakuomba sana ndani ya Jimbo langu la Kwamtipura tayari tumeanzisha Chuo cha Amali. Tumeanzisha Chuo cha Amali na leo hii kabla ya kuja hapa tayari nilitoka hapo Chuoni kwenda kukabidhi gari, hatuzungumzi vitu vya mas-hara mas-hara. Kwa hivyo, tunategemea pale katika Chuo chetu tutazalisha madereva wengi, hivi sasa hivi tuna madereva karibu 60 wanasoma pale vijana wabichi kabisa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, nitaomba kwa nafasi yako kwa wakati wako kama kawaida yako utafute namna uje utembelee kile Chuo, uje uwape nasaha halafu uje uwape matumaini ya baadae. Kwa sababu masuala ya ajira hatutaki sana tuangalie lazima ajira ziwe Serikalini, sasa hivi *Private Sectors* imeajiri watu wengi sana. Na pale Mhe. Mwenyekiti, tuna fani karibu 7; tuna fani ya udereva, tuna fani ya upishi, tuna fani ya ushoni, tuna fani ya mambo ya *electronic*, mambo ya *electricity*, mambo mengi sana pale tunajifunza mpaka mambo ya uchoraji, mpaka uchoraji biarusi pia atakuwa anachorwa pale pale ndani ya Chuo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hawa vijana ambao tumewasomesha mambo ya uchoraji wa hina, kuna mahoteli mangapi sasa hivi yanavyokuja wazungu wanataka kuchorwa hina, kwa hivyo, tutatoa vijana tutaanza kuwapeleka katika soko la ajira pale pale. Lakini naamini ujio wako utaweza sana kuja kutusaidia vijana wetu wale kuwapa moyo ili waendelee kujifunza.

Chengine nilichokuwa nataka kukisema naomba sana Mhe. Waziri ujaribu kukaa na Waziri wa Elimu hasa hii Bodi ya Mikopo, Bodi ya Mikopo Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho tunachokiona sasa kuna vijana wengine pale wanakwenda wanasoma wanapata mkopo wanasoma, lakini wakishamaliza kusoma inakuwa ajira hawana. Sasa nilikuwa naomba Mhe. Waziri kwa kuwa wewe masuala ya kazi yako chini ya dhamana yako, hebu tuangalie tuna mapungufu ya aina gani katika maeneo gani katika sekta ya ajira hasa katika sekta ya taaluma.

Mfano Mhe. Mwenyekiti, katika masuala ya *Hotel Management,* sijui kama Chuo chetu cha Hoteli na Utalii kama tayari sana hivi kinatoa *degree* ya *Human Recource*, sijui kama tumeshafikia *level* hiyo. Kama hatujafikia basi nadhani iko haja na wakati umefika ili hizi kelele za Waheshimiwa zipungue kuhusu ajira kwenye mahoteli, lazima tuwasomeshe wataalam wetu *at least* katika ngazi ya *degree* na kwenda katika *masters* halafu tuangalie, je, *Private Sectors* kama hayo mahoteli hawatoweza kuajiri. Lakini kama hatuna pale Chuo cha Hoteli na Utalii tuangalie mpaka sasa ngazi ya *diploma* ninajua tayari ipo, sasa sijajua baada ya ngazi ya *diploma* kama *degree* wameshaingia lakini kuendelea mbele vile vile. Sasa kama hawapo basi wale ambao tayari wamepata *degree* waweze kupata mkopo wa elimu ya juu ili waweze kujiendeleza wapate *masters* na nyengine ili waweze kuja kushika hatamu katika hayo mahoteli makubwa ya kitalii.

Tunaishukuru sana Serikali yetu sasa hivi kila siku ukicha mahoteli makubwa ambayo yana uwezo ya kuleta watu wenye kutumia pesa nyingi yanajengwa. Lakini sasa hiyo changamoto ya ajira kama huna *Human Resource Manager* ambaye anajua mazingira yetu ya kizanzibari na namna ya kuweza kuishi nao hawa kwa kweli inakuwa ni mtihani na ndio maana kila siku itakuwa migogoro haishi. Mhe. Mwenyekiti, naamini Mhe. Waziri ukiweza kukaa na Bodi ya Mikopo

kuangalia zile changamoto hasa katika nafasi za juu katika *Private Sectors* basi itaweza kusaidia sana katika kutoa elimu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, ninakuja katika hii *vote* namba mbili, maana yake ninachangia bajeti hii ya nyuma lakini naingia vile vile na hii bajeti mpya inayoangalia programu. *Vote* 02 Kamisheni ya Utumishi ya Umma. Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi tumepiga kelele sana kuhusu Kamisheni ya Utumishi wa Umma na mimi kuna maeneo bado nitaendelea sana kuyapigia kelele kwa sababu.

Mhe. Mwenyekiti, ninakuja katika suala la Vikosi vya SMZ. Pamoja na *scheme* tumeambiwa imepelekwa lakini *scheme* yao imetiwa mikono sana. Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika sekta ambazo zinatakiwa ziwe na maslahi bora za kutosha ni hizi Idara zetu Maalum. Kwa hivyo, naomba sana Kamisheni ya Utumishi wa Umma wasiangalie Idara Maalum kama Idara nyengine za Serikali, wale mazingira yao sio watu, wale majeshi. Na kwa sababu ule wakati ukitokezea ile gharki sisi tunaingia ndani kujificha mvunguni na wao ndio wanatoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, waswahili wanasema; "aisifiae mvua basi imemnyea". Mhe. Mwenyekiti, tuangalie majirani zetu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ndugu yetu ule kijana wetu Nkururinza tayari watu walikuwa wameshamuweka nje ya uwanja, nani aliyemrejesha pale? Lazima tujiulize, kwa hivyo, sisi pamoja na suti zetu hizi na jeuri yetu hii wale jamaa wakichachamaa hapakaliki hapa, lakini wale ndio waokozi wetu.

Sasa naomba sana Mhe. Wazairi ukae na Waziri wa Idara Maalum. Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma uangalie Idara Maalum na hili Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema safari hii ninajua mmepanga mipango yenu kwa ajili ya kujiandaa, tunapitisha hii na tunakupeni, tunakuwekeni katika viti hivyo hivyo mlivyokaa, katika watu wa mwanzo wa kuja kuboreshewa maslahi yao Mhe. Waziri, iwe Idara Maalum. Leo Mheshimiwa, askari wetu akikutajia Cheo chake na mshahara wake kamaliza, ni aibu, mtu ana maperemende humu, matepe makubwa makubwa lakini mfukoni mfuko uko bapa.

Mhe. Mwenyekiti, sisemi itakuja kutokezea kama ya Nkururinza, aa, hapa kwetu ninaamini sisi tunaishi katika hali ya ustaarabu, lakini hawa ndio waokozi wetu wakubwa, kwa hivyo, mimi naomba na Mhe.Waziri wa Utumishi wa Umma mimi bajeti ya mwakani tukijaaliwa na uhai na Mwenyezi Mungu akituweka katika meza hizi hizi na *Inshaallah* atatuweka, kitu cha mwanzo nitakuja kuhoji maslahi ya watumishi wa Idara Maalum yameboreshwa vipi. Hii ambayo *scheme* iliyopitishwa sasa hivi inapita lakini mimi bado sijaridhika nayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakutolea mfano, kuna vijana wetu hawa JKT.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, dakika zako zimemalizika.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ningelitegemea leo ungenipa angalizo, lakini unanikatisha moja kwa moja lakini kwa kuheshimu kiti chako na kwa kuwa nilileta tangu asubuhi, lakini nilikuwa na kazi maalum ambayo unaijua, ninakushukuru sana lakini Mhe.Waziri tu hii *vote* 02 bajeti ya mwakani kama maslahi ya wafanyakazi wa Idara Maalum maarufu Vikosi vya SMZ haikuzingatiwa, kwa kweli mimi nitakuja kuning'inia sana hapa sitokubali kwa sababu *scheme* yao ipo imetiwatiwa mikono mikono, kwa sasa hivi tunaridhika kutokana na hali ya mambo, uchaguzi na mambo mengine, utawala bora na nini. Lakini tukishamaliza mwakani hakuna uchaguzi hakuna mambo mengine sasa yale yarejeshwe ili maslahi yao yatune.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache ninakushukuru, ninakupongeza sana na ninaunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo:** Ahsante sana Mwenyekiti, ninakushukura naogopa dakika zangu zisishe, kwa hivyo, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda moja kwa moja kwenye kitu kidogo nina uzoefu nacho na ninakifahamu, nayo ni hii Idara ya *e-government.* Idara hii naweza kusema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina nia njema kubwa sana kuja na kitu kama hiki na wengi hawafahamu, kwa hivyo, mimi nitajaribu kutoa ufafanuzi wa kitu gani kilichowekwa pale ambacho kipo hivi sasa na kitu ambacho kinaweza kufanyika ili yale yaliyozungumzwa humu ndani yakaweza kupatikana.

La kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti, *e-government* ni *phases* mbili; *Phase* ya kwanza ni kuweka mashine zile wenyewe, yaani *hardware* na ndio kitu ambacho Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutiliana mkataba saini na Serikali ya Watu wa China, imetoa tenda ile wakashinda walioshinda ile tenda na ndio imewekwa miundombinu ya *hardware,* yaani pale kuna *sarver,* kuna *infrastructure,* kuna *table* zile ambayo *fiber optic cable* imezunguka naweza kusema nchi nzima katika visiwa vyote viwili Unguja na Pemba. Hata wenzetu Bara tumewashinda hawana kitu hiki, ukenda baadhi ya Mikoa hakuna miundombinu siku hizi ndio inaitwa miundombinu yaani *infrastructure*. Sasa tatizo lilokuwepo hapa sisi tayari tumeshatandika barabara na ile barabara ni kubwa naweza kusema ni *super high way* kwa sababu yanaweza kupita magari manne huku, magari manne huku.

Sasa hiyo *phase II* tunayotakiwa kwenda sasa hivi, ndio maana mimi kidogo nikamshangaa Mhe. Waziri, hapa bajeti hii haitoshelezi kwa kweli kwa *phase II*. Hii ni *operational budget* labda atakuja kuweka sawa Mhe. Waziri, mwenyewe akija, hii ni *operational budget* ya kukiendesha kile ambacho kipo tayari pale hizi milioni tisiini na kitu hizi ni *operational budget* za kuendesha kile ambacho kimewekwa tayari. Lakini kitu kinachohitajika sasa ni *software* njia ushawekea lakini huna magari, sasa hatua ya pili nawaomba wajumbe pamoja na kiti chako Mwenyekiti, tui-*support budget* hii ili Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, akishirikiana na Waziri wa Fedha aweze kwenda kwenye *Phase II*, *Phase II* anaweza akapata yoyote yule si lazima yule yule anaweza akapata yeyote ambaye ataweza kuweka ile miundombinu sasa ya *software*, yaani miundombinu ya pili.

Itakapowekwa miundombinu ya pili ndio haya yote yaliyoandikwa humu nilikuwa nikisoma kwamba tutaweza sasa sisi kubadilishana barua pepe na Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mhe. Mohammed Aboud, itakuwa haihangaiki tena kuja na ma-*documents* na mabarua hapa Baraza la Wawakilishi, kwa sababu Baraza la Wawakilishi litaweza moja kwa moja kuzungumza nayo Ofisi na Mhe. Rais mwenyewe ataweza kupata ripoti ya nchi nzima juu ya meza yake kwa *click off finger,* yaani kubonyeza *button* moja ataweza kupata kila kitu na ndio zinavyotumika hizi mambo ya *e-government*. Singapore wameshafanikiwa wameweza na wako mbali na sisi tume-*copy* mfano wao wa Singapore. Kwa sababu wakati haya yanakuwa *designed* wataalam wetu ninakumbuka vizuri walikwenda Singapore kutazama *system* gani iliyokuwepo kule wameona na kwa kweli ni jambo jema sana ambalo tumelifanya.

Sasa mimi ninamuomba Mhe. Waziri hii *phase II* aihimize kwa sababu na mimi *interested part* kwa *phase* II na nitaeleza kwa nini *interested part* kwa *phase* II. Kwa sababu *phase II.* ina *e-education*, *Electronic Education* kwa lugha nyengine, yaani elimu kwa njia ya mtandao. Ina *e-health,* yaani afya kwa njia ya mtandao. Na afya kwa njia ya mtandao ni jambo moja muhimu sana kwa sababu hapa masuala yote tunayoulizwa kila siku, mimi ndie ninayejibu hapa maswali, haji *doctor* kutoka Mnazimmoja, wala kutoka Muembeladu wala kutoka Kidongo Chekundu ila ninajibu mimi maswali yote hayo.

Yale ikishawekwa hii *e-health* itaweza kutusaidia kupunguza hasara kubwa kwa Serikali kwanza kwa kuwapeleka wagonjwa kila siku, sasa tutaweza kuwasiliana nao mahospitali yote duniani yakiunganishwa ambayo mengine tayari yameshaungana katika mtandao huu madaktari wetu wataweza moja kwa moja kuwasiliana ili waweze kufanya *consultation*.

Mpaka sasa hivi kitengo cha *neurosurgery* kwa pale Mnazimmoja ndio pekee wale Waspanish wameunga unga *system* yao kidogo wanaweza wale wagonjwa wao wanaowafanyia *operation* wanaweza kuwa-*monitor* kwa sababu wanafanya *operation* ya vichwa maji pamoja na uti wa mgongo. Kwa hivyo, wale hivi sasa wanaweza wagonjwa wao wakishaondoka, wakishawafanyia wanaweza ku-*monitor* wagonjwa wao vipi hali zao, vipi wanaendeleaje wanaweza kupata zile ripoti za picha, wanaweza kupata ripoti za *scan* na kadhalika.

Kwa hivyo, imepunguza sehemu kubwa sana, la sivyo wagonjwa wale wote ingebidi sasa tuwasafirishe kwa wale wale madaktari waliowafanyia *operation* Spain na kwa uwezo wetu tusingeweza, tuambizane ukweli, kwa uwezo wetu tusingeweza kufanya hivyo. Kwa hivyo, kwa *system* hiyo ikipatikana *e-health* nayo itaweza kwa sehemu kubwa sana kutatua matatizo ambayo sisi Wizara ya Afya tunayo.

Lakini katika *system* hiyo hiyo kuna *e-tax*, *e*-tax kwa mshahara wako wewe Mwenyekiti, ndio mshahara wangu mimi niliokaa huku, ndio mshahara wao wote waliokaa *back bancher* maana sisi wengine tuko katikati hapa, ndio mishahara yetu na ndio bajeti yetu. Kwa sababu bajeti yetu fungu kubwa kabisa maana safari tumeona ile mia nne na kitu imewekwa mbali na ile itakayokuja huko baadae baada ya mikwamuko kuja imeweka mbali.

*Almost fifty fifty* nikitia hizi *percent* kama nitakuwa sijakosea 58.2% ambayo 80% *plus* inatokana na *e-tax*. Kwa hivyo, hakuna mfumo muhimu sana kama *e-tax*. Kwa hivyo, *e-tax* ndio itaweza kutusaidia kutuletea madawa, tutaweza kununua madawa kwa wakati, *e-tax* ndio hayo malalamiko ya Wawakilishi wote humu wanaolalamika kila siku kwamba dawa zinachelewa, hiki kinachelewa, hakuna usafiri, wafanyakazi kuajiriwa wa nyongeza, yote haya yatatokana na pale panapokuwa na mshiko.

Kwa hivyo, huwezi ku-*plan* kutumia bila ku-*plan* kwanza kupata kuwa nacho mkononi, lazima u-*plan* kupata. Na *plan* nzuri ya kupata ndio *e-tax system*, sasa kutakuwa na *system* ambayo imeunganisha na mitandao, hayo mahoteli, hawa walipa kodi wakuu wote, Kampuni za mafuta na Kampuni za Simu zote zitaweza kuunganishwa huu mtandao moja kwa moja. Kwa hivyo, *ZRB* ataweza ku-*monitor* moja kwa moja *revenue* inayoingia hata kabla ya kwenda kudai kule au wale kujaza fomu zao za *tax return* mwisho wa mwaka.

Kwa hiyo, naendelea kusisitiza na baada ya hapo ndio mengine yote yatakuja baada ya hii *e-tax* itakuja *e-tourism*, itakuja *e*-mengineyo na hayo *e*-mengineyo ndio mwisho wake, *the end product* ndio *e-government* au *e-governess system*. Kwa hiyo, kwa sasa hivi hatuna bado *e-governess* tuna *infrastructure*. Naomba hili

tumsaidie sana Mhe. Waziri, maana tusipigie mabuti wakati kile kitu yeye hatujamuwezesha au hatujampa. Tusipige mabuti katika vifungu vyake wakati ile *software* pengine ni *CD* moja tu, lakini gharama zake kuna gharama zake hiyo *CD* ambayo itakuwa na *e-health, e-tax, e-tourism, e-education* na kadhalika.

Sasa mimi ningependa kuomba Baraza na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwamba hivi sasa hivi madamu hii miundombinu tumeshaweka tumuombe Mhe. Waziri akae na Mhe. Waziri wa Fedha waweze kufanya haraka katika hiyo *Phase II,* hata wale waliokuwa wanaweka ile miundombinu wa *Phase I* walikuwa wanajua kwamba kutakuwa na *Phase II* inakuja. Hata hawa watendaji wetu sisi tukiwabana sana, tukiwalaumu sana inakuwa hatuwasaidii, tunachotakiwa kuwasaidia Baraza litoe tamko rasmi kwamba Mhe. Waziri sasa nenda kaikalie *Phase II,* ule mkopo ambao baadhi ya wajumbe waliokuwa wamesema kwamba tumekopa watoto, wajukuu zetu, vitukuu vyetu tukiweka kuanzia kwenye *Phase II* hatuna haja hata vitukuu, wala vijukuu sisi wenyewe ule mkopo utakwisha.

Kwa sababu ile *e-tax system* itaweza kufanya kazi vizuri na kuweza ku-*collect* pesa vizuri na fedha zetu zikaongezeka zikawa marudufu, na Mwenyezi Mungu akitujaalia huko mbele tunakokwenda *Inshaallah* mambo ya Katiba haya yote yamekwenda vizuri, mbele tunakokwenda mafuta, gesi, gesi asilia na gesi nyenginezo zote hizi zinategemewa kuleta *revenue*.

Sasa kama *system* hii haikuweza kufanyishwa kazi sasa hivi au haikuweza kufanya kazi, mimi namuomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Maalim Haroun maana yake ni Mwalimu wangu huyu. Mhe. Maalim Haroun ili kuondokana na haya yote mazungumzo yote na kuondokana na lawama nakuomba sana uhimize *Phase II,* kwa sababu *Phase II* itatuokoa pia maisha yetu, kwa sababu tukiweza kupata *e-health* sisi, mimi naelewa pale matatizo tuliyokuwa nayo pale Wizara ya Afya, masuala hapa kila siku tunapigwa lakini naelewa matatizo yaliyokuwepo pale. Tukiweza kupata *Phase II* naweza kusema robo au robo na robo nyengine tena nusu tutakuwa tumepunguza yale matatizo.

Kwa hiyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, sijui nimebakisha dakika ngapi? Ninachotaka kusema upande wa *human resource* hayo yote kwenye kitabu hiki kuna masuala ya *human resource,* yaani *scheme of services,* serikali inavyopanga *human resource allocation,* naamini serikali ndio mwajiri mkuu kwa hapa Zanzibar, lakini zikiweza kupatikana hizo *systems* kwa hao wafanyakazi waliokuwa wanafanya kazi watajuulikana, *scheme of services* zao zitajuulikana na pale wanapohitaji *promotion* au kwenda kusoma au kwenda kuongeza elimu au kupangiwa cheo baada ya kurudi kusoma mtu anatakiwa kupandishwa cheo, basi kwa *systems* kama hizi itawezekana.

Kwa hiyo, kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, nikiwa huku naunga mkono hoja kwa asilimia 100, mimi naomba sana Wajumbe tumetembelea mara nyingi, mimi kabla sijakaa nafasi hii nilikuwa katika Kamati ya Katiba na Sheria tumetembelea pale, wajumbe wameuliza masuala mengi sana, Mwenyekiti wewe ni Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, maana ile sehemu imegawika sehemu tatu.

Nakumbuka kile kitabu cha Bwana Msa wanasema "mke mmoja waume watatu", ndio ile idara ile ina waume watatu. Mume wa kwanza Maalim Haroun ndiye mume maana yake anaye-*on* nyumba ndio imo kwenye kitabu chake. Lakini mume wa pili ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano utanisahihisha Mwenyekiti maana wewe ndiye Mwenyekiti, Mwenyekiti hapa na Mwenyekiti huko pia. Mume wa pili ndiye huyo Wizara ya Miundombinu kwa Mhe. Juma Duni Haji, Mwalim Mkuu wangu alikuwa Lumumba pale. Na mume wa tatu ni Wizara ya Fedha hata ile *structure* yao ya *steering committee* inaonesha waume watatu, si wanakaa Makatibu Wakuu watatu wale.

Kwa hiyo, inaonesha *structure* yake kwamba iko hivyo, sasa ni mke mmoja waume watatu. Mimi nasema mke huyu ana bahati kwa sababu kajaaliwa bahati, waume watatu yule ninayemwambia ashirikiane nae mmoja ni Waziri wa Fedha, Mhe. Juma Duni Haji, nimemsahau kidogo naomba na yeye pia awemo katika ushiriki huu kwa sababu Katibu Mkuu wake anaingia katika *steering committee*.

Kwa hiyo, tukiweza kukamilisha *Phase II* eneo kubwa tayari kazi kubwa tayari imeshafanyika, *fiber optic* imefika tulikwenda sisi kutembelea mpaka Kaskazini kule, Vumawimbi, nani aliyekuwa anafikiria kwamba leo Vumawimbi itakuwa na *fiber optic infrastructure* nani katika ndoto alikuwa anafikiria, Vumawimbi eeh, *remote area* ya *North Pemba* huku Micheweni ndio wameshapita maana kituo kile cha redio jamii pale inapita pale pale *fiber optic*. Kwa hiyo, tukiweza kuweka na hii *software* hata *TV* yetu itaweza, kuingia redio yetu, *internet* na serikali itaweza kufanya mambo mengine chungu nzima. Lakini nataka kuongezea moja miundombinu hii tukiitumia vizuri sisi serikali tutatumia asilimia 5 mpaka 10 *maximum* kumi hatuwezi kuzidi kumi, asilimi 90 itakuwa imebakia bakaa tu, ile asilimia 90 sisi tuna uwezo wenzetu Bara tayari wanauza *infrastructure* yao, *TTCL* wanaita *back born*. *TTCL* sasa hivi tayari *back born* wanatumia kama asilimia 20, asilimia 80 wanawauzia wengine.

Tukiweza kuuza *capacity*, sisemi kuuza *infrastructure* aah, nisielewe ivyo, yaani kukodisha ile *capacity, extra capacity,* upande wa ki-*technology* wanaitwa *band venue,0* tukiweza kuuza hiyo *capacity* hata hizo fedha tulizokopa zitaweza kurudi *within no time* tunaweza kurudisha. Kwa sababu *capacity* ile wenzetu wanakodishana kwa dola tena si dola kidogo ni dola nyingi, kuanzia dola 200,000 mpaka 300,000 kwa mwezi.

Sasa ukipata *operators* kama 10 wewe unaongelea dola 3,000,000, dola 3,000,000 ndani ya kipindi cha miaka mitatu ushalipa kila kitu, huna haja ya kusubiri mtoto mzae mpaka mjukuu, mpaka kitukuu huna haja inawezekana. Sasa *infrastructure* tunayo Mhe. Maalim Haroun *infrastructure* unayo lakini umeikalia, ndio sawa sawa na kusema uchumi unao lakini umeukalia, kwa sababu ule ni uchumi kamilifu ambao leo nchi yetu pia nayo inaweza kufaidika baada ya kufanya *deployment* ama kufanya *implementation* ama kufanya utekelezaji wa hiyo *e-government infrastructure*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ya kwangu ni hayo nawaomba wakubwa zangu mawaziri hawa watatu wakae pamoja tuelekee kwenye *Phase II* tuanze kwa nia njema ya Rais wetu aliyeleta mradi huu na hiyo ilani iliyotajwa ndio iliyoleta mradi huu na serikali hii, basi inaweza ikakamilika mradi huu *within no time*. Na hao waliokuwa na *interest* wako tayari, kuna makampuni tele, makampuni kadhaa wa kadhaa ambao wako tayari kufanya *Phase II* na Mhe. Mwenyekiti, *Phase II* sio tena kuchimba ile mitaro na misingi na mapauro, hapana ni *CD* moja tu pengine inaweka kwenye *saver* tunamaliza kazi. Naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Naibu Waziri ambapo kwa leo umetupa darsa ya kutufundisha malengo na hoja nzima kuhusu *e-government* tunashukuru kwa mchango wako huo kwa wizara hii.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa orodha ambayo nilikuwa nayo ya wachangiaji tumemaliza, tumemaliza na Mhe. Naibu Waziri wa Afya ambapo kwa leo alitupa taaluma ya *e-government*. Sasa kilichobakia ni nafasi ya Mhe. Waziri, ili kuja kutoa majumuisho yake, lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu Mhe. Waziri alikuwa anapaswa kupata masaa sita ili aweze kufanya uwiano wa nyaraka zake pamoja na zile hoja hatimae aweze kutujibu hoja zetu.

Na dakika tulizobakiwa nazo mpaka sasa si zaidi ya dakika 40, kwa msingi huo basi nahisi tutampa fursa Mhe. Waziri ili aende akakae na watendaji wake na kesho asubuhi baada ya taratibu zetu Mhe. Waziri, atakuja kujibu hoja za Wajumbe na hatimae kuweza kupitisha vifungu kama zilivyo taratibu. Baada ya maelekezo hayo sasa niwaombe kuahirisha Baraza hili hadi kesho tarehe 27/05/2015 saa 3:00 za asubuhi, naomba kuahirisha.

*(Saa 1:12 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 27/05/2015 saa 3:00 asubuhi)*